Sh 3,000/-

# USAWAZISHAJI WA USEMI KATI YA WAASIA NA WAAFRIKA KATIKATI MWA JIJI LA NAIROBI

NA

NELLY NZULA KITONGA

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA

**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA**

**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**JUNI 2005**

Nelly Nzula Kitonga
*Usawazishaji wa usemi kati ya waasia*
05/277405

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine.

NELLY NZULA KITONGA

Tarehe 20/6/2005

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu.

PROF. I. MBAABU

Tarehe 22/06/05

na

DKT. P. MBATHA MATHOOKO

Tarehe 22/06/05

**TABARUKU**

Naitabaruku kazi hii kwa watoto wangu wapenzi Benjamin Kitonga na Ann Kitonga.

**SHUKRANI.**

Ninawashukuru wasimamizi wangu Prof. I. Mbaabu na Dkt. P. M. Mathooko kwa kunipa mwongozo, ushauri na usaidizi ulioniwezesha kuimaliza kazi hii.

Nawashukuru pia wahadhiri wangu wote katika Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika kwa kuniongezea maarifa na kunitia moyo masomoni.

Ningependa kuwashukuru wenzangu, Mary Muigai, Ann Munuku, Jacinta Mwangi, Stephen Kamau, Agnes Savala na wengine ambao tulianza nao safari hii ya usomi kwa kuniongezea maarifa, kunitia moyo wa kuendeleza kazi hii na kuniombea.

Ninamshukuru sana mume wangu James Kitonga kwa kunitia moyo masomoni, watoto wetu Benjamin Kitonga na Ann Kitonga kwa kunivumilia, na Bi. Naomi Katunge kwa kuwatunza watoto wetu nikiwa masomoni.

Natoa shukrani zangu kwa Esther Mutua kwa bidii na kujitolea kwake kuipiga chapa kazi hii.

Zaidi ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa neema, afya na uwezo wa kuendeleza masomo .

**IKISIRI**

Utafiti huu wa isimujamii unachunguza usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika katikati mwa jiji la Nairobi. Unajikita katika maingiliano ya kikazi pale ambapo Waasia ni waajiri na Waafrika ni wafanyakazi na wateja katika maduka ya Waasia hao. Lengo la uchunguzi huu ni kubainisha namna ya usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika, kuchunguza, kutambua na kueleza viwango vya kiisimu hasa vya kisemantiki na kisintaksia vinavyobadilishwa wakati wa utaratibu wa usawazishaji wa usemi. Aidha utafiti huu unanuia kufafanua sababu zinazowamotisha Waafrika na Waasia kubadilisha usemi wakati wa maingiliano ya ana kwa ana.

Waafrika na Waasia walibadilisha mtindo wa usemi ili kuonyesha mwingiano na ujitengaji. Mwingiano na ujitengaji kiusemi ulisababishwa na uchaguzi wa lugha wa kipekee, uchaguzi wa lugha usio wa kipekee na uchaguzi wa lugha wa kubahatisha, na uzingativu wa muundo wa sentensi .Wazungumzaji wanaonyesha mwingiano iwapo wanatafuta kukubalika, kueleweka, kuwa sawa na wasikilizaji, kupunguza gharama kiusemi na kuzidisha manufaa yanayotarajiwa. Watajitenga kiusemi kama njia ya kujitambulisha kijamii, kuonyesha kutokubaliana na mada ya mazungumzo na pia kutaka kuwa tofauti na wasikilizaji.

Kazi yote iligawanywa katika sura tano: Sura ya kwanza ni usuli wa utafiti, swala la utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu za kuchagua mada, mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti. Sura ya pili inafafanua msingi wa nadharia, launi ya Kiswahili ya Waasia na lugha ya Kiswahili. Katika sura ya tatu,

usawazishaji wa usemi katika kiwango cha semantiki umefafanuliwa pamoja na uhusiano wake na nadharia za Upekee na Usawazishaji Usemi. Sura ya nne inatoa maelezo ya namna inavyokuwa wakati Waasia na Waafrika wanapojisawazisha kiusemi katika kiwango cha sintaksia kwa msingi wa nadharia za Sarufi Miundo Virai, Upekee na Usawazishaji Usemi. Mwisho, sura ya tano inahusu muhtasari, matokeo, mahitimisho na mapendekezo yanayojitokeza katika utafiti.

Kupitia nadharia ya Usawazishaji Usemi na nadharia ya Upekee utafiti huu umebaini kwamba Waasia na Waafrika wanabadili lugha kwa sababu za kiuchumi na kisaikolojia.

YALIYOMO

**Mada** **Ukurasa**

Ungamo ........................................................................i

Tabaruku ........................................................................ii

Shukrani ........................................................................iii

Ikisiri ........................................................................iv

Yaliyomo ........................................................................vi

Ufafanuzi wa Dhana........................................................................x

Vifupisho ........................................................................xii

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi........................................................................1

1.1 Usuli wa Utafiti........................................................................1

1.2 Swala la Utafiti........................................................................5

1.3 Maswali ya Utafiti........................................................................7

1.4 Madhumuni ya Utafiti........................................................................7

1.5 Nadharia Tete........................................................................7

1.6 Sababu za Kuchagua Mada........................................................................8

1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti........................................................................9

1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada hii........................................................................9

1.8.1 Tafiti Nchini Kenya Zinazohusiana na Utafiti huu........................................................................10

1.8.2 Lugha za Waasia........................................................................11

1.8.3 Lugha ya Kiswahili........................................................................13

1.9 Mbinu za Utafiti....13

1.9.1 Ukusanyaji wa Data....14

1.9.2 Uchanganuzi wa Data....15

1.9.3 Uwasilishaji wa Data....15

SURA YA PILI

2.0 Utangulizi....16

2.1 Msingi wa Nadharia....16

2.1.1 Nadharia ya Usawazishaji Usemi....18

2.1.2 Nadharia ya Upekee....22

2.1.3 Nadharia ya Sarufi Miundo Virai....27

2.1.3.1 Sarufi....27

2.1.3.2 Sarufi Miundo....27

2.1.3.3 Mikabala ya Uchambuzi wa Sarufi....29

2.1.3..4 Nadharia ya Sarufi Miundo Virai....29

2.2 Launi ya Kiswahili ya Waasia....34

2.2.1 Utangulizi....34

2.2.2 Fonolojia katika launi ya Kiswahili ya Waasia....36

2.2.3 Mofolojia katika launi ya Kiswahili ya Waasia....39

2.2.4 Sintaksia katika launi ya Kiswahili ya Waasia....42

2.3 Lugha ya Kiswahili....47

SURA YA TATU

3.0 Utangulizi....51

3.1 Usawazishaji wa Usemi katika Kiwango cha Semantiki....52

3.2 Sifa Bainifu katika Usawazishaji wa Usemi wa Kisemantiki........................89

3.3 Hitimisho........................................................................................95

SURA YA NNE

4.0 Utangulizi.........................................................................................96

4.1 Muundo wa Sentensi katika Lugha ya Kiswahili....................................97

4.2 Muundo wa Sentensi katika Launi ya Kiswahili ya Waasia........................101

4.3 Usawazishaji wa Usemi katika Kiwango cha Sintaksia..............................106

4.4 Hitimisho.........................................................................................139

SURA YA TANO

5.0 Muhtasari, Matokeo na Mapendekezo...................................................141

51. Utangulizi.........................................................................................141

5.2 Muhtasari wa Utafiti..........................................................................141

5.3 Matokeo na Mahitimisho.....................................................................141

5.4 Mapendekezo ....................................................................................144

MAREJELEO ........................................................................................146

VIAMBATISHO......................................................................................151

MAZUNGUMZO KUHUSU USAWAZISHAJI WA USEMI..........................151

Kiambatisho 1

Mwingiano............................................................................................151

Kiambatisho 2.

Ujitengaji...............................................................................................152

Kiambatisho 3.

Uchaguzi wa Lugha wa Kipekee........................................................152

Kiambatisho 4.

Uchaguzi wa Lugha Usio wa Kipekee....................................................154

Kiambatisho 5.

Uchaguzi wa Lugha Bahatishi............................................................155

Kiambatisho 6.

Maswali ya Mahojiano Yasiyo Rasmi.....................................................155

## UFAFANUZI WA DHANA

**Usawazishaji wa usemi** - Huu ni urekebishaji wa usemi kati ya wazungumzaji ili kuwa sawa na wasikilizaji. Unajitokeza wakati mtu anapobadilisha jinsi ya kuongea ili awe sawa na wasikilizaji.

**Mwingiano** – Huku ni ama kujinasibisha au kuwa sawa kiusemi. Kunajitokeza katika hali mbili:

(a) Mwingiano – juu – Ni ile hali ya mzungumzaji wa hadhi ya chini kujisawazisha kiusemi na msikilizaji wa hadhi ya juu.

(b) Mwingiano – chini – Ni ile hali ya mzungumzaji wa hadhi ya juu kujisawazisha kiusemi na msikilizaji wa hadhi ya chini.

**Ujitengaji** – Ni ile hali ya kujitofautiasha kabisa baina ya mzungumzaji na msikilizaji kupitia kwa matumizi ya lugha za kwanza, lafudhi au ishara zinazowatenga wengine.

**Upekee** – Ni ile sifa ya lugha iliyo kawaida, ya kijumla na isiyopendelea upande wowote. Upekee unajitokeza katika hali mbili:

(a) Uchaguzi usio wa kipekee – Ni uchaguzi wa lugha wa kawaida, unaotarajiwa na ambao unazingatia kanuni za kijamii.

(b) Uchaguzi wa kipekee – Ni uchaguzi wa lugha usiotarajiwa.

**Lugha mawasiliano** – Ni lugha inayotumika kwa mawasiliano katika eneo lenye lugha nyingi tofauti kama vile Kiswahili katika Afrika Mashariki

**Launi za lugha** – Ni namna tofauti za matumizi ya lugha kutegemea mazingira, muktadha, lahaja, n.k.

**Waasia** – Ni watu wa nchi za Mashariki au pande za Asia, zaidi ni watu wa asili ya Pakistani na Bara Hindi.

**Viziada lugha** – Ni sifa za usemaji kama vile mpumuo, kupunguza au kuongeza kasi katika usemi ambazo si sehemu ya mfumo wa lugha.

VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| K | Konsonanti |
| k | Kiyeyusho |
| KV | Konsontanti Vokali |
| S | Sentensi |
| KN | Kirai Nomino |
| KT | Kirai Kitenzi |
| KE | Kirai Kielezi |
| KV | Kirai Kivumishi |
| KU | Kirai Kiunganishi |
| V | Kivumishi |
| E | Kielezi |
| N | Nomino |
| T | Kitenzi |
| U | Kiunganishi |
| WKT | Wakati |
| n.k | Na kadhalika |

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Usuli wa Utafiti

Ulumbi huchukuliwa kama hali ya kisaikolojia ya mtu ambaye anaweza kutumia lugha mbili au zaidi katika mawasiliano yake na wengine (Hammers na Blanc, 1982). Mawasiliano kwa kutumia lugha (na lahaja) mbili au zaidi huhusu makundi ya watu wanaotumia lugha zinazotofautiana.

Sifa moja ya mawasiliano kwa kutumia lugha nyingi ni kule kubadili msimbo, ambako kunafafanuliwa kama kubadilisha kutoka lugha moja hadi nyingine tofauti katika mawasiliano (Grosjean,1982).

Usimbaji na usimbuaji wa lugha katika mawasiliano kwa kutumia lugha nyingi hutegemea sana mwingiliano wa hali za kaida au kanuni za maingiliano, hali za kumotisha na hali za muundo wa jamii.

Hali za kanuni za maingiliano kama zinavyofafanuliwa na wanaisimujamii huhusu kaida za kubadili msimbo kulingana na mkao wa jamii ambamo mawasiliano yanatokea, madhumuni ya mawasiliano na sifa za wazungumzaji (Hymes, 1972; Trudgill, 1974). Hali za kumotisha mawasiliano kama zinavyoelezewa kupitia nadharia ya Usawazishaji Usemi hufafanua kubadili msimbo kulingana na kinachomotisha mzungumzaji, mtazamo wa mzungumzaji, utambuzi wa mzungumzaji na uaminifu katika kikundi.

Hali za muundo wa jamii hufafanuliwa kama makundi fulani tofauti ya watu, nguvu na vyeo vya makundi haya katika jamii husika – kwani mazungumzo kwa kutumia lugha

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

mbili au zaidi hutokea pale ambapo makundi yanayoingiliana hutumia lugha zinazotofautiana. Kulingana na Giles na wengine (1977) cheo cha kikundi, nguvu za kidemografia, ufadhili wa kitaasisi na hali za kurekebisha huungana pamoja kuunda nguvu zinazohuzishwa na kundi fulani la watu.

Dhana ya usawazishaji wa usemi ina maana ya namna ya urekebishaji wa usemi. Ni kule kurekebisha au kubadilisha usemi ili mzungumzaji awe sawa na wanaomsikiliza – kubadilisha jinsi ya kuongea ili kuwa sawa na wasikilizaji. Kubadilisha usemi kamwe hakudhihirishi kutokuwa na umilisi wa lugha kwa upande wa mzungumzaji bali ni ishara ya ulumbi (Milroy na Muysken, 1995).

Usawazishaji wa usemi ni tofauti na dhana kama vile kubadili msimbo na kuchanganya lugha. Katika kubadili msimbo, watu hubadilisha kutoka lugha moja hadi nyingine tofauti . Katika mawasiliano, uchanganyaji wa lugha ni ile hali ya kutumia lugha mbili kwa pamoja katika matumizi ya wakati mmoja katika mkutadha huo huo mmoja.

Katika utafiti huu dhana hizi tatu zimechukuliwa kuwa tofauti na utafiti utajishungulisha na usawazishaji wa usemi ingawa dhana za kuchanganya lugha na kubadili msimbo zitatajwa hapa na pale katika kujaribu kufafanua au kuweka wazi usawazishaji wa usemi. Kuna mitazamo tofauti kuhusiana na ubadilishaji wa usemi (au lugha). Kwa mfano, mtazamo wa Kisaikolojia (Steinberg, 1982; Michael, 1990), mtazamo wa Isimujamii (Giles na wengine, 1979; Scotton, 1983, 1993) na mtazamo wa Kiisimu (Trudgill, 1986). Utafiti huu unafuata mtazamo wa Isimujamii. Unachunguza urekebishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika wakitumia lugha ya Kiswahili.

Lugha ya Kiswahili ni lugha mawasiliano ambayo huunganisha makundi ya watu tofauti nchini Kenya. Lugha hii hufunzwa kama lugha ya pili nchini katika shule za msingi, upili na vyuo.

Ingawa kuna lahaja bainifu kumi na tano za lugha ya Kiswahili katika upwa wa Afrika Mashariki, kunazo lahaja zinginezo za Kiswahili ambazo hazijabainika kabisa kama zile za pwani (Munyua, 2002). Lahaja hizi zisizobainika hutokea kutokana na wazungumzaji wa Kiswahili kutoka kabila tofauti tofauti wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Kiswahili wanachozungumza huwa na athari tofauti zitokanazo na lugha za kwanza. Hali hii husababisha kuwepo kwa launi za lugha ya Kiswahili ambazo ni tofauti na Kiswahili sanifu. Watoto mjini hujifunza launi hizi na kuzitumia katika mawasiliano ya kila siku. Sifa moja ya launi hizi za lugha ni ugeuzaji wa sarufi katika Kiswahili sanifu. Ugeuzaji au ubadilikaji huu hujitokeza katika viwango vyote: fonolojia, mofolojia, sintaksia, na semantiki (Mukuria na Ipara, 1999 wakinukuliwa katika Munyua, 2002).

Mfano mwafaka wa launi ya lugha ya aina ni aina ya Kiswahili ambayo Waasia wanatumia wanapoingiliana na Waafrika jijini Nairobi. Kiswahili sanifu hakipo baina ya Waasia, bali kunayo launi ya Kiswahili ambayo imeongezewa na baadhi yao, na hutumika kuwasiliana na Waafrika na wakati mwingine Waasia wenzao na pia Wazungu (Neale, 1974).

Matumizi ya lugha moja kati ya Waasia wanaoishi Kenya ni jambo ambalo haliko bali wameweka pamoja lugha za Kenya pamoja na zao na huzitumia hizi zote katika mawasiliano na hizi lugha huchaguliwa kutegemea muktadha na washiriki.

Kulingana na Neale (1974) kundi hili la Waasia, ingawa ndogo likilinganishwa na Waafrika wanaoishi jijini Nairobi hutumia lugha nyingi ambazo si rahisi kubainika. Baadhi ya waasia waliingia nchini Kenya miaka michache iliyopita kutoka Pakistani na Bara Hindi lakini wengi wao ni wana wa vizazi ambao waliingia Kenya miaka ya mwanzo wa karne ya ishirini: wafanyabiashara kutoka Gujarati, wafanyakazi wa reli kutoka Punjabi, na makarani kutoka Goa. Waliohamia Kenya ni wachache sana wakilinganishwa na wale ambao ni wazaliwa wa Kenya (Neale, 1974). Wakati Waasia walipowasili Kenya kulikuwa na Waafrika wachache ambao walikifahamu Kiingereza kwa hivyo iliwabidi watumie Kiswahili ili kuwasiliana na Waafrika watumishi nyumbani na wafanyakazi katika maduka ya Waasia.

Kiswahili wanachotumia Waasia si sanifu bali kimeathiriwa na lugha zao za kwanza. Wale Waafrika ambao wanaingiliana na Waasia wamejifunza launi hii ya Kiswahili inayotumiwa na Waasia na ndiyo wanayotumia wakati wanapozungumza na Waasia. Waasia wamedumisha kitengo fulani cha utamaduni kwa namna fulani ya usimilishwaji au uigaji teule, kwa kukopa yale wanayohitaji kutoka kwa wengine na kuyafanya yao, kama vile wale wanaotumia lugha mbili kwa pamoja katika matumizi ya wakati mmoja katika muktadha huo huo mmoja hukopa maneno kutoka lugha zingine na kuyabadilisha ili yawe sawa na lugha yao. Wamesimilisha Kiswahili na kukibadilisha kwa kuweka athari fulani na papo hapo kuibusha launi ya Kiswahili ambayo ni tofauti na Kiswahili sanifu. Watu wengi nchini Kenya wanapoingiliana na Waasia husawazisha usemi wao kwa hii launi ya Kiswahili ya Waasia.

Waasia na Waafrika jijini Nairobi huwa na mahusiano ya Kiuchumi ya karibu kama vile ya kibiashara.

Nairobi ni mji mkuu wa Kenya na biashara aina tofauti tofauti huendashwa hapa. Aidha watu kutoka bara tofauti zikiwemo Uropa, Asia, Marekani, Afrika na Australia hupatikana hapa. Watu wengi Nairobi wana ujuzi wa lugha zaidi ya moja na mara nyingi katika mazungumzo yao hubadilisha kutoka lugha moja hadi nyingine (Kanana, 2003).

Utafiti huu unalenga kuchunguza matumizi ya lugha baina ya Waasia na Waafrika katika mahusiano ya ana kwa ana katika eneo la katikati mwa jiji la Nairobi. Utafiti utajikita katika mahusiano ya kikazi pale ambapo Waasia wamewaajiri Waafrika madukani mwao na pale ambapo Waafrika watakuwa wateja katika maduka haya.

Lengo la utafiti huu ni kuchunguza jinsi Waasia wamejisawazisha kiusemi kwa Waafrika kwa kutumia Kiswahili ambacho ni lugha ya Kiafrika na kwa upande mwingine namna ambavyo Waafrika wanajinasibisha kwa Waasia kwa kutumia launi ya Kiswahili ya Waasia .

**1.2 Swala la Utafiti**

Utafiti huu unajikita katika somo la Isimujamii na unalenga kuchunguza, kuchanganua na kueleza usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika katika eneo la katikati mwa jiji la Nairobi.

Waasia wamedumisha kitengo maalum cha utamaduni kwa namna fulani ya usimilishwaji,au uigaji teule, kwa kukopa yale wanayohitaji kutoka kwa wengine na kuyafanya yao kama vile wale wanaotumia lugha mbili kwa pamoja katika matumizi ya wakati mmoja katika muktadha huo huo mmoja, hukopa maneno kutoka lugha zingine na kuyabadilisha ili yawe sawa na lugha yao. Wamesimilisha Kiswahili na kukibadilisha

kwa kuweka athari fulani na papo hapo kuibusha aina fulani ya Kiswahili ambayo ni tofauti na Kiswahili sanifu (Neale,1974). Wakenya wengi wanapoingiliana na Waasia husawazisha usemi wao kwa 'Kiswahili cha Waasia'. Waasia na Waafrika huwa na mahusiano ya kiuchumi ya karibu kama vile ya kibiashara. Hali kama hii inafaa kuchunguzwa ili kubainisha matumizi ya lugha kati ya watu hawa, mbinu za maingiliano yao, hasa katika maduka ya Waasia ambapo Waasia wamewaajiri Waafrika.

Kadri ya ujuzi wetu, hakuna utafiti ambao umewahi kufanywa unaochunguza na kueleza viwango vya kiisimu vya usawazishaji wa usemi na vile vile mambo yanayomotisha usawazishaji huu wa usemi kati ya Waasia na Waafrika. Tafiti chache ambazo zimeandikwa kuhusu lugha za Waasia zinahusu mambo ya kiisimu kwa jumla , kama vile matumizi ya lugha kati ya Waasia nchini Kenya (Neale, 1974). Pia kuna mengi kuhusu usawazishaji wa usemi katika mbari na lahaja za lugha za Kiafrika (k. m Mathooko, 2004 na Kebeya,1997) lakini sio kuhusu usawasishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika na zaidi viwango vya semantiki na sintaksia. Aidha nadharia za kijamii, kisaikolojia – jamii na kimuundo zinatumiwa kwa pamoja. Kwa hivyo jambo hili linasababisha haja ya kuchunguza ni kwa namna na kiwango gani wazungumzaji hawa hubadilisha na kurekebisha usemi wao wakati wanapoingiliana.Utafiti huu unachunguza namna na kiasi cha usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika kwa kutumia mihimili ya nadharia ya Usawazishaji Usemi, nadharia ya Upekee na nadharia ya Sarufi Miundo Virai.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu unaongozwa na maswali yafuatayo:

1. Ni kwa njia gani Waasia wanavyosawazisha usemi wao kwa Kiswahili?
2. Ni kwa njia gani Waafrika wanavyosawazisha usemi wao kwa launi ya Kiswahili ya Waasia?
3. Ni mambo gani yanayowamotisha Waafrika na Waasia kurekebisha usemi?

## 1.4 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu ni pamoja na:

1. Kubainisha namna ya usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika
2. Kutambua, kuchunguza na kueleza viwango vya kiisimu hasa vya kisemantiki na kisintaksia vinavyobadilishwa katika utaratibu wa usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika jijini Nairobi.
3. Kufafanua sababu za usawazishaji wa usemi kati ya Waafrika na Waasia.

## 1.5 Nadharia tete

Utafiti huu una nadharia tete zifuatazo:

1. Kuna usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika wakati wa maingiliano.
2. Waasia na Waafrika wanajinasibisha katika viwango tofauti vya kiisimu.
3. Utaratibu wa usawazishaji wa usemi huongozwa na sababu za kiuchumi na kijamii.

## 1.6 Sababu za Kuchagua Mada

Usawazishaji wa usemi ni jambo ambalo limeshughulikiwa kwa kina kuhusiana na lugha za Wazungu lakini machache sana yenye utaratibu yamefanyiwa lugha za Kiafrika kwa jumla na kwa udhahiri Kenya (Kebeya, 1997 na Mathooko, 2004). Usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika ni jambo ambalo halijachuguzwa. Kunazo tafiti ambazo zinashugulikia usawazishaji wa usemi kati ya lahaja za lugha moja (Kebeya, 1997; Russell, 1982; Scotton and Ury, 1977). Tafiti zingine zimeangalia ubadili wa msimbo kati ya makundi ya wazungumzaji wanaotumia lugha tatu tofauti kwa wakati mmoja katika muktadha mmoja (Muthwii, 1994).

Kwa hivyo utafiti huu unahalalishwa na ile hali ya kuwa unalenga wazungumzaji kutoka jamii kutoka maeneo yanayotofautiana, kutoka bara tofauti na ambao ulifanywa katika maeneo ya mjini. Unatofautiana na tafiti zingine ambazo zinajikita katika maeneo ya mashambani (kama vile Mathooko, 2004). Utafiti huu unaweza kuchangia kuelewa kaida zinazotawala matumizi ya lugha katika hali rasmi (hali za kikazi). Kanana (2003) alichunguza matumizi ya lugha sokoni. Wengine kama Kebeya (1997); Parkin (1974); Mũthwii (1994) na Gachinu (1996) walichunguza matumizi ya lugha katika hali zisizo rasmi.

Utafiti huu pia unaweza kusaidia kutoa maelezo zaidi kuhusu matumizi ya nadharia za Usawazishaji Usemi, Upekee na Sarufi Miundo Virai. Pia unafafanua sababu za kijamii na kiuchumi zinazosababisha ubadilishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika. Muhimu zaidi unaweza kuwafaa wakuza mitaala kuibua mbinu na nadharia mwafaka katika ufunzaji wa Kiswahili sanifu.

## 1 .7 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ni wa Isimujamii na umefanywa katika eneo la katikati mwa jiji la Nairobi kuchunguza utaratibu wa usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika wakati wa maingiliano ya ana kwa ana.

Lengo kuu ni kubainisha namna na sababu za usawazishaji wa usemi .Utafiti umelenga kuelezea viwango vya usawazishaji na madhumuni ya huo ujinasibishaji .

Tafiti za awali zimeshughulikia viwango mbalimbali vya usawazishaji wa usemi lakini utafiti huu unashughulikia usawazishaji wa usemi katika viwango vya semantiki na sintaksia wakati wa maingiliano ya ana kwa ana. Mifano ya tafiti hizi za awali ni kama utafiti wa Mathooko (2004) ambaye ameangalia usawazishaji wa kifonolojia na kileksia. Tafiti hizi za awali katika Isimujamii pia hazikujishughulisha na sababu za kiuchumi zinazosababisha usawazishaji wa usemi. Kwa hivyo kunayo haja ya kuchunguza hoja hizi. Utafiti huu ulifanywa katika jiji la Nairobi hasa katikati mwa jiji hilo kwa sababu hapa ndipo wale Waasia ambao wanamiliki maduka makubwa ya bidhaa tofauti tofauti wanapatikana wakiingiliana na Waafrika wafanyakazi na wanunuzi.

## 1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada hii.

Upitiaji wa vitabu katika utafiti huu ulifanywa katika hatua tatu: Yaliyoandikwa kuhusu lugha za Waasia, tafiti nchini Kenya zinazohusiana na utafiti wetu na mwisho machache kuhusu lugha ya Kiswahili yanayoambatana na utafiti wetu.

**1.8.1 Tafiti nchini Kenya zinazohusiana na Utafiti huu.**

Kunazo tafiti nyingi hapa nchini zinazochunguza usawazishaji wa usemi wakati wa maingiliano ya ana kwa ana. Mathooko (2004) ameangalia jinsi Watharaka na Wakamba wanavyojisawazisha kiusemi katika maeneo ya mipakani wilayani Mwingi. Utafiti huu unachunguza makabila kutoka kundi la Wabantu. Uchunguzi wake una data muhimu kuhusu usawazishaji wa usemi, lakini ni tofauti na utafiti huu kwani ulijikita katika maeneo ya mashambani ilhali utafiti wetu unachunguza usawazishaji wa usemi maeneo ya mjini.

Kanana (2003) alichunguza kubadili msimbo katika hali za kibiashara katika soko la Wamaasai jijini Nairobi. Utafiti wa Kanana unatofautiana na wetu kwa kuwa wetu unaangalia usawazishaji wa usemi.

Utafiti wa Muthuri (2000) ulichunguza matumizi ya lugha kati ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kenyatta. Unafafanua jinsi wanavyobadilisha kutoka Kiswahili, Kiingereza na lugha za kwanza katika maingiliano yao. Utafiti wake anatofautiana na wetu kwani wetu unajikita katika hali rasmi na pia unahusu usawazishaji wa usemi.

Kebeya (1997) ni utafiti unaochunguza usawazishaji wa usemi kati ya lahaja mbili za lugha ya Kiluyia, yaani Logooli na Lwitakho. Utafiti wa Kebeya unatofautiana na utafiti huu kwa sababu unaangalia watu kutoka lugha tofauti na pia kutoka bara tofauti.Pia utafiti wake unatofautiana na wetu kwa vile wetu unachunguza matumizi ya lugha katika hali rasmi. Muthwii (1994) alichunguza mfumo wa kifonolojia wa kundi la wazungumzaji la Wakalenjin. Amefafanua jinsi mfumo huu unavyoingiliana na ule wa Kiingereza na Kiswahili. Utafiti wake unafanana na utafiti wetu kwani unachunguza

ubadili wa kiusemi wakati mifumo tofauti ya kiisimu inavyoingiliana. Utafiti wake una data muhimu kuhusu usawazishaji wa usemi.

Russell (1982) alichunguza usawazishaji wa usemi kati ya wazungumzaji wa lahaja mbili za Kiswahili huko Mombasa – yaani Kimvita (Kiswahili cha Mombasa) na Kiswahili sanifu. Russell anaelezea kuwa wanawake ambao wamesoma hujisawazisha kiusemi zaidi kuliko wanaume ambao hawajasoma. Pia anaeleza kuwa wazungumzaji wazee hujitenga kiusemi zaidi kuliko vijana. Utafiti wa Russell unafanana na wetu kwa sababu unachunguza usawazishaji wa usemi na unajikita katika lugha ya Kiswahili. Ni tofauti na wetu kwani hauchunguzi yale mabadiliko ya kiisimu yanayotokea wakati wa usawazishaji wa usemi.

Naye Parkin (1974) alichunguza ubadilishaji wa lugha kati ya watu wanaoishi katika mtaa wa Kaloleni (Nairobi). Alibainisha kuwa wanabadilisha lugha kutoka Kiingereza, Kiswahili na lugha za kwanza. Utafiti wa Parkin unafafanua jinsi na sababu za ubadilishaji lugha wakati wa maingiliano ya ana kwa ana. Utafiti wake unafanana na wetu kwani unachunguza kubadilisha lugha kati ya wazungumzaji wakati wa maingiliano ya ana kwa ana.

Kwa hivyo utafiti wetu utajikita katika kuchunguza usawazishaji wa usemi kati ya makundi tofauti ya wazungumzaji katika hali rasmi huko mjini.

### 1.8.2 Lugha za Waasia.

Asia kama bara ina jumla ya nchi arobaini na nane (48), na makabila ya watu tofauti, wanaotumia lugha tofauti.

Waasia wanaoishi Kenya wanaweza kugawanywa katika makundi matatu ya kikabila kulingana na asili yao: Wagujarati (70%), Wapunjabi (20%) na Wagoa (10%) pamoja na idadi nyingine ndogo kutoka Sandhis, Marathis, Bengalis, n.k. Waasia wanaoishi Kenya hujitambulishi kama Wahindi kutoka Kaskazini (Neale, 1974). Wanatumia lugha nyingi asilia na pia wanatumia lugha za Kenya. Lugha wanazozitumia ni kama vile Kihindi na Kigoa pamoja na lugha mawasiliano tatu – Hindustani, Kiswahili na Kiingereza. Waasia waliohamia Kenya walitumia Kiingereza pamoja na lugha mbili kutoka Goa (Kireno na Kilatin). Lugha zingine walizozitumia hapa Kenya ni kama Kigujarati, Kibengali , Kicutchi, Konkani, Kiarabu n.k.

Kiswahili hutumika kama lugha ya mawasiliano na Waafrika na Kiingereza hutumika wanapowasiliana na Wazungu. Lugha zingine za Kiafrika kama vile Kidholuo na Kikuyu ni lugha mawasiliano kwa Waasia wafanyabiashara katika maeneo ya mashambani.

Tofauti katika idadi ya Waasia wanaoishi Kenya hazijahusishwa kamwe na makundi yao ya kijamii; Wapunjabi kutoka kaskazini mwa bara Hindi wana utamaduni na kaida za matumizi ya lugha, na hivyo ndivyo ilivyo na Wagujarati kutoka eneo la kati na Wagoa kutoka eneo la kusini. Wote huzungumza lugha za kaskazini mwa Bara Hindi ambazo zina asili yake katika lugha ya Kisanskriti, lakini hawawezi kuwasiliana wao kwa wenyewe kwa kutumia lugha hizi na ndio sababu wanatumia lugha mawasiliano katika mawasiliano yao kama vile wanavyofanya wanapowasiliana na Waafrika au Wazungu (Neale, 1974).

Waasia wote hutumia ishara fulani ili kuonyesha tofauti kati yao na ruwaza za tofauti hizi kwa urahisi huhusishwa na nembo za utamaduni kama vile kilemba sawasawa kwa

Wasikh wa Namdharia na kilemba kiliochongoka kwa Wasikh wale wengine; tofauti zingine ni kama vile majina ya kwanza, mavazi, vyakula na mila katika ndoa.

Utafiti huu utajishughulisha na matumizi ya lugha ya Kiswahili (lugha ya Kiafrika) kati ya Waafrika na Waasia wanapoingiliana.

### 1.8.3 Lugha ya Kiswahili

Kulingana na Guthrie(1967:118) Kiswahili ni lugha ya Kibantu na katika ugawanyaji wa lugha ameorodhesha Kiswahili kama G42.

Kiswahili ni lugha ya Kiafrika na hutumika kama lugha mawasiliano na huunganisha makundi tofauti ya watu nchini Kenya. Lahaja 15 za Kiswahili zimebainika katika upwa wa Afrika Mashariki kama vile Kiamu ,Kimvita,na Kiunguja lakini kuna launi za lugha hii ambazo hazijabainika wazi (Munyua, 2002). Kiswahili sanifu hufunzwa shuleni Kenya kama lugha ya pili na ni somo la lazima linalotahiniwa.

## 1.9 Mbinu za Utafiti

Mbinu mbili za utafiti zimetumiwa katika utafiti huu. Mbinu ya kwanza ni kusoma yale yaliyoandikwa na yanahusiana na utafiti huu -kuhusu lugha za Waasia, kuhusu lugha ya Kiswahili na kuhusu tafiti zingine zinazohusiana na utafiti huu maktabani. Maktaba mbalimbali zilitembelewa kama vile maktaba ya Chuo Kikuu cha Kenyatta, Chuo Kikuu cha Nairobi na Taasisi zingine .

Mbinu ya pili ni utafiti wa nyanjani ambapo mtafiti alikusanya data katika eneo la utafiti, yaani sehemu za katikati jijini Nairobi ambapo kundi lengwa la utafiti linapopatikana. Waasia ambao wamewaajiri Waafrika katika maduka ya rejareja na ya jumla

wanapatikana kwa wingi hapa. Utafiti huu ulifanywa katika sehemu ya katikati mwa jiji la Nairobi.

Utafiti wa nyanjani ulikuwa wa hatua mbili: hatua ya kwanza ya utafiti ni utafiti wa awali ambapo sampuli ya utafiti ilibainishwa na pia kupima kijumla viwango vya usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika.

Baadaye hatua ya pili ilikuwa ni ule utafiti kamili unaohusu ukusanyaji wa data:

### 1.9.1 Ukusanyaji wa Data

Data ilikusanywa kwa kutumia njia tatu: kunasa sauti, mahojiano na uchunguzi.

Njia mbili za uchunguzi zilitumiwa – uchunguzi ushiriki ambapo mtafiti alishiriki katika hali inayochunguzwa – yaani alishiriki katika mazungumzo ya waarifu. Njia hii hujenga imani kati yake na wahusika. Na kwa upande wa uchuguzi usio-shiriki, mtafiti alijitenga na mazungumzo yao lakini akawa anafuata na kuandika yanayoendelea.Hii ni kwa sababu watu wakigundua wanachunguzwa huenda wakazidisha au kupunguza maongezi yao na hapo kutoa data ambayo si asilia (Romaine, 1984).

Mahojiano yasiyo rasmi yalifanywa kwani njia hii husaidia wazungumzaji kuwa tulivu na kuongea kwa njia iliyo asilia (Mugenda na wengine, 1999).Mazungumzo ya waarifu huwa ya kawaida na mtafiti hupata data inayoonyesha wazi sifa bainifu za mazungumzo yao.

Unasaji wa sauti ulifanywa katika hatua ya mwisho ya ukusanyaji wa data wakati ambapo mtafiti na waarifu walikuwa wameweka uhusiano dhabiti na pia wakati ambapo waarifu humchukua mtafiti kama mmoja wao na hakuna kule kumshuku mtafiti.

### 1.9.2 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa ilifafanuliwa kwa njia ya kimaelezo (Mugenda na wengine, 1999:117) kwa kuzingatia vigezo kama vile njia na sababu za usawazishaji wa usemi. Mazungumzo yaliyonaswa katika kinasa sauti yaliweza kuandikwa. Mazungumzo katika lugha ingine kando na Kiswahili yalitafsiriwa katika lugha lengwa (Kiswahili). Matokeo ya uchunguzi na mahojiano yalichunguzwa na kupata ile habari inayofaa.

### 1.9.3 Uwasilishaji wa Data

Data iliwasilishwa kwa njia ya kimaelezo na kwa kutumia jedwali na michoro. Njia hizi zimetumiwa kufafanua njia na sababu za usawazishaji wa usemi.

# SURA YA PILI

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii tutajikita katika mambo matatu tofauti: nadharia zilizoongoza utafiti huu zitafafanuliwa ili kueleza jinsi zitakavyotumiwa kuchanganua data, ufafanuzi wa launi ya Kiswahili ya Waasia na lugha ya Kiswahili ili kuonyesha jinsi zinavyotofautiana.

## 2.1 Msingi wa Nadharia

Kuna nadharia mbalimbali ambazo zilichunguzwa kama mwongozo wa kuelezea ubadili msimbo miongoni mwa wazungumzaji. Nadharia hizi ni pamoja na nadharia za Awali za Isimujamii (Gumperz, 1982), nadharia za maingiliano za Isimujamii (kama vile nadharia ya Sheria ya Majadiliano iliyoelezwa katika Scotton, 1983b), nadharia za saikolojiajamii (kama vile katika Giles na St. Clair, 1979; Giles na Robinson, 1990), na nadharia za muundo wa jamii (kama vile katika Giles na wengine, 1977; Giles na Robinson, 1990).

Kwa udhahiri nadharia ambazo zinafafanua mabadiliko ya lugha na ambazo zinaweza kutumiwa katika uchunguzi wa usawazishaji wa usemi ni kama vile nadharia ya Uamilifu (utafiti wa Jacobson na Halliday; Mulhausler, 1981 wakinukiliwa katika Appel na Muysken, 1987), nadharia ya Utofauti (Labov, 1972), nadharia ya Usawazishaji Usemi (Giles na St. Clair, 1979) na Upekee (Scotton, 1983). Hatukutumia nadharia hizi zote ingawa zinahusiana na kazi yetu.

Katika utafiti huu nadharia tatu zilitumiwa: nadharia za Usawazishaji Usemi, Upekee na Sarufi Miundo Virai. Kabla ya kufafanua nadharia hizi tatu kwanza tutatoa maelezo mafupi kuhusiana na nadharia ambazo zina uhusiano na utafiti huu lakini hazikutumiwa. Nadharia ya Utofauti iliasisiwa na Labov (1972). Ni madai ya nadharia hii kuwa lugha zote huwa na tofauti za aina na kwamba lugha huchukuliwa kama mfumo unaobadilika. Kulingana na Labov, lugha huwa na mifumo tofauti ambayo hujitokeza katika wazungumzaji wa lugha hizi. Nadharia hii haikutumiwa katika utafiti wetu kwa sababu lengo letu si kubainisha mifumo ya lugha tofauti bali tumejikita katika kuchunguza usawazishaji wa usemi katika makundi mawili tofauti ya watu wanaozungumza lugha moja lakini launi tofauti.

Nayo nadharia ya Uamilifu inasema kuwa matumizi ya lugha hujumuisha majukumu tofauti ambayo hubainika katika mfumo wa lugha. Nadharia hii imeelezea majukumu sita ambayo yanatekelezwa na lugha miongoni mwa watumiaji wa lugha – jukumu la kufahamisha, jukumu linaloongoza ujumuishi wa watu, jukumu la kujieleza, jukumu la kutoa hisia na kusisitiza, jukumu la kutumbuiza na jukumu la kutoa mafumbo. . Kulingana na nadharia hii majukumu yanayotekelezwa na lugha fulani huathiri uchaguzi na matumizi ya lugha hiyo. Hii ni kwa sababu lugha tofauti hutekeleza kazi tofauti katika maisha ya walumbi. Nadharia hii inahusu zaidi uchaguzi wa lugha unaotegemea jukumu la lugha tofauti na zikiwa nyingi kwa hivyo haikutumiwa katika utafiti wetu kwa sababu tunajishughulisha zaidi na ubadilishaji wa usemi baina ya walumbi wanaotumia launi tofauti za lugha moja.

Kutokana na nadharia za awali za Isimujamii, kaida zinazotawala hali zinazowazingira wazungumzaji zimeweza kuelezewa. Kaida hizi huelezea sifa zinazohusishwa na usemi kama vile sifa za kijamii za washiriki, mada, mazingira ya usemi na madhumuni ya mawasiliano (Hymes, 1972; Trudgill, 1974; Gumperz, 1982). Kaida hizi ni muhimu katika kuchunguza ubadilishaji wa usemi lakini hazikutumiwa katika utafiti huu kwa sababu utafiti haujikiti katika kufafanua hali zinazozingira washiriki katika mazungumzo bali utafiti unalenga kueleza njia na sababu za ubadilishaji wa uneni kati ya Waasia na Waafrika.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tatu: nadharia ya Usawazishaji Usemi (Giles na St. Clair , 1979), nadharia ya Upekee (Scotton, 1983) na nadharia ya Sarufi Miundo Virai.

### 2.1.1 Nadharia ya Usawazishaji Usemi

Nadharia ya Usawazishaji Usemi iliasisiwa na Giles (Giles na St. Clair, 1979). Imetumiwa na wanasaikolojia jamii pamoja na wanaisimu katika kuchunguza tabia na matumizi ya lugha kati ya wazungumzaji wanaotumia lugha tofauti (Giles na St. Clair 1979; Giles na wengine, 1980; Russell, 1982; Trudgill, 1986; Kebeya, 1997). Hii ni nadharia inayoshugulikia ubadili wa msimbo na ambayo ilianzishwa kwa upande mmoja kufidia mwelekeo dhaifu wa wanaisimujamii wa awali na pia kushughulikia ubadili msimbo kutegemea lengo, mielekeo, hisi na uaminifu katika kikundi cha wazungumzaji (Giles na Robinson, 1990).

Usawazishaji Usemi hufafanua ni kwa njia gani wazungumzaji hubadilisha lugha wanapowasiliana. Cha muhimu kuhusu nadharia hii ni hoja kuwa wazungumzaji

hubadilisha jinsi ya usemaji kama njia ya kupata au kutopata kukubalika, kuwasiliana kwa ufasaha na kudumisha nafasi mahsusi katika jamii (Giles na wengine, 1982). Nadharia hii hulenga usemi, hujaribu kueleza ni kwa nini wazungumzaji hubadilisha lugha yao wakizungumza na wengine kwa njia na kiwango wanavyofanya.

Katika kuendeleza nadharia ya Usawazishaji Usemi, inaaminika kwamba ubadilishaji wa usemi hutia nguvu mawasiliano na kupunguza tofauti kati ya washiriki. Usawazishaji Usemi hujitokeza kwa njia mbili: Mwingiano na Ujitengaji. Katika mwingiano, wazungumzaji watachagua ile lugha ambayo inaeleweka au inapendwa na wasikilizaji. Watafanya hivi kama njia ya kuwa sawa kijamii au kutaka kukubalika. Nadharia ya Usawazishaji Usemi huchukulia mwingiliano kama mbinu ya kukadiria gharama ya kijamii wakati ambapo wazungumzaji watapata gharama ambayo mwishowe huleta faida. Kuhusiana na mwingiano inaelezwa kuwa wakati watu wawili wanapokutana, mara nyingi wanakuwa sawa katika lugha - matamshi, kipimo cha usemi, mipumuo, urefu wa tamko na pia kule kuelewana. Kinyume cha hali hii huweza kutokea, pale ambapo watatofautiana katika lugha (ujitengaji). Ujitengaji huchukuliwa kuwa njia mzungumzaji anayotumia ili kuwa mbali na msikilizaji kwa kuzidisha tofauti za lugha kati yao. Kwa mfano, mzungumzaji anaweza kuamua kuwa tofauti na msikilizaji katika lugha au kutomkubali. Wakati wa ujitengaji tofauti za lugha huzidishwa .Wazungumzaji hivyo watajitenga kiusemi iwapo wanataka kuwa tofauti kijamii (Giles na St. Clair, 1979).
Kulingana na nadharia hii, usemi wa mzungumzaji unaweza kuwa sawa au tofauti na ule wa msikilizaji. Mara nyingi mwingiano ni ishara ya umoja kati ya wazungumzaji na ujitengaji ni dhihirisho la utengano kiusemi kati yao (Fasold,1984). Kulingana na Fasold, mwingiano hujitokeza zaidi pale ambapo mzungumzaji atachukua lugha ya mwingine na

kutamka kwa matamshi kama ya mzungumzaji asilia wa lugha hiyo. Mwingiano uliopungua ni pale mzungumzaji anatumia lugha ya mwingine na kuitamka kama yake. Nadharia ya Usawazishaji Usemi ina mihimili minne:-nadharia ya Kufanana – Kuvutiana, nadharia ya Kukadiria Gharama kati ya Wanajamii, nadharia ya Sababu-Husishi na nadharia ya Kujitambulisha Kijamii. Mihimili hii inajitokeza kama vijinadharia ndani ya nadharia kuu. (Giles na St. Clair, 1979)

Mihimili hii husaidia kufafanua dhana za mwingiano na ujitengaji katika usawazishaji wa usemi. Tutaelezea mihimili hii hivi punde:

- Mhimili wa Kufanana-Kuvutiana.

Mhimili huu hulenga kueleza kuwa mfanano wa mitazamo na imani kati ya watu husababbabisha mvuto kati yao. Mwingiano kiusemi ni njia moja ya kuonyesha mvuto kati ya watu. Zaidi mhimili huu unahusu kuongezea ufanano wa kiusemi unaoongezea kule kukaribiana au kuwa sawa katika lugha. Haya huwezekana kupitia kupunguza tofauti kati ya wazungumzaji. Mzungumzaji ataonyesha mwingiano kwa kiasi sawa na ile haja yake ya kutaka kukubaliwa na msikilizaji ( Giles na St. Clair, 1979). Kulingana na mhimili huu mzungumzaji ana uwezo wa kumfanya msikilizaji amkubali kwa kupunguza tofauti kati yake na msikilizaji . Mhimili huu ulisaidia utafiti wetu kufasiri uchaguzi wa lugha fulani ikilinganishwa na lugha ya mzungumzaji na utambulisho wake. Pia ulisaidia kuelezea sababu za kubadilisha mtindo wa usemi.

- Mhimili wa Kukadiria Gharama kati ya Wanajamii.

Mhimili huu husema kuwa kabla ya kushughulikia jambo fulani kwanza mtu hupima gharama na manufaa ya jambo hilo. Mara nyingi watu huonyesha mwingiano ikiwa

faida ni nyingi (mali, kukubalika) kuliko gharama (kupoteza utambulisho katika kikundi, jitihada kilugha (Giles na Robinson, 1990).

Kwa hivyo watu hujishughulisha na mambo yanayowaletea faida na kujiepusha na yale yenye gharama kwa upande wao. Hii ina maana kuwa watu watajisawazisha kiusemi ili kupata faida (kujinufaisha kifedha na kihali) na kujitenga kiusemi ili kuepuka gharama. Kuhusiana na mhimili huu mwingiano huwa wa aina mbili: mwingiano – juu na mwingiano – chini. Mwingiano - juu hujitokeza pale ambapo mzungumzaji wa hadhi ya chini anajifanya sawa kiusemi na msikilizaji wa hadhi ya juu, kwa mfano, mwanafunzi kwa mwalimu. Nao mwingiano – chini ni hali inayotokea hivi kwamba mzungumzaji wa hadhi ya juu anajisawazisha kiusemi kwa msikilizaji wa hadhi ya chini, kwa mfano, mwajiri kwa mwajiriwa . Mhimili huu ulitusaidia kuelezea sababu zinazomotisha usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika (hasa mwingiano juu na chini)

- Mhimili wa Kujitambulisha Kijamii.

Mhimili huu hufafanua ujitengaji kiusemi. Wazungumzaji hubadilisha usemi ili kujitofautisha na wasikilizaji. Hii humotishwa na kule kutaka kujitambulisha na kundi fulani au kuwa tofauti na lingine. Mhimili huu ulitumika kuchuguza iwapo Waasia wanajitenga kiusemi na Waafrika na kwa kiasi na jinsi gani. Vile vile ulitumika kubainisha iwapo kwa Waafrika wanajitenga kiusemi na Waasia kwa jinsi na kiwango gani.

- Mhimili wa Sababu – Husishi.

Mhimili huu unasema kuwa tabia za watu wengine hufasiriwa na kutathimini watu wenyewe kulingana na mitazamo na makusudi yanayochukuliwa kama sababu au

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

chanzo cha tabia hiyo. Mhimili huu haukutumiwa katika utafiti wetu kwani utafiti huu hauhusiki na mitazamo na mielekeo ya watu.

Utafiti huu ulitumia vijinadharia vitatu vya nadharia ya Usawazishaji Usemi, yaani Kufanana – Kuvutiana, Kukadiria Gharama Kati ya Wanajamii na Kujitambulisha Kijamii. Nadharia ya Usawazishaji Usemi husaidia kuelewa sababu za kisaikolojia za usawazishaji wa usemi lakini haitoi sababu za kijamii za usawazishaji wa usemi. Kwa hivyo nadharia ya Upekee ilifidia udhaifu wa nadharia ya Usawazishaji Usemi katika kufikia malengo ya utafiti huu.Nadharia ya pili katika utafiti huu basi ilikuwa nadharia ya Upekee.

### 2.1.2 Nadharia ya Upekee

Nadharia ya Upekee ilijengeka katika msingi wa imani kuwa wazungumzaji wana namna ya upekee kuhusiana na zile lugha wanazozijua na wanaweza kuzitumia katika maingiliano yoyote, lakini huishia kuchagua lugha ya mawasiliano kutegemea msikilizaji na uhusiano kati yao ambao wangetaka uendelee kuwepo. Dhana ya Upekee ni sifa ya lugha iliyo kawaida, ya kijumla na isiyopendelea upande wowote (Crystal, 1985: 322). Huelezea sheria za lugha ambazo ni rahisi kueleweka (Ellis, 1986: 300). Naye Scotton (1993) anasema kuwa upekee humaanisha kuwa uchaguzi wa lugha huchukuliwa kama mifumo inayopigana. Hii inatokana na hoja kuwa upekee ni kipengele cha upinzani. Hata hivyo si rahisi kuwa na uchaguzi wa kipekee au usio wa kipekee bainifu ukitawala mazungumzo peke yake. Kanuni ya upekee inachukuliwa kuwa ni kule kutambua mivuto tofauti inayojitokeza ndani ya mifumo ya lugha (Scotton, 1993).

Hali kadhalika, madai muhimu kuhusiana na nadharia ya Upekee ni kuwa uchaguzi wa lugha unachukuliwa kama utambulishi wa jozi za haki na majukumu zinazobainishwa na washiriki katika maingiliano yanayohusika. 'Sheria ya majadiliano' iliyoasisiwa na Scotton (1983) inaipa nguvu nadharia hii inaposema kwamba uchaguzi wowote wa lugha zaidi kabisa unaweza kuelezewa kuhusiana na kile kinachomotisha mzungumzaji. Nayo 'sheria ya majadiliano' ilijengwa juu ya 'sheria ya ushirikiano' ya Grice. 'Sheria ya ushirikiano' (Grice, 1975) husema kuwa *"chagua muundo wa mchango utakaotoa katika mazungumzo unaoashiria jozi za haki na majukumu ambazo ungetaka zibainike kati yako na msikilizaji"* (Scotton,1993) ( tafsiri yetu) 'Sheria ya ushirikiano' inaweza kufafanuliwa kwa vijisheria vinne ambavyo tutaviita kanuni (Grice, 1975, akinukuliwa katika Yule, 1996). Kanuni za 'sheria ya ushirikiano' katika mawasiliano huwa hazitajwi lakini zinafuatwa. Cook (1989: 29) anatilia nguvu wazo hili anaposema kuwa mawasiliano huendeshwa kulingana na kanuni inayojulikana na ambayo inatumiwa na binadamu wote. Kwa ufupi, kanuni hizi ni pamoja na :

- Kanuni ya Kiasi

Kulingana na kanuni hii mzungumzaji anahitajika asipunguze wala kuzidisha mchango wake wa habari katika mazungumzo yanayoendelea – atoe habari inayohitajika wakati huo peke yake. Yaani, asipunguze sana wala kuongeza sana. Atoe habari kiasi kinachokubalika.

- Kanuni ya Ukweli

Kanuni hii inahusu ukweli katika habari inayotolewa katika mazungumzo, kwamba mzungumuzaji asiseme yale ambayo anaamini si ya ukweli na pia asiseme yale ambayo hana ushahidi wa kutosha kwayo.

- Kanuni ya Mwelekeo

Hii kanuni inasema kuwa mzungumzaji anafaa kufanya mchango wake wa mazungumzo kuwa na mwelekeo kwa kulenga mada ya mazungumzo.

- Kanuni ya Udhahiri

Kanuni hii inalenga kuwa mzungumzaji aepuke utata katika mazungumzo, aongee kwa ufupi na kwa mpangilio.

Kanuni hizi nne zinatumiwa kufafanua usawazishaji wa usemi katika kiwango cha semantiki na sintaksia baina ya Waasia na Waafrika kwa kuelezea iwapo washiriki katika mazungumzo wanatoa habari inayohitajika, ya ukweli, yenye mwelekeo na ya udhahiri. Haya ni kuambatana na madai ya Scotton (1993) kuwa uchaguzi wowote wa Kiisimu zaidi unachukuliwa kuwa majadiliano ya umuhimu wa sifa zinazozingira mazungumzo. Haya yana maana kuwa nadharia ya Upekee huelezea uchaguzi wa lugha kama majadiliano ya jozi za haki na majukumu, na kwa vile jozi hizi hutokana na hali au sifa zinazozingira mazungumzo, taratibu hizi huweka uhusiano kati ya uchaguzi wa lugha na umuhimu wa majadiliano ya sifa zinazozunguka mazungumzo fulani.

Nadharia hii hujaribu kuelezea sababu za kisaikolojia na za kijamii za kubadilisha lugha.Imejengeka katika misingi ya 'sheria ya majadiliano' iliyo asisiwa na Scotton (1983) kwamba uchaguzi wa lugha hutegemea kinachomotisha mzungumzaji.

Nayo sheria ya majadiliano ilijengwa juu ya 'sheria ya Grice ya ushirikiano' (Scotton,1993:113). Kunazo kanuni tatu kuu za nadharia hii ambazo zinatumiwa kuchanganua data katika kazi hii. Kanuni hizi ni :

- Kanuni ya Kipekee ya Uchaguzi

- Kanuni isiyo ya Kipekee ya Uchaguzi
- Kanuni Bahatishi ya Uchaguzi.

Aidha kuna vijikanuni viwili chini ya Kanuni isiyo ya Kipekee ambavyo humwelekeza mzungumzaji kwa Kanuni ya Kipekee. Vijikanuni hivi ni Kanuni ya Weledi na Kanuni ya Kuondosha. Kanuni hizi zote za nadharia ya upekee zinafafanuliwa katika sehemu inayofuata.

- Kanuni ya Kipekee ya Uchaguzi.

Kanuni hii husema: " *Fanya uchaguzi wa kipekee na ambao sio utambulishi wa jozi ya haki na majukumu isiyo ya kipekee katika maingiliano iwapo ungetaka kuthibiti jozi mpya ya haki na majukumu isiyo ya kipekee kuhusiana na mazungumzo yanayoendelea"* (Scotton, 1993) (tafsiri yetu). Kwa jumla, uchaguzi huu wa lugha unahusu majadiliano ya lugha yatakayoleta kubadilika kwa ukuruba wa kijamii unaotarajiwa baina ya washiriki: kuupunguza au kuuongezea. Katika kanuni hii mzungumzaji anatarajiwa aepuke kujiunga na jozi ya haki na majukumu inayotarajiwa. Wazungumzaji hupima gharama na manufaa yanayotarajiwa iwapo lugha fulani itatumiwa na hivyo wanafanya uchaguzi usiotarajiwa. Kwa kutimiza kanuni hii mzungumzaji anasema *'weka kando makisio ya awali ulio nayo kuhusu kaida za kijamii na uuangalie uhusiano wetu vingine'* (Scotton,1993 :131) (Tafsiri yetu).

Inachukuliwa kuwa ni bora kufanya uchaguzi usio wa kipekee lakini hii haiwi hivyo kwani wazungumzaji huchagua lugha kutegemea manufaa au gharama inayotarajiwa.Uchaguzi huu hufanywa pasipo kuamua (bila hiari) na hivyo wanafanya uchaguzi usiotarajiwa (wa Kipekee).Hivi ni kusema uchaguzi wa lugha usiotarajiwa hutoa habari kwa udhahiri, yaani habari inayomawanda yasiyo mapana. Kanuni hii

hufafanuliwa kwa kuzingatia uchaguzi usio wa kipekee kwani zote mbili hutokea katika jozi. Kanuni hii inasaidia utafiti huu kuchunguza viwango vya usawazishaji wa usemi kwa upande wa Waasia na Waafrika. Pia inasaidia kueleza sababu zinazowafanya wazungumzaji kubadili usemi jinsi wanavyofanya.

- Kanuni isiyo ya Kipekee ya Uchaguzi .

Kanuni hii hueleza kuwa wazungumzaji huchagua lugha ya mawasiliano ambayo zaidi inatarajiwa kwa kuzingatia kaida za kijamii kuhusu hali za mazungumzo, wasikilizaji, mada na mahali pa mazungumzo. Kanuni hii huchukuliwa kuwa bora kwani inazingatia yanayotarajiwa na washiriki na hakuna mambo yasiyo ya kawaida. Inafidiwa na Kanuni ya Weledi au Ujuzi (wa lugha) inayosema kuwa *'iwapo wazungumzaji hawana uwezo wa kuchagua kanuni isiyo ya kipekee, wachague lugha yoyote ili kuendeleza mazungumzo pamoja na kuhusisha washiriki wote katika mazungumzo'*(Scotton 1993:148) (tafsiri yetu). Kanuni isiyo ya Kipekee humwongoza mzungumzaji kwa namna ifuatayo: "*Fanya uchaguzi wako uwe utambulishi usio wa kipekee wa jozi ya haki na majukumu yasiyo ya kipekee katika mazungumzo iwapo ungetaka kuthibiti jozi hiyo*" (Scotton,1993) (tafsiri yetu). Uchaguzi wa aina hii huwa ni rahisi kufanya na kawaida unatoa habari isiyo dhahiri. Kanuni hii inatusaidia kuchunguza viwango vya usawazishaji wa usemi pamoja na sababu zinazowafanya wazungumzaji wabadili usemi jinsi wanavyofanya.

- Kanuni Bahatishi ya Uchaguzi.

Wazungumzaji watatumia kanuni hii iwapo hawana uhakika na lengo la mazungumzo yao, au hawana uhakika wa lugha itakayowasaidia kufikia malengo yao ya kijamii. Hii

hutokea wakati kaida zinazotawala maingiliano fulani hazijabainishwa na washiriki. Kanuni bahatishi ya uchaguzi inasaidia kubainisha zaidi viwango na sababu za usawazishaji wa usemi.

Kwa jumla nadharia ya Upekee ilifidia nadharia ya Usawazishaji Usemi kwa kusaidia kufafanua sababu za kijamii za usawazishaji wa usemi zinazoongoza uchaguzi wa lugha moja tofauti na nyingine na pia viwango vya usawazishaji wa usemi sana sana kiwango cha sintaksia.

### 2.1.3 Nadharia ya Sarufi Miundo Virai

Katika kuelezea nadharia ya Sarufi Miundo Virai, kwanza tutaijengea msingi kwa kuelezea sarufi na sarufi miundo kwa jumla na pia nadharia za uchambuzi wa sarufi zilizotangulia nadharia ya Sarufi Miundo Virai.

#### 2.1.3.1 Sarufi

Sarufi ni taaluma ya uchambuzi wa lugha inayojumuisha viwango vyote vya uchambuzi, yaani, kiwango cha umbo-sauti (fonolojia); kiwango cha umbo – neno (mofolojia); kiwango cha miundo- maneno (sintakisia); na kiwango cha umbo-maana (semantiki) (Massamba na wengine, 1999).

#### 2.1.3.2 Sarufi Miundo

Sarufi miundo nayo ni utanzu wa sarufi unaojishughulisha na uchanganuzi wa mpangilio wa maneno katika sentensi na uhusiano wa virai vyake.

Sarufi Miundo ni mkabala unaoendelezwa na wanaisimu waitwao wanasarufi miundo. Mkabala huu ulipata mashiko miaka ya 1950 kutokana na mawazo ya wanaisimu kama

vile Bloomfield, Harris, Halliday, Trubetzkoy, Martinet, Jackbson, Saussure na Chomsky, tukitaja wachache tu. Wanaisimu hawa walieleza kuwa, lugha ina muundo na imejengwa kwa mofimu; walichambua muundo wa tungo kwa kuchunguza jinsi vipashio vinavyojenga tungo hizo.

Kwa mujibu wa Nkwera (1989:29), Sarufi Miundo huangalia maneno ya tungo kwa mujibu wa nafasi zake katika tungo, yanasimamia nini katika tungo na yanafanya kazi gani maalumu katika tungo.

Kulingana na maoni ya Mdee (1986:24), Sarufi Miundo hujikita katika mpangilio wa ruwaza zinazojirudia na ambazo zina nafasi zilizojazwa na vipengele vya kisarufi.

Kwa jumla Wanasarufi Miundo hujihusisha na uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi. Ili kufanya hivi, wanaangalia viambajengo vya vipashio na vya aina za maneno. Wanaangalia nafasi ya vipashio na jinsi vipashio hivyo vinavyojengana katika sentensi. Vipashio hivi ni mofimu, neno, kirai, kishazi na sentensi. Kiini cha uchambuzi wao ni neno. Tena wanaangalia uhusiano wa aina za maneno uliopo katika sentensi, kwa mfano, jinsi kielezi kinahusiana na kitenzi na jina na kivumishi. Wanasarufi Miundo huangalia sheria ambazo hazina budi kufuatwa katika kuyapanga maneno ya lugha katika mfuatano utakaoleta maana inayokubalika. Waliongozwa na muundo wa sentensi. Miundo mbalimbali huzua uchambuzi mbalimbali wa tungo.

### 2.1.3.3 Mikabala ya Uchambuzi wa Sarufi.

Mikabala ya uchambuzi wa sarufi imekuwa ikibadilikabadilika kadri uchunguzi wa lugha mbalimbali ulimwenguni ulivyokuwa ukiendelea kufanywa na wataalamu mbalimbali (Massamba na wengine, 2001). Tutataja tu bila kufafanua mikabala hii ili kuwekea msingi nadharia ya Sarufi Miundo Virai. Mkabala uliotangulia ni ule wa Kimapokeo. Wanamapokeo walijishughulisha na sentensi sahihi bali si Sarufi Miundo kwa mapana na marefu. Katika sarufi za Kimapokeo sentensi ziliainishwa kama kiima- prediketa-yambwa. Hatutautumia mkabala huu kwa sababu tunahusika na muundo wa lugha katika utafiti huu.

Mkabala wa Sarufi Msonge nao ni mkabala ambao uliwahi kupata mashiko. Katika mkabala huu, lugha huchukuliwa kama mfumo mkuu wenye mifumo mingine ndani mwake. Mifumo hiyo midogo hupangika katika utaratibu wa kimsonge. Kazi yake kubwa ni kujaribu kuonyesha mtandao wa mifumo mbalimbali na uhusiano uliomo katika lugha na jinsi mifumo inavyopangika. Kimsingi Sarufi Msonge haitofautiani sana na sarufi nyingine za Kimapokeo. Tofauti hapa ni kwamba mkabala huu hautumii dhana ya kitendwa. Badala yake hutumia shamirisho. Hatutatumia nadharia ya Sarufi Msonge kwa sababu hiyo.

### 2.1.3.4 Nadharia ya Sarufi Miundo Virai

Nadharia ya Sarufi Miundo Virai ilianza kutumika miaka sitini baada ya nadharia za sarufi zilizotangulia (Kama vile za Kimapokeo na Sarufi Msonge).

Nadharia hii ina msingi wake katika Sarufi Miundo. Baadhi ya wanaisimu wanaohusishwa na nadharia hii ni Trubetzkoy, Bloomfield, Saussure, Chomsky na

Harris. Kwa mujibu wa Massamba na wenziwe (2001:58), Sarufi Miundo Virai ni nadharia inayotumia utaratibu wa uchambuzi wa viambajengo. Huchambua sentensi au tungo kwa kuzingatia virai vyake na kuviainisha.

Sarufi Miundo Virai kulingana na Kihore (2003:106) ni mkabala na uchambuzi wa kiisimu unaojihusisha na kanuni zinazozalisha vijenzi mbalimbali vya sentensi pamoja na uchambuzi wa viambajengo vyake.

Kulingana na nadharia hii kuna dhana mbili kuu na ambazo ndizo zinachukuliwa kama mihimili yake:

- Dhana ya upanuzi

Huu ni utaratibu wa uchambuzi wa vijenzi katika tungo kuanzia vile vidogo hadi kufikia kiwango cha sentensi:

Mofimu ⟶ neno ⟶ kirai ⟶ kishazi ⟶ sentensi.

- Dhana ya kanuni za uchambuzi wa viambajengo:

S ⟶ KN + KT

KN ⟶ N + V

KT ⟶ T + KN

T ⟶ N + WKT + T

KV ⟶ V

KN ⟶ N + KE

KE ⟶ E


Lengo kuu la Sarufi Miundo Virai ni kufafanua makundi ya sarufi kwa kuonyesha uhusiano kati yake katika sentensi. Kwa hivyo Sarufi Miundo Virai hujihusisha na uchambuzi wa tungo na kwa kufanya hivi wanaainisha vijisehemu (virai).

**Mfano 2.1.3.4.1**

Kwa mfano, sentensi kama vile

*Msichana mrembo alicheza densi vizuri*

inaweza kuchambuliwa katika mchoro matawi. Sentensi hii itawakilishwa kama ifuatavyo:




Dhana ya virai tutaieleza hivi punde na kuonyesha aina mbalimbali za virai.


### 2.1.3.4.2 Muundo wa Virai

Kirai ni kipashio chenye maneno zaidi ya moja na ambacho hakina muundo wa kiimakiarifu. Virai vyote isipokuwa Kirai Kitenzi havijitoshelezi kimaana. Kirai Kitenzi hujitosheleza kimaana. Kirai hujulikana kama kikundi au kifungu.

Tunaweza kutambulisha virai katika sentensi.

**Mfano 2.1.3.4.3**

Mama huyu mkali aliwapiga watoto wake kwa hasira:




Muundo wa virai hutegemea aina ya maneno. Kuna aina kadha za virai. Tutaelezea aina tano kiufupi kutegemea aina za maneno. Hizi aina tano zinaelezwa kwa sababu ndizo zitakazotumika katika kazi hii.

KENYATTA UNIVERSITY

- Kirai nomino

Ni aina ya kirai ambacho muundo wake umekitwa kwenye nomino. Kirai nomino huchukua miundo mingi tofauti. Mifano ya miundo hii ni pamoja na :

KN ⟶ N

*Mwalimu* anafundisha hesabu.

KN ⟶ N +N

*Baba na mama* wanakula chakula.

KN ⟶ N+V

*Mbuzi mnono* atachinjwa leo.

- Virai vitenzi

Ni vile ambavyo vimejikita katika kitenzi. Vitenzi virai huchukua miundo kadhaa.

Mifano ya miundo ya virai vitenzi ni kama vile:

KT ⟶ T

*Alikimbia* akielekea mtoni.

KT ⟶ T +N

*Wamemsamehe mwizi.*

KT ⟶ $T+N_1 + N_2$

*Nitamwimbia mgeni wimbo.*

- Virai vivumishi

Ni vile ambavyo muundo wake umekitwa katika kivumishi. Vivumishi virai huchukua miundo ifuatayo:

KV ⟶ V

Kitabu *kizuri* kimenunuliwa

KV ⟶ V +E

Uimbaji *mzuri kabisa* unahitajika

KV ⟶ V+ KN

Mzee *mwenye duka kubwa ameuwawa.*

- Virai viunganishi

Hiki ni kirai ambacho muundo wake umekitwa katika mahusiano baina ya neno kuu ambalo ni kiunganishi na fungu la maneno linaloandamana nacho. Virai viunganishi huwa na muundo mmoja, ule wa kiunganishi kufuatwa na kirai nomino.

Kwa mfano,

Wanafunzi watasafiri *kwa gari.*

Mzee ameenda *kwa mtoto wake.*

- Virai vielezi

Kulingana na Massamba na wenzake (2001:116) miundo ya virai vielezi haielekei kukitwa kwenye mahusiano ya lazima baina ya neno kuu (kielezi) na neno au fungu la maneno yanayoandamana nalo. Tazama mifano ya sentensi zifuatazo:

1. Nilimwona Roda *kwa mara ya kwanza* mwezi huu.
2. Huyu mtoto hulia *sana sana* akiwa mgonjwa.

Nadharia ya Sarufi Miundo Virai inatumika katika utafiti huu kuchambua miundo ya lugha ya Kiswahili na launi ya Kiswahili ya Waasia kisintaksia.

## 2.2 LAUNI YA KISWAHILI YA WAASIA

### 2.2.1 Utangulizi

Katika mtazamo wa kiisimu, vigezo vinavyotambulika katika ubainishaji wa lugha katika makundi mbalimbali ya lugha za ulimwengu ni fonolojia , mofolojia , msamiati wa msingi , na sintaksia (Massamba na wenziwe, 1999). Jambo linalojitokeza katika utafiti huu ni kwamba launi ya Kiswahili ya Waasia inatofautiana kwa kiasi fulani na Kiswahili sanifu katika viwango hivi. Katika sehemu hii tutafafanua kwa ufupi launi ya Kiswahili ya Waasia kwa kuangazia muundo wa launi hii katika viwango vya fonolojia ,mofolojia, na sintaksia . Kwa kufanya hivi tutaweza kutofautisha Kiswahili cha Waasia na Kiswahili sanifu.

Ili kuwasiliana na Waafrika,Waasia hutumia launi ya Kiswahili ambayo ni tofauti na Kiswahili sanifu. Tofauti hii imesababishwa na ule uigaji teule wa Waasia katika matumizi ya Kiswahili, kwani Waasia huchukua kile tu wanachohitaji kutoka lugha ya Kiswahili na kukifanya kiafikiane na lugha zao.


Kulingana na Neale (1974), launi ya Kiswahili ya Waasia ina konsonanti ishirini na moja (21) - /p/, /b/, / t/, /d/, /k/, /g/, /č/, /ɟ/, /f/, /v/, /h/, /s/, /z/, / ʃ /, /m/, / ɲ /, / ŋ /, /l/, /r/, /w/, na vokali tano (5) - / i/, /ɛ/, /a/, /ɔ/, /u /.

Vipasuo ghuna hujitokeza kwa mlipuko na sio bila mlipuko kama ilivyo /b/, /d/, /g/ katika baadhi ya lugha za Kiswahili za pwani. /č/, /ɟ/ hujitokeza kama vizuiwakwamizwa.

Vikwamizwa vitatu vya Kiswahili sanifu /θ /, / ð /, /ɣ / havipo katika launi hii. Jedwali inayofuata linafafanua konsonanti katika launi ya Kiswahili ya Waasia kwa kuzingatia mahali pa kutamkia na jinsi ya kutamka.

| Mahali / Namna | Mdomo | Meno na mdomoni | Meno na ufizi | Ufizi | Kaakaa gumu | Kaakaa laini | Koromeo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vizuiwa | p,b | | | t,d | | k,g | |
| Vikwamizwa | | f,v | ʃ | s,z | | | h |
| Nasali | m | | | ŋ | ɲ | | |
| Vizuiwa vikwamizwa | | | | | č,ɟ | | |
| Kitambaza | | | | l | | | |
| Kimadende | | | | r | | | |
| Viyeyusho | w | | | | | j | |

Wakati wa kutamka vokali, hali ya midomo na ulimi huzingatiwa. Jedwali inayofuata inaainisha vokali katika launi ya Kiswahili ya Waasia.




**2.2.2 Fonolojia katika launi ya Kiswahili ya Waasia.**

Katika kulinganisha lugha katika kiwango cha fonolojia, kuna mengi ya kuzingatia, lakini muhimu ni mpangilio wa vitamkwa kuunda silabi na kanuni mbalimbali za kujenga maneno. Kulingana na utafiti uliofanywa na Neale (1974), Waasia huweza kuingiza mabadiliko mengi ya kifonolojia katika Kiswahili. Baadhi ya mabadiliko haya yanaelezewa katika mifano ifuatayo:

Katika launi ya Kiswahili ya Waasia , /θ/ hubadilika na kuwa /s/.

θ ⟶ s

θɛna ʃ ara ⟶ sɛna ʃ ara

/ŋ/ haitokei mwanzoni mwa neno katika launi ya Kiswahili ya Waasia .Badala yake, /g/ huanza maneno. Tazama mfano ufuatao:

ŋ ⟶ g

ŋ ⊃mbɛ ⟶ g⊃mbɛ

/z/, /h/, /j / hazipatikani katika baadhi ya launi za Kiswahili za Waasia na zinapopatikana huwa hazina msimamo dhabiti wa mahali zinamotokea katika neno bali hujitokeza bila mpangilio maalumu (katika mtawanyiko). /W/ huwa haijitokezi kikamilifu katika neno ikifuata konsonanti.

Hivi ni kusema Waasia watadondosha /w/ iwapo imetokea katika maneno ikifuata konsonanti, yaani, w⟶ ∅ (/w/ hujitokeza kapa). Tazama jedwali ifuatayo:

| **Kiswahili sanifu** | **launi ya Kiswahili ya Waasia** |
|---|---|
| twaɛnda | taɛnda |
| mwaka | maka |
| bwana | bana |
| mwɛzi | mɛzi |

Launi ya Kiswahili ya Waasia haina /h/ au /j/ mwanzoni mwa neno. /h/ na /j/ hupotea ikitangulia vokali.

**/h/na/j/** ⟶ **/∅ /.**

Tazama jedwali ifuatayo:

| **Kiswahili sanifu** | **launi ya Kiswahili ya Waasia** |
|---|---|
| hapana | apana |
| huk⊃ | uk⊃ |
| jɛtu | ɛtu |
| j⊃tɛ | ⊃tɛ |

Vile vile Waasia hudondosha irabu iwapo zimetangulia konsonanti, yaani vokali hujitokeza kapa ikitangulia konsananti.

$$V \longrightarrow \varnothing \;\text{—}/K$$

Tazama jedwali ifuatayo:

| **Kiswahili sanifu** | **launi ya Kiswahili ya Waasia** |
|---|---|
| asubuhi | ∅ subui |
| iʃirini | ∅ ʃirini |
| ilikuwa | ∅ likuwa |

Kwa jumla vokali na nasali huwa hazijitokezi kikamilifu zikitangulia konsonanti. Mfano hapa chini unaonyesha udondoshaji wa nasali ikitangulia kosonanti. Baadhi ya Waasia huweka irabu pahali palipoondolewa nasali.

| **Kiswahili sanifu** | **launi ya Kiswahili ya Waasia** |
|---|---|
| ŋ⊃mbɛ | g⊃mbɛ / ig⊃mbɛ |

Mabadiliko mengine ya kofonolojia katika launi ya Kiswahili ya Waasia ni pamoja na:

| Sauti awali | Mabadiliko | Mfano | Kiswahili sanifu |
|---|---|---|---|
| w | v | vɛvɛ | wɛwɛ |
| l | r | sarɛwa | zaliwa |
| n | l | tɛngɛlɛsa | tɛngɛnɛza |
| ʃ | s | sida | ʃinda |
| v | β | β⊃i | v ⊃i |
| t | č | kiču | kitu |
| p | b au v | baka/avana | mpaka/hapana |
| ɟ | č | mači | maji |

### 2.2.3 Mofolojia katika launi ya Kiswahili ya Waasia.

Maneno ya Kiswahili yasiyotokana na mkopo yanafuata utaratibu wa viambishi na mzizi.Viambishi vinaweza kuwa mwishoni mwa mzizi (tamk-a, tamk-i-a) au vinaweza kutangulia mzizi (m-toto, wa-toto) (Massamba na wenzake,1999). Hali kadhalika, katika uundaji wa maneno katika Kiswahili kanuni fulani hufuatwa. Kwa mfano maneno yanaweza kuundwa kwa kufuata baadhi ya kanuni zifuatazo:

| **Mfuatano wa fonimu (Kanuni)** | **Mfano wa maneno** |
|---|---|
| KVKV | mama |
| KKV | mba |
| KKkV | mbwa |
| KkV | mwa |

Nayo launi ya Kiswahili ya Waasia imeweza kukwepa utaratibu wa viambishi na mzizi na pia baadhi ya kanuni za uundaji wa maneno. Jambo linalojitokeza ni kuwa hakuna utaratibu maalumu wa uundaji wa maneno, kila Mwasia huweka mabadiliko kutegemea lugha yake ya kwanza. Mifano ya maelezo yafuatayo inathibitisha madai haya:

**Mfano 2.2.3.1**

Baadhi ya Waasia hudondosha viambishi awali vya maneno na kuanza neno kwa mzizi.

| Kiswahili sanifu | launi ya Kiswahili ya Waasia |
|---|---|
| mtoto | toto |
| nitaenda | taenda |
| ilikuwa | likuwa |

**Mfano 2.2.3.2**

Vitenzi hutokea pamoja na viambishi awali vitatu: kiambishi awali kisicho na kikomo *ku-*, na viambishi viwili vya wakati *na-* na *ta-*; na ambavyo haviwekwi katika sentensi kanushi. Hii inadihirika katika sentensi zifuatazo:

| Kiswahili sanifu | launi ya Kiswahili ya Waasia |
|---|---|
| sisi hatukuenda | sisi apana kwenda |
| mimi sijui | mimi apana jua |
| kuona / aliona | naona |
| ataona | taona |

**Mfano 2.2.3.3**

Viambishi kanushi *si* – na *hu* – hujitokeza katika maneno machache na ambayo yana umbo thabiti kama vile '*sijui*' na ' *hujui*' na *li* – (kiambishi cha wakati uliopita) hudhihirika mara moja, kwa mfano, katika '*ilikuwa*'.

Neno '*ilikuwa*' pia hutokea pamoja na vitenzi katika baadhi ya launi za Waasia ikiwa na utata kati ya viambishi vya wakati uliopo (*na-)* na wakati uliopita (*li-)* yaani ( *ilikuwa* + *na* - ). Tazama jedwali ifuatayo.

| Kiswahili sanifu | launi ya Kiswahili ya Waasia |
|---|---|
| hawa walikuwa wanajua | ilikuwa najua. |

Viambishi vile vingine awali na tamati havimo na uamilifu wavyo hauwezi kufafanuliwa; kama hupo labda hufafanuliwa kupitia maumbo ya maneno mengine – viwakilishi nomino vitenda na vitendewa, ukanushaji (hapana) na vielezi misemo vya wakati (*kama*) na mahali (*huko*).

| Kiswahili sanifu | launi ya Kiswahili ya Waasia |
|---|---|
| tuliwaona | sisi naona |
| hatukulala | sisi apana lala |
| nilipomwona Patel | kama namwona Patel |
| ninaenda huko | mimi nakwenda uko |

Nomino huwa na viambishi awali vinne: *ki-* , *m-* , *wa-* , *∅*. na vivumishi huwa na viambishi awali vitatu: *ki-* , *m* -, *∅*

Viunganishi huwepo katika launi hii lakini mara nyingi hujitokeza katika sentensi mahali visivyotarajiwa, Kwa mfano mwanzoni mwa sentensi.

Mara nyingi nomino hutokea na kiambishi cha mahali *-ni,* na viambishi vingine vya mahali hupewa maumbo mawili ; *-pa* na *-ko.* Tazama mifano ifuatayo.

**Mfano 2.2.3.4**

Nyumba*ni*

Ha*pa*

Hu*ko*

*-ni* wakati mwingine haihitajiki katika sentensi lakini huwekwa na pia inaweza kuwa ni ya kiuvumbuzi . Tazama mifano ifuatayo :

**Mfano 2.2.3.5**

| Kiswahili sanifu | launi ya Kiswahili ya Waasia |
|---|---|
| ndani ya nyumba | ndani ya nyumba*ni* (1) |
| tulienda kulala | nakwenda lale*ni* (2) |

*-ni* katika sentensi (1) haihitajiki nayo *-ni* katika sentensi (2) ni ya kiuvumbuzi.

**2.2.4 Sintaksia katika launi ya Kiswahili ya Waasia**

Katika sehemu hii tutachanganua sentensi katika launi ya Kiswahili ya Waasia. Launi hii ina ruwaza ya virai katika sentensi, yaani S ⟶ KN + KT (+KN). Tazama sentensi hii:

**Mfano 2.2.4.1**

Kijana natembea na mimi iko ita veve (*kijana unaenda na ninakuita*).

KN KT KN

Pia kuna ugeuzajimaumbo kinyume hivi kwamba muundo sentensi utakuwa :

S ——→ KN + hapana +KT (+KN).

**Mfano 2.2.4.2**

Kijana hapana tembea kama mimi naita veve(*kijana usiende kama nina kuita).*

KN KT KN

Vielezi nyongeza pia hutokea , kwa mfano '*kama*' mwanzoni mwa neno, na '*huko*' mwishoni mwa neno.

**Mfano 2.2.4.3**

1. Kama nataka nguo takuuzia
2. Kama naona *customer* ongea
3. Mimi kwisha tembea huko
4. Magari ote kwisha aribika huko.

Mifanyiko mingine kama vile kauli tendwa , urejeshi na upatanishi haipo (Neale, 1974).

**Mfano 2.2.4.4**

- **Kauli tendwa**

| Launi ya Kiswahili ya Waasia | Kiswahili sanifu |
|---|---|
| 1. Gari naaribu mtu ile | Gari liliaribiwa na mtu yule. |
| 2. Mimi naacha yeye kazi shauri yeye apana fanya kazi musuri | Mimi nilimwachisha kazi kwa sababu hakuwa akifanya kazi vizuri. |

**Mfano 2.2.4.5**

- **Urejeshi**

Katika launi hii urejeshi haudhihiriki wazi bali unajitokeza kupitia matumizi ya maneno *iko* na *wewe*.

| Launi ya Kiswahili ya Waasia | Kiswahili sanifu |
|---|---|
| 1. Mtu mimi iko ambia veve | Mtu ambaye nilikuambia. |
| 2. Nyumba veve iko ona ni yangu | Nyumba uionao ni yangu. |

**Mfano 2.2.4.6**

- **Upatanishi**

Katika launi ya Kiswahili ya Waasia mara nyingi upatanishi wa kisarufi (ngeli) hauzingatiwi. Tazama mifano ifuatayo:

| **Launi ya Kiswahili ya Waasia** | **Kiswahili sanifu** |
|---|---|
| mtoto ile | mtoto yule |
| nguo msuri | nguo nzuri |
| chuma yake | chuma chake |
| mipango nyingi | mipango mingi |
| mambo nyingi | mambo mengi |
| mahali hii | mahali hapa/ humu/ huku |
| peremende mingi | peremende nyingi |
| gari mingi | magari mengi |

Baadhi ya watumiaji wa launi ya Kiswahili ya Waasia huanza sentensi kwa viunganishi. Tazama mifano ifuatayo.

**Mfano 2.2.4.7**

| **Launi ya Kiswahili ya Waasia** | **Kiswahili sanifu** |
|---|---|
| na sisi sote iko saidia yeye. | sisi sote tulimsaidia |
| na nguo ote iko namna io. | nguo zote zinafanana |

Vivumishi havibadiliki – kama vile *'yetu', 'yote'* n.k na *'hii', 'ile'* hufuata mpangilio wa maneno katika Kiswahili lakini '*ile*' huweza kutokea kabla ya nomino. Tazama mfano ufuatao

| **Launi ya Kiswahili ya Waasia** | **Kiswahili sanifu** |
|---|---|
| lakini ile gari likua napita upesi sana subui. | lakini gari ile ilipita upesi sana wakati wa Asubuhi. |

Upatanishi (wa kisarufi) na tofauti za kinyume za kisemantiki hazipo katika launi ya Kiswahili ya Waasia. {wa-} huashiria wingi na vile viambishi awali vingine vinaweza kuashiria umoja au wingi. Sentensi zifuatazo zinafafanua madai haya.

**Mfano 2.2.4.8**

| **Launi ya Kiswahili ya Waasia** | **Kiswahili sanifu** |
|---|---|
| kichwa mzuri | fikira nzuri |
| kichu ote | kila kitu |
| gombe bili | ng'ombe wawili |
| mutoto ote | watoto wote |

Nyakati kwa jumla hazitiliwi maanani katika matumizi ya launi ya Kiswahili ya Waasia. Mifano ifuatayo inaelezea jambo hili.

**Mfano 2.2.4.9**

| **Launi ya Kiswahili ya Waasia** | **Kiswahili sanifu** |
|---|---|
| 1. Wewe apana uza | Wewe hukuuza |
| 2. Kama namwona *customer* | Nilipomwona *customer* |
| 3. Kama iko serewa | Ikiwa nimechelewa |

Launi hii ya Kiswahili ya Waasia imepungukiwa katika sarufi na pia msamiati lakini hata hivyo Waasia huweza kuwasiliana .

## 2.3 LUGHA YA KISWAHILI

Kiswahili ni lugha ya Kibantu. Neno Bantu na lugha zinazoitwa lugha za Kibantu huashiria watu wa familia ya lugha za Nija-Kongo (Guthrie, 1967). Ni jumuia ya lugha zenye asili moja zilizoko Kusini mwa jangwa la Sahara. Jina hilo linatumika kurejelea baadhi ya lugha zinazozungumzwa Afrika ya Mashariki na ya Kati.

Kati ya lugha zinazozungumzwa Afrika Mashariki, lugha ya Kiswahili ndiyo inayozungumzwa kwa upana Kusini mwa Sahara. Zaidi ya watu milioni hamsini huzungumza kwa Kiswahili katika Mashariki na Kati mwa Afrika. Kiswahili ni lugha inayozungumzwa Kenya, Tanzania, Uganda, Rwanda, Burundi na Kongo. Kinatumika katika uongozi wa serikali, biashara, shuleni na vyombo vya kurushia matangazo huko Afrika ya Mashariki na Kati.

Nchini Kenya, kinatumika kama lugha rasmi ya kitaifa. Asilimia hamsini na moja wanaweza kusoma na kuandika Kiswahili nchini Kenya.

Nchini Kenya, lugha ya Kiswahili huzungumzwa kama lugha ya kwanza hasa mwambao wa pwani. Pia nchini Kenya, Kiswahili ni lugha mawasiliano na huunganisha makundi ya watu kutoka mbari tofauti (Munyua, 2002).

Haya yanatokana na ukweli kuwa nchi ya Kenya ina watu mbalimbali ambao lugha zao za kwanza ni tofauti. Kwa hivyo lugha ya Kiswahili hutumiwa kama lugha ya mawasiliano kati ya watu wanaoishi Kenya katika shughuli za kibiashara, kidini, kisiasa na pia katika maingiliano ya kawaida.

Hali kadhalika, Kiswahili ni lugha inayofundishwa kama somo la lazima linalotahiniwa katika shule zote nchini. Aidha, Kiswahili ni somo linalofunzwa katika baadhi ya vyuo nchini ( Mbaabu,1996). Takribani karibu kila sehemu nchini Kenya watu huzungumza lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, matumizi ya Kiswahili ni mengi katika miji mikuu kama vile Nairobi, Mombasa, Nakuru, Kisumu na Eldoret. Hii ni kwa sababu maingiliano katika miji hii yanahusu watu wanaotumia lugha za kwanza tofauti. Lugha ya Kiswahili huwaunganisha na kuwaleta pamoja wananchi wa nchi za Afrika ambao wanatofautiana kidini, kitamaduni,na kijiografia. Katika makala ya "Swahili a Language of Tanzania'' yaliyoko katika ripoti ya Ethnologue Report for Code:Languages of the World (2003), Ngonyani katika makala yake "Languages of Tanzania" anasema kuwa Kiswahili huwezesha makabila tofauti kuwasiliana.

Kulingana na ***Mulika*** jarida na. 25 (1999:33) lugha na fasihi ya Kiswahili inathaminiwa zaidi na kufunzwa kwa dhati Marekani, Korea, Uchina, Urusi, Uingereza na Ujerumani. Uchunguzi uliofanywa unaonyesha kwamba Kiswahili ni lugha ambayo inakua na kuenea kwa kasi sana.

Kwa jumla lugha hii ina upekee katika ufanikishaji wa mawasiliano na ubadilishanaji wa maarifa, ujuzi na teknolojia. Kiswahili kwa sasa kinaziba mianya ya kimawasiliano kati ya wasomi na wasio wasomi wa Afrika Mashariki na Kati na ulimwengu kwa jumla (Amutabi, 2002).

Lugha ya Kiswahili (Mbaabu, 1992 na Mgullu, 1999) ina vokali tano / a/, / ɛ/, /i/, / ɔ/ na /u/. Vokali za Kiswahili hupatikana kama silabi, viishio vya sibabi au katika mwisho wa maneno. Idadi ya konsonanti katika lugha ya Kiswahili ni kubwa zaidi ikilinganishwa na

irabu. Waandishi tofauti wametoa idadi ya konsonanti za Kiswahili kuwa ishirini na tano na ishirini na sita.

Kwa mfano Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala (1988), imetoa orodha ya konsonanti hizi kama, /p/, /b/, /t/, /d/, / č /, /ɟ/, /k/, /g/, /f/, /v/, / ʃ /, /s/, /z/ /h/, / θ/, / ð /,/r/, /l/, / ŋ /, / ɲ /, /n/, /m/, /w/, /j/, na / ɣ /. Kuna konsonanti zinazoambatana na zingine kama vile /nj/, /mb/ na /nd/ (Mutugu, 2001).


Konsonanti za Kiswahili huainishwa kwa kuzingatia mahali pa kutamkia na namna ya kutamka. Jedwali hapa chini inafafanua uainishaji wa konsonanti katika lugha ya Kiswahili.

**Jedwali 2.3 (a)**

| Mahali / Namna | Mdomo | Meno na mdomo | Meno | Meno na ufizi | Ufizi | Kaa kaa gumu | Kaa kaa laini | Koromeo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vizuiwa | p,b | | | | t,d | | k,g | |
| Vikwamizwa | | f,v | θ, ð | ʃ | s,z | | ɣ, ɣ | h |
| Nasali | m | | | | n | ɲ | ŋ | |
| Vizuiwa vikwamizwa | | | | | | č, ɟ | | |
| Kitambaza | | | | | l | | | |
| Kimadende | | | | | r | | | |
| Viyeyusho | w | | | | | | j | |

Wakati wa kutamka vokali midomo inaweza kuwa imevirigwa au iko wazi, ulimi unaweza kuwa juu, chini au katikati mwa kinywa. Kwa kuzingatia hali ya midomo na ulimi , vokali tofauti hutamkwa. Jedwali ifuatayo yaelezea haya:

**Jedwali 2.3 (b)**




Vokali na konsonanti tulizoeleza hutumiwa katika mwingiano na ujitengaji wa kifonolojia. Hata hivyo jambo hili halikuchunguzwa katika kazi hii. Tumezieleza kwa sababu mabadiliko haya yanajitokeza katika maneno yanayotumika wakati Waasia na Waafrika wanaingiliana.

# SURA YA TATU

## 3.0 UTANGULIZI

Kulingana na Laver (1994) tofauti za lahaja za lugha miongoni mwa wazungumzaji hujitokeza katika viwango vya fonolojia, mofolojia, sintaksia, semantiki na leksia vya matumizi ya lugha. Tofauti hizi ni baadhi ya mambo ambayo yanabainika katika matumizi ya Kiswahili kati ya Waasia na Waafrika; pale ambapo Waasia hutumia launi ya lugha ya Kiswahili ambayo ni tofauti na Kiswahili sanifu. Wengi wa Waafrika ambao wana mahusiano ya karibu na Waasia (sana sana ya kibiashara) huwa na umilisi wa Kiswahili sanifu lakini wanapowasiliana na Waasia hubadilisha mitindo ya uneni na kuongea katika launi ya Waasia ya Kiswahili. Kuambatana na Trudgill (1986) na Wallwork (1985), wazungumzaji wa lahaja tofauti za lugha moja ambazo zimekaribiana wanapowasiliana huweza kuhamisha vipengele vya lahaja hizi kutoka lahaja moja hadi ile nyingine.

Wazo hili linatiliwa mkazo na Scherer na Giles (1979) wanaposema kuwa uchaguzi wa lugha kuhusiana na utambulishi wa uneni ni jambo lisilosita kwani sifa za kiisimu katika kikundi fulani cha wazungumzaji hupatikana zikijidukiza katika kikundi kingine tofauti katika viwango tofauti: katika upande mmoja ni kule kuchanganya maneno ya lugha tofauti (Shaffer, 1976; Agheyisi, 1977) na katika upande ule mwingine kabisa ni kule kuweka vibadala vya kifonolojia au kileksia vya kikundi kimoja katika kingine. Kwa hivyo kutokana na utafiti huu inabainika kuwa katika maingiliano ya ana kwa ana, Waasia hubadilisha mtindo wa uneni ili wawe sawa na Waafrika na vivyo hivyo Waafrika hubadilisha uneni ili kufanana na Waasia. Hali inavyokuwa hivyo uneni wa Waasia hubadilishwa na ule wa Waafrika na pia kinyume chake hutokea.

Katika sura hii tutajikita katika usawazishaji wa usemi katika kiwango cha semantiki ambapo maneno ya kimsamiati hubadilishwa na mengine katika maingiliano ya washiriki ili kuwasiliana na kufikia lengo fulani. Usawazishaji wa usemi wa kisemantiki hutegemea maneno mnasaba kwa sababu maana katika lugha hupatikana kupitia maneno. Tutashughulikia kiwango cha semantiki kwa sababu imebainika kuwa katika maingiliano ya Waasia na Waafrika tofauti za kiusemi huweza kujitokeza katika kiwango hiki.

## 3.1 USAWAZISHAJI WA USEMI KATIKA KIWANGO CHA SEMANTIKI

Wakati wa mawasiliano, mwingiano unaweza kutokea kuhusiana na umbomaana. Kwa kuzingatia ujuzi ambao wanaamini wasikilizaji wanao,wazungumzaji wataongea kwa kutumia lugha ambayo itawafanya wawe sawa na wasikilizaji. Kwa mfano, imeonyeshwa kuwa watu hutumia lugha rahisi iwapo wasikilizaji hawana ujuzi sawa nao kuhusiana na mada fulani (Moscovici, 1967). La sivyo msikilizaji atapata shida kujaribu kumwelewa mzungumzaji iwapo maneno yenye maana ya kimsamiati yametumiwa .

'Kufanana' sio kigezo cha pekee cha kuthaminia mtindo wa uneni. Makusudio ya maingiliano ni mengi kama ilivyo miktadha ya maingiliano hayo. Mtindo fulani wa uneni unaweza kuwa tofauti na wakati mwingine mikinzano ya uthamini kutokea tunapolinganisha maana yake katika nyanja tofauti.

Kulingana na Finch (1997) maneno hayawi na maana sawa kila wakati kwa kila mtu. Tukiweka kando wazungumzaji ambao ujuzi wao wa lugha fulani si timilifu, hali itakuwa kwamba maneno mengi hayana maana sawa kwa sababu uelewaji wetu wa maneno hayo

si sawa. Francis 1967: 119 akinukuliwa katika Finch (1997) alieleza kuwa *" maneno hayana maana; watu huwa na maana ya maneno"* (tafsiri yetu ). Tena kwetu maneno huwa na uhusiano wa siri. Maana ya neno pia hutegemea muktadha wa matumizi. Ili kuelewa maana ya maneno inatubidi kuzingatia mazingira, njia ya mawasiliano, na mzungumzaji, kwa hivyo, la maana zaidi katika uelewaji wa maana ni kufasiri (Wallwork,1985).

Maana ya neno haiwezi kusemekana kuwa kwamba haibadiliki au ina msimamo dhabiti – inachukuliwa kuwa maana katika matumizi; neno lililo 'hai' ndilo lijitokezalo katika hali (Gregory, 1978). Uchunguzi wa matamshi binafsi huficha tofauti nyingi, hata katika matamshi yaliyotolewa na mzungumzaji mmoja.

Katika sura hii maneno yatachukuliwa kuwa yanapata maana yake kuhusiana na nafasi yake katika mfumo wa kiisimu ( maana ya kisemantiki) na pia kuhusiana na muktadha wa matumizi na mazingira (maana ya kipragmatiki).

Baada ya kukusanya data kuhusiana na maingiliano ya ana kwa ana kati ya Waasia na Waafrika, ilibainika kuwa kuna usawazishaji wa usemi wa kisemantiki kati yao. Jambo hili linabainika pale ambapo wazungumzaji wanatatumia maneno yenye maana ya kimsamiati kimakusudi kutegemea ukadiriaji wao kuhusu ujuzi wa lugha wa msikilizaji, hali (mazingira) na pia kusudio la mawasiliano. Mzungumzaji atachagua maneno yenye maana fulani kwa kusudi fulani. Uchaguzi huu pia utategemea muktadha, msikilizaji na baadhi ya sifa za msikilizaji. Mzungumzaji hutilia maanani sifa hizi za msikilizaji

ndiposa katika mazungumzo afanye ukadiriaji utakaomwezesha kujisawazisha au kujitenga na msikilizaji na mwishowe afikie malengo yake.

Sehemu inayofuata itabainisha madai yetu. Sehemu hii imegawika katika sehemu sita kuu. Katika sehemu hizo, data itachanganuliwa kwa kuzingatia misingi ya mihimili ya nadharia ya Usawazishaji Usemi na nadharia ya Upekee.

## SEHEMU A

Sehemu hii inahusu mazungumzo yanayoonyesha Waasia wakionyesha mwingiano kwa Waafrika.Wanafanya hivyo kwa kutumia maneno ya kimsamiati katika lugha ya Kiswahili.

**Mfano 3.1.1**

Mazungumzo yafuatayo yanahusu Mwafrika (baadaye AF) mwanaume wa umri wa makamo mnunuzi na Mwasia (baadaye AS) mzee mwenye duka la kuuzia viatu. Mazungumzo yao zaidi yanaonekana ya kirafiki. AS anaonyesha mwingiano kwa AF kama njia ya kupata manufaa ya kibiashara na kikazi.

AF - Msee, unajua wewe hukuelewa *customer* huyo?

AS - Nini? Mimi nimemambie vizuri, yeye apana taka elewa.

AF - Wewe **unakula** maneno, na yeye hapana kuelewa. Hio ndio sababu ukakosana na yeye.

AS - Mimi iko Mhindi. Apana
jua Swahili. Mhindi
**takula** maneno shauri ajui
Swahili, ala! Nini veve?

AF - Mhindi mara nyingi **anameza na kukula**
maneno na hata mimi siku nyingi hapana
kuelewa. Ndio unaona mimi
nikiuliza wewe maswali mingi.

AS - Na pepe lazima ufungue sikio
mzuri apana saa ya kuaribu,
kama mimi **nakula na namesa**
io shauri ya nani? Pungua
sikio kasi naendelea.

Katika mazungumzo hayo (mfano 3.1.1) Mwafrika anatumia neno 'kula' kwa maana ya kule kutotamka maneno wazi naye Mwasia anajisawazisha kwa Mwafrika kwa kutumia neno hilo kuleta maana hiyo hiyo. Neno 'kumeza' pia linatumika lakini halileti maana tofauti na 'kula'. Kula na kumeza zinajumuishwa kuwa na maana sawa.

**Mfano 3.1.2**

Mazungumzo yafuatayo yanahusu Mwafrika (AF) kijana mfanyakazi na Mwasia (AS) kijana katika duka la Mwasia la kuuzia mapambo. Mwingiano katika mazungumzo haya unazingatia kanuni ya Ukweli katika 'Sheria ya Ushirikiano', pale ambapo Mwasia

anatumia maneno ya kimsamiati sawa na Mwafrika. Anafanya hivyo kama njia ya kuendeleza mazungumzo ili apate habari kamili kutoka kwa Mwafrika.

AS - Ilegwa , wewe mjanja sana!

AF - Kwa nini? Iko nini?

AS - Bona mimi inaelezwa
maneno ingine saa hii na Kamau?

AF - Sema nisikie. Umeambiwa nini?
Kama ni maneno ya **kutorokea**
**nyumbani** jana, mimi sina makosa.

AS - Mbona veve **katorokea njumbani**
mapema na kasi iko, mashaara
nagojea misho ya mezi?
Mimi sikia, tasema veve.

AF - Mimi kwisha elezea musee
maneno hayo siku ingine. Nilimwambia
mimi iko na mgonjwa nyumbani
kwa hivyo **tatoroka nyumbani** kumwangalia
halafu narudi kazi.

AS - Namulisa veve, kama **natoroka nyumbani**
veve kwisa nambia mimi?

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

**Mfano 3.1.3**

Haya ni sehemu ya mazungumzo baina ya Mwasia (AS) mama mke wa Mwasia mwenye duka la kuuzia nguo na Mwafrika (AF) msichana mfanyakazi. Msichana anafanya kazi dukani na wakati mwingine anaenda kusaidia kazi ya nyumba kwa Mwasia. Mazungumzo haya yanaonyesha mwingiano lakini mwingiano huu hauzingatii kanuni ya Kiasi ya 'Sheria ya Ushirikiano'. Hata hivyo mwingiano unasaidia wazungumzaji kufikia malengo yao ambayo ni kuendeleza biashara. AS analenga kuona kuwa kazi yake inafanywa naye AF anataka kudumisha kazi na ikiwezekana apate nyogeza ya mshahara. Haya yanatimilika wakati AS anaamua kutumia maneno ya kimsamiati sawa na AF.

AS - Veve ameselewa sana. Kazi gani
namfanya veve selewa?

AF - Uliniambia ningojee **kibiriti ya**
**Mungu itoke** kisha niweke *mattress* nje **nichome**.

AS - Kama **kibiriti ya Mungu naselewa kutoka**
veve nakuja dukani. Kazi iko mingi. *Mattress*
veve **tachoma** saa ingine.
Kuja hapa, tengeleza maguo ote
pande ile, alafu nasaidia mimi apa.

**Mfano 3.1.4**

Mazungumzo haya ni maendelezo ya mazungumzo katika mfano 3.1.3

AF - Mama, tuma Yohana **kuchoma maji**
ya mtoto. Mimi nilifanya kazi na
nikasahau **kuchomea mtoto maji** ya

kuoga. Saa hii ni saa tisa, yeye karibu kuingia.

AS - Yohana iko kazi nyingi saa hii
apana muona. Natoa fagio, nasema na
customer alafu veve iko taka
yeye naende njumbani **kuchoma maji**.
Saa io ote veve apana **choma maji.**
Veve iko shinda mimi. Kama makono
yako apana fanya kasi veve taenda njumbani.

AF - Sasa unachokosa mimi na uoni
ile kazi mimi nafanyie wewe? Mimi
natengeneza chakula, **nachoma maji,**
**nachoma nguo moto**, tena nikifika
dukani wewe unaniambia shika hii, peleka
hii. Uoni hio ni kazi nyingi na
mkono ni mmoja. Kwanza mimi
nataka pesa saidi ya hii kazi.

AS - Wangari, veve kwisa kuwa baya.
Kila siku ongeza pesa, pesa
iko wapi? Mimi nameeleza veve
**maguo nachoma moto** saa moja
tu ya wiki. Apana sikia mimi?

**Mfano 3.1.5**

Mazungumzo yanahusu kijana Mwafrika (AF) mfanyikazi na Mwasia (AS) mzee mwenye duka la kuuzia vitambaa vya kushonea nguo. AS anaonyesha mwingiano kwa AF kimsamiati kama njia ya kutaka kufaidika kutokana na uhusiano wao. AS anajisawasisha kiusemi kwa AF kwa sababu anataka kuona kazi yake ikiendelea vyema.

AF - Mzee, shikilia hii mti. Mimi nataka kukanyanga **niende juu ya duka**.

AS - **naenda juu ya duka** kufanya kasi gani?

AF - Nataka kupeleka hii *material* huko juu. Pale inawekangwa.

AS - Peleka ote juu. Hata ile ingine, zote peleka juu.

Katika mfano 3.1.1 – 3.1.5. , Waasia wanajisawazisha kiusemi kwa Waafrika kwa kutumia maneno ya kimsamiati wanayotumia Waafrika. Katika kila mfano, Mwasia anaonyesha mwingiano –chini kwa madhumuni ya kutaka kufaidika. Maneno ya kimsamiati yanayotumiwa katika mazungumzo haya si ya Kiswahili sanifu. Ni maneno ambayo yanafafanua kitendo fulani. Huu ni ubunifu pia kwa upande wa Waafrika. Jedwali hapa chini linafafanua ubunifu huu.

| **Maneno yaliyobuniwa** | **Kawaida** |
|---|---|
| Unakula (*kumeza*) maneno | Hautamki maneno vizuri (kwa wazi). |
| Kutorokea nyumbani | Kwenda nyumbani |
| Kibiriti ya Mungu likitoka | Jua likichomoza |
| Kuchoma maji | Kuchemsha maji. |
| Kuchoma nguo moto | Kupasa nguo/ piga nguo pasi. |
| Kuenda juu ya duka | Kupanda kwenye paa. |

**SEHEMU B**

Mazungumzo katika sehemu hii yanathibitisha kuwa Waafrika walionyesha mwingiano kwa Waasia kwa kutumia maneno ya kimsamiati katika launi ya Kiswahili ya Waasia.

**Mfano 3.1.6**

Haya ni mazungumzo baina ya Mwasia (AS) mzee na Mwafrika ( AF) wa umri wa makamo. Mwafrika anatafuta nguo katika duka la Mwasia. Mwasia anatumia maneno yenye maana fulani na ambayo kisarufi ni tofauti na kile anakusudia ili kufafanua jambo fulani. Maneno anayatumia kwa kuyahuzisha na dhana fulani. Huu ni uchaguzi wa lugha kimaana wa Kipekee. Anafanya hivyo ili kueleweka na wateja na wafanyikazi ndiposa aweze kuuza zaidi na kuwadumisha wateja na wafanyikazi. Hii inatokana na kule kutokuwa na umilisi wa lugha ya Kiswahili. Pia ni njia ya kurahisisha mazungumzo na papo hapo kufikia lengo lake. Waafrika nao hujisawazisha kwa msamiati huu wanapoingiliana na Waasia ana kwa ana. Wanaonyesha mwingiano kama njia ya kuendelea kuwa na uhusiano mwema wa kikazi. Mwingiano huu utachukuliwa kuwa mwingiano - chini.

AS – *Customer* karibu nguo saiz yote iko.

Nimpe veve nini?

AF – Shati ya mwanamme iko pesa ngapi, hii mimi

naonyesha wewe.

AS – **'budget' iko igapi**, seva, mimi tategezea

Veve msuri.

AF - **budget iko chini**, iko mia mbili.

AS – *'customer'* apana kimbia, nini, kuja, mimi

naseva.

AF – mimi iko mia mbili.

AS – **mafuko iko baridi** au

**mafuko iko moto?**

**Apana enda *ATM?***

AF – **Mfuko saa hii nakwambia**

**ni baridi. (Hapana kuwa moto)** Ala! mwezi iko mbaya.

**Tena mimi naenda *ATM*, hapana narudi.**

Muhtasari wa mabadiliko yanayojitokeza katika matini yamewekwa katika jedwali ifuatayo.

| **Msamiati unaotumiwa na Waasia** | **Maana katika Kiswahili sanifu.** |
|---|---|
| Mafuko iko moto? | Kuna na pesa. |
| Mafuko iko baridi | Hakuna pesa . |
| *'Budgeti'* iko igapi? | Unataka kutumia pesa ngapi? |
| *ATM* hapana narudi | Nilipoenda kwa mtambo wa *ATM* kuchukua pesa sikupata. |

Katika jedwali inayofuata maana kamili ya maneno yaliyotumiwa kwa kuhusishwa na dhana fulani inaelezwa.

| Neno | Maana husishi |
|---|---|
| Moto | -neno hili huhusishwa na wingi, hali ya juu au kuwepo kwa kitu. |
| Baridi | -neno hili huhusishwa na uchache, hali ya chini au kutokuwepo kwa kitu. |
| Budgeti | -neno hili huhusishwa na mpango, jumla ya hesabu ya matumizi. |

Katika utumiaji wa Kiswahili, ilibainika kwamba Waasia hujumuisha au kutumia msamiati rahisi na ambao unatoa maelezo ya kitendo wanacholenga kufafanua. Hali hii huwepo kwa kuwa kama tulivyoelezea mbeleni Waasia wamepungukiwa na ujuzi wa Kiswahili sanifu-yaani mara nyingi huwa hawana msamiati wa kutosha wa kukidhi mawasiliano.

**Mfano 3.1.7**

Hii ni sehemu ya mazungumzo baina ya Mwasia (AS) mwenye duka la kuuzia nguo na Mwafrika (AF1) mwanamke mnunuzi na Mwafrika (AF2) Kijana mfanyikazi. Hapa kuna uchaguzi wa lugha wa Kipekee. Haitarajiwi kawaida mtu kutoka kundi sawa na mwingine kumtenga na kujiunga na mwingine kutoka kundi tofauti. AF2 anajitenga kiusemi na AF1 (Mwafrika mwenzake) na kujisawazisha kwa AS ambaye ni Mwasia. Huu ni ujitengaji usio wa kawaida. Gharama ya kujitenga kwa AF2 kutoka AF1 inaonekana kuwa bora kwa AF2 kuliko kuwa sawa. Hii ni kwa sababu AF2 analenga kumpendeza mwajiri wake (AS). Tena AF2 akijitenga kiusemi kwa mwenzake watafunga kazi na atapumzika.

AS – wewe mama saa hakuna sasa

Kuja kesho, saa subui. Mimi tasaidie wewe.

AF 1– Mbona naharakisha mimi sana.

AS – Hii saa ya **kufunga malango**. Wewe Mutuku, **funga malango**.

AF 2– Mama sisi nataka **kufunga mlango**, saa ya kazi kwisha isha. Kuja kesho.

Jedwali hapa chini inafafanua maana iliyokusudiwa katika matumizi ya maneno yaliyowekwa kwa maandishi mazito.

| Launi ya Kiswahili ya Waasia | Kiswahili sanifu |
| --- | --- |
| Kufunga malango | Kufunga kazi. |

Kule kujumuisha au kurahisisha mazungumzo kwa kutoa maelezo ya kitendo pale mzungumzaji anapopungukiwa na msamiati kunadhihirika tena wakati neno fulani hutumiwa kuelezea mambo mawili tofauti. Maana hueleweka tu kwa kutegemea muktadha wa matumizi na vilevile uhusiano kati ya mzungumzaji na msikilizaji.

**Mfano 3.1.8**

Tazama mfano wa mazungumzo yafuatayo kati ya kijana Mwafrika (AF1) wa mitaani (chokora) na mtoto wa Mwasia (AS) mwenye duka la kuuzia vyuma. Mazungumzo haya hayana mwingiano mbali ni ujitengaji wa kiusemi. AS anatumia maneno ambayo maana yake kwa AF1 ni hasi. Analenga kujitenga kwa AF1 kwa sababu uhusiano wao ni gharama kwa AS. AS akitumia maneno hayo hayo kwa AF2 (Mwafrika mnunuzi) yanatoa maana tofauti ambayo yanakusudiwa kusababisha mwingiano.

AS – Wewe kajana iko taka nini hapa?

AF1 – Kamkate tu *boss.*

AS – Wewe saa ote mkate mkate

Ondoka **konda kabisa** ***( 1)***

( baada ya muda wa saa moja AF1

anarudi dukani akiandamana na AF2)

AF1– Sasa! Wewe unanicheki aje?

Saa hii mimi ni *customer*

Nataka kununua *brakes.* Huyu

*Customer* nimekuletea.

AS – Iko nataka nini

AF1 – Huyu *customer*, natafuta *brakes*

AS – (Kwa mzee anayeandamana na kijana wa mitaani)

Uziwa nini *customer?*

AF2 – (mzee) – Nataka *brakes* za *canter*, ile mimi nanunuanga.

AS – fanya hivi, **konda** pale kwa *(2)*

Patel, *next door*, na yeye tampa wewe *brake*s.

**Konda** ya kwanza inaweza kueleweka kwa njia tatu: kwanza kile kitendo cha kukonda (kudhoofika kiafya) na pia inaweza kueleweka kama kupata shida. Pia inaelezea kumfuta mtu kazi katika mazungumzo ya Waasia. **Konda** ya pili inamaanisha 'enda', yaani 'kwenda pale kwa Patel'.

Maana ya neno hilo **konda** yanategemea muktadha wa matumizi na pia uhusiano wa washiriki.

**Mfano 3.1.9**

Mazungumzo haya yanahusu Mwafrika (AF) Kijana mfanyikazi na Mwasia (AS) mzee mwenye duka la kuuzia vifaa vya ujenzi. AF anajisawazisha kiusemi kwa AS kwa kutumia msamiati wa ujumuishi kutoka launi ya Kiswahili ya Waasia. AS angependa kazi ifanywe kwa haraka ili biashara iendelee naye AF analenga uhusiano mwema na mwajiri wake na angetaka kumaliza sehemu ya majukumu aliyowekewa na mwajiri wake.

AS - **Toa mukono**. Wewe iko kijana<br>na nguvu bado iko.

AF - **Nina toa mkono** lakini ni ngumu.

AS - Kijana **toa mukono** araka .<br>Saa akuna na kazi iko mingi.

Katika mazungumzo haya maneno 'kutoa mkono' ni ya kimsamiati na yanatumiwa kumaanisha 'fanya kazi'.

## MWINGIANO – JUU NA MWINGIANO – CHINI

Kawaida, watu hutambulisha kabila au mbari yao katika mazungumzo (Finch, 1997). Waasia, ingawa ni wachache wakilinganishwa na Waafrika jijini Nairobi wana hadhi ya juu kiuchumi na pia kijamii (Neale, 1974). Ikiwa basi Waafrika hawaelewi uduni wao kwa Waasia kuhusiana na hadhi ya kijamii na lugha, na pia jinsi wanavyojichukua wenyewe kuhusiana na lugha yao, zaidi wataendelea kujisawazisha kwa launi na vitambulishi uneni vya Waasia na kuendelea kujitenga na vile vinavyohusishwa na

Waafrika. Kuhusiana na usawazishaji wa usemi (Giles, 1973;1977) utaratibu huu huitwa mwingiano – juu.

Katika jamii nyingi ambazo zina tamaduni tofauti kuna sheria kuhusiana na lugha ya matumizi katika miktadha rasmi ( Brown na Fraser wakinukuliwa katika Finch 1997; Herman, 1961; Hymes, 1972) na mara nyingi huwa ni ile lugha ya kikundi cha watu chenye hadhi ya juu katika jamii hiyo. Hata hivyo, wakati mwingine hali haiwi hivyo. Kuna wakati ambapo watu wa kikundi chenye hadhi ya juu katika jamii hutumia lugha ya kikundi chenye hadhi ya chini (Scherer na Giles, 1979; Appel na Muysken, 1987). Utaratibu huu huitwa mwingiano – chini. Waasia ambao wamewaajiri Waafrika wanachukuliwa kuwa wenye hadhi ya juu wakilinganishwa na wafanyakazi wao. Wakati Waasia hao wanapojisawazisha kiusemi kwa Waafrika inachukuliwa kuwa wanaonyesha mwingiano - chini.

Katika sehemu inayofuata tutafafanua mwingiano – juu na mwingiano – chini katika mazungumzo.

## SEHEMU C

**Mwingiano juu**

Katika sehemu hii tunafafanua mwingiano – juu wakati ambapo Waafrika ambao wameajiriwa na Waasia wanajisawazisha kiusemi kwa waajiri wao.

**Mfano 3.1.10**

Mazungumzo yafuatayo yanahusu Mwasia (A.S) mzee mwenye duka la kuuzia mapambo na Mwafrika (AF) mfanyakazi. AF anajisawazisha kiusemi kwa AS ambaye ni mwajiri wake kwa kutumia maneno ya kimsamiati sawa na AS.

AS – kuja pande hii.

AF – unasema nini?

AS – **nataka kutia** veve **maneno,**

iko sikia?

AF – **unataka kutia maneno** gani?

AS – kesho nataka wewe aingie subui sana.

Shauri mimi tatuma veve

kachukue masigo ya kazi.

AF – unataka nikuchukue masigo wapi.

AS – Kama veve nakuja mimi tamambia,

veve iko sikia?

AF – Mimi hapana iko shinda ya kuingia kazini mapema. Wewe tapata mimi hapa.

**Mfano 3.1.11**

Mazungumzo haya yanahusu Mwasia (AS) mwajiri mwenye duka la kuuzia nguo na Mwafrika (AF) mfanyikazi. Wanaonyesha mwingiano kiusemi pale ambapo Mwafrika anajisawazisha kiusemi kwa Mwasia kwa kutumia maneno ya kimsamiati sawa na Mwasia. Huu ni uchaguzi unaotarajiwa kwa sababu hili ni jambo la kawaida kwa washiriki wa aina hii. Kujisawazisha kiusemi kunafanywa ili kupata faida kwa wazungumzaji hawa. AS analenga kumvuta AF ili asaidie katika kazi naye AF anajisawazisha kwa AS kiusemi ili adumishe kazi.

AS – veve Nzomo, veve nakaa sana nche.

AF – mimi iko kwenda kula

AS – veve **nakula** soda masaa ote.

AF – mimi **nilikula** chakula na soda, kama wewe kwisha nambia mimi.

AS – keso hapana kaa sana kama **nakula** soda.

Katika mazungumzo hayo hapa juu mfano 3 .1.11 kati ya Mwasia AS (mwajiri) na Mwafrika AF (mfanyakazi), Mwasia anatumia neno 'kula' kwa kuzingatia utangamano wake. Maneno 'kula', 'kunywa' hutokea katika shughuli zinazokaribiana na kwa hivyo Mwasia anatumia neno 'kula' badala ya 'kunywa' kwa sababu matumizi yake ni mengi yakilinganisha na yale ya 'kunywa'. Tena kutamka 'kula' ni rahisi kuliko kutamka 'kunywa'.

**Mfano 3.1.12**

Mazungumzo yafuatayo yanahusisha Mwasia (AS) mzee mwenye duka la kuuzia nguo na Mwafrika (AF) mvulana mdogo. Mwafrika anajisawazisha kiusemi kwa Mwasia kwa sababu angependa kuendelea kufanya kazi kwa Mwasia. Anafanya hivyo kwa kuondoa tofauti za lugha kama njia ya kuwafanya wavutiane.

AS – Nzomo, **kuja chini**.

Hii mita naweka juu ya nini?

Weka kwa mbao.

AS – Mbona wewe kwisa nambia mimi niweke juu.

Si wewe uliniambia hivyo?

**Nakuja chini** halafu uniambie tena enda juu, kazi gani hii?

## SEHEMU D

**Mwingiano – chini**

Katika sehemu hii Waasia (waajiri) wanajisawazisha kiusemi kwa Waafrika (wafanyakazi), jambo ambalo linadhihirisha mwingiano – chini.

**Mfano 3.1.13**

Mazungumzo yafuatayo yanahushu Mwasia (AS) mwenye umri wa makamo anayeuza nguo za wanawake na Mwafrika (AF) mwanamke mnunuzi. Mwasia anajisawazisha kiusemi kwa Mwafrika kama njia ya kutaka uhusiano mwema kati yao na pia Mwafrika aendelee kununua bidhaa kutoka duka lake.

AS – Karibu *Customer*
iko taka nunua nini?

AF – Ngoja **niangalie angalie** na baadaye nitasema ile mimi nataka.

AS – Iko kila kitu
Kuja **angalia angalia** ile veve napenda.

AF – Sema bei ya hii.

AS – Mimi tampa veve na mia tisa.

AF – Bwana, hiyo juu sana **hali mbaya**, punguzia mimi bwana.

AS – **Hali mbaya** na kila mutu, nafikiri mezi dio baya kabisa.
Veve apana ona *custome*r siku izi ameenda ote?
Leta tu mia tisa mimi namemuuzia nguo msuri.

**Mfano 3.1.14**

Mazungumzo haya ni sehemu ya mazungumzo kati ya kijana Mwafrika (AF) na kijana Mwasia AF katika duka la kuuzia vitambaa vya kushonea nguo. Mwasia anajisawazisha kiusemi kwa Mwafrika kwa kutumia maneno ya msamiati sawa na Mwafrika kwa sababu anataka Mwafrika amsaidie kubeba mzingo mzito.

AS – Ongojea mimi nabeba ii nguo tena twendelee.

AF – Sawa, akuna shida.

AS – Wee, apana weza.

AF – Sasa unataka nini?
Kama nataka mimi nikusaidie
ninaweza **kuruka hapo**
na nipeleke na wewe mbele.

AS – **ruka apa** mara moja. Kuja saidia mimi.

AF – Ongoja dakika moja. Mimi nakimbia hapo saa hii.

Katika mazungumzo haya Mwafrika anatumia neno 'ruka' kwa maana ya 'kukimbia', naye mwasia anajisawazisha kwa msamiati huo akinuia kutoa maana hiyo hiyo.

**Mfano 3.1.15**

Haya ni mazungumzo ambayo yanahusu Mwafrika (AF) mfanyakazi katika duka la kuuzia vyuma na Mwasia (AS) mwenye kazi hiyo. Mwasia anaonyesha uchaguzi wa lugha wa kipekee anapojisawazisha kiusemi kwa Mwafrika kwa kutumia lugha ya Kikamba. Uchaguzi huu wa lugha unawafanya wawe sawa kiusemi kama njia ya kutaka kufaidika kutokana na uhusiano wao.

AS – Mutio, fanya araka .

Kuja peleka ii pale.

AF – Mimi siwezi hii peke yangu.

Patel, **ũka ũndetheesye**

(kuja unisaidie)

AS – Mimi **ndikũtetheesya**

(sitakusaidia)

**Nditonya kũũtetheesya**

(siwezi kukusaidia)

AF – Lakini unajua hii chuma mutu mmoja hapana weza.

AS – Enda, mwite Njoroge, yeye tasaidia wewe.

Mimi iko na *customer*.

## SEHEMU E

Sehemu hii inaonyesha mifano ya mazungumzo pale ambapo Waasia wanaonyesha ujitengaji kiusemi kwa Waafrika kwa kutumia lugha zao za kwanza na wakati mwingine Kiingereza.

**Mfano 3.1.16**

Mazungumzo haya ni sehemu ya mazungumzo kati ya Mwasia (AS1) mzee mwenye duka la kuuzia vitambaa vya kushonea nguo, mkewe (AS2) na Mwafrika (AF) mnunuzi. Waasia katika mazungumzo haya wanajitenga kiusemi kwa Mwafrika wanapotumia lugha ya Kiasia (Kigujarati) wakichanganya na Kiswahili.

AS1 anatanguliza mazungumzo kwa lugha ya Kiswahili. Huu ni uchaguzi wa lugha wa kibahatishi kwa sababu hajui kama lugha hiyo itamwezesha kufikia malengo yake (kuuza) lakini anapogundua kuwa AF anafahamu Kiswahili na Kiingereza anaanza kuchanganya lugha hizi mbili katika mazungumzo yao.

Matumizi ya Kiingereza ni uchaguzi wa lugha wa kipekee kwa sababu lugha hii haitarajiwi kutumika katika shughuli kama hii. Hata hivyo, AS1 anatumia lugha zote mbili kama AF kama njia ya kutaka kuonyesha mwingiano ili amvutie AF anunue nguo. Anamvutia kwa kuwa sawa naye kiusemi. Kwa upande mwingine AS1 anajitenga kiusemi kwa AF wakati anapozungumza na AS2 kwa Kigujarati. AS1 hangetaka AF asikie wanapojadiliana bei waone kama wataipunguza. Uchaguzi wa lugha katika mazungumzo haya unafanywa kutegemea ukadiriaji wa haki na majukumu ambazo wazungumzaji wangetaka zihusishwe katika maingiliano. Haki na majukumu zilibadilika wakati washiriki walipobadilika (AS2 akaingilia mazungumzo na AF akatengwa).

AS1 - *Customer* karibu,
iko taka nini?
Sema nguo iko bei msuri.

AF - *Material* hii ya *net*
upana wa *sixty* ni
bei gani mita mbili?

AS1 - Mimi tauzia veve
na *seven hundred* ,
shauri veve ni *customer*,
mimi naona veve apa sana.

AF1 - Hio ni juu zaidi
tena mimi iko taka
mita nyingi , tafadhali
punguza bei.

AS1 - (Kwa AS2)
**Apne bhav ochho kari sakie?**
(tunaweza kumpunguzia bei?).

AS2 - **kefla** igapi?
(iwe ngapi?)

AS1 - **Panchso**
(mia tano)

AS2 - *Customer*, leta
mia tano , mwisho
kabisa sasa.

AF - Nikatie mita kumi na mbili,
hata unaweza kunipatia *discount,*
shauri nimenunua sana.

**Mfano 3.1.17**

Mfano huu ni maingiliano baina ya Waasia wawili (AS1 na AS2) na Waafrika Wawili (AF1 na AF2) katika duka la kuuzia mapambo. AS1 anatumia lugha ya Kiswahili ili kuwahusisha AF1 and AF2 akiwa na lengo la kuona kuwa biashara yake inaendelea. Huu ni uchaguzi wa lugha unaotarajiwa (usio wa kipekee) na ambao unasababisha mwingiano

kiusemi kwa kutumia lugha hii. AF1 na AF2 wanaonyesha uzalendo wao kwa mwajiri wao. Pia haki na majukumu katika maingiliano haya si za kipekee kwa sababu uhusiano huu unatarajiwa baina ya mwajiri na mwajiriwa. Wakati AS2 anaingilia mazungumzo , haki na majukumu na uchaguzi wa lugha unabadilika na kuwa wa kipekee (tukizingatia Waafrika na Waasia). AS1 na AS2 wanapotumia lugha ya Kihindi wanawatenga AF1 na AF2 kiusemi. AS1 angetaka kujitambulisha kijamii na AS2 kulingana na mhimili wa nadharia ya Usawazishaji Usemi wa Kujitambulisha Kijamii.

AF1 - *Customer* atarudi saa nane
kuchukua maua.

AS1 - Umetegelezea yeye?

AF2 - Nilikuwa nimeanza lakini
*customer* wengine wakaingia.
Nitatengenezea yeye saa hii.

AS1 - Angalia io *customer* musuri
yeye iko nunua sana sana apa.

AF2 - Huyo *customer* mzuri zaidi.
Yeye awezi enda duka ingine.
Yeye anasema hapa ni nyumbani.

AS2 - **Bhok lagi he**
(nina njaa)

AS1 - **Ander chal**
(twende ndani)

**cha he**

(kuna chai)

AS2 - Nataka **chahi ye**

( … chakula)

AS1 - (Kwa AF)

Kuja apa. Simamia apa shauri

ya *customer*. Mimi tarudi saa hii.

**Mfano 3.1.18**

Yafuatayo ni maingiliano baina ya Waasia (AS1, AS2 na AS3) wote wazee na vijana Waafrika (AF1 na AF2) wawili (Mkikuyu an Mkamba). Waasia wanajitenga kiusemi kwa Waafrika wanapotumia Kigujarati. Katika mazugumzo haya AS1, AF1 na AF2 wanaonyesha mwingiano ambao unatokana na uchaguzi wa lugha unaotarajiwa. Wanatumia lugha ya Kiswahili. Haki na majukumu si ya kipekee kwa sababu huo ndio uhusiano unaotarajiwa. Lakini AS1 anachagua lugha kwa namna ya kipekee anapoongea na AF2 na AS2 kwa Kigujarati. Hili halitarajiwi kwa sababu AF2 hakifahamu Kigujarati. Hata hivyo AS1 anafanya hivyo ili kujitenga kiusemi kwa AF1 kimakusudi na kumhusisha AS2. Mshiriki mwingine tofauti (AS2) anapoingia uchaguzi wa lugha na haki na majukumu yanabadilika na kuwa ya kipekee.

AF1 - Mzee, huyo *customer*

hapana patia mimi pesa

yote. Amesema atarudi jioni….

AS1 - Io ni rogo, veve iko
danganya saa ote.

AS2 - Kwa nini veve chukua
pesa na siku nyingi mimi
iko mambia veve kama
*customer* nanunua veve
nampa mimi pesa.
Sema,apana iko sikio?

AS3 - (kwa AS1 na AS2)
Wakikuyu **kharab** watu **che**
( … wabaya …ni)

AS1 - **Ane kadi nak**
(fukuza yeye)

AS2 - Wanyoike, sema musuri,
mimi naita polisi saa hii
kama veve apana nimpa
mimi pesa.

AF2 - (kwa AS2) Mzee, mimi
nimekwisha elezea wewe-huyu
jamaa taingiza wewe kwa shida.

AS2 - Wewe kwisha nimambia mimi
Wanyoike iko makono baya!

AF2 - Na Wanyoike ameenda

wapi saa hii?

AS1 - (Kwa AF2 na AS2)

Angalia yeye nche

**Jaldi key e nikle** atoke

(Kimbia kabla…)

AS2 - (kwa AS1 na AS3)

***Nai awade***

(msimruhusu)

AS3 - **Nai** kubali

(kamwe…..)

**Mfano 3.1.19**

Haya yalikuwa maingiliano kati ya mwanamke Mwafrika (AF) akinunua dawa katika duka la kuuzia dawa la Mhindi na Mhindi (AS1) mwenye duka. Baadaye Mhindi mwingine (AS2) anaingilia mazungumzo yao. Wahindi wanajitenga kiusemi kwa Mwafrika kwa kutumia lugha za Kiasia (Kigujarati na Kihindi kwa pamoja).

AF anaanza mazungumzo kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu inatarajiwa kwamba Kiswahili kinafahamika na watu wote; ambao ni uchaguzi wa lugha usio wa kipekee. Baadaye anapogundua kuwa AS1 anazungumza Kiingereza anaanza kutumia Kiigereza pia. Matumizi ya Kiingereza ni uchaguzi wa lugha wa kipekee kwa sababu lugha ya Kiingereza haihusishwi na shughuli kama hii. Hata hivyo ubadili huo wa lugha kati ya AF na AS1 unalenga kuwasaidia kufikia nia zao (AF apate dawa na kwa bei inayomfaa

na AS1 apate kuuza). Hapa AF anaonyesha mwingiano-juu. Anafanya hivyo baada ya kufanya ukadiriaji wa gharama na manufaa zitakazofuata uchaguzi wake.

Sehemu ya mwisho ya mazungumzo haya inaonyesha ujitengaji kiusemi. Haya yanadhihirika pale ambapo AS1 na AS2 wanaanza kuongea kwa kutumia maneno ya kimsamiati ya Kigujarati na Kihindi kama AF anasikiliza. Wanafanya hivyo ili kujitambulisha kijamii na pia kama njia ya kuelezea masaibu yao bila kumshirikisha AF.

AF - Nataka dawa ya minyoo
ya mtoto miaka mbili.

AS1 - Iko dawa ya minyoo
kabila nne (anamwonyesha).
Angalia, taveva igani?
*Which one do you prefer?*

AF - Ni gani *effective* zaidi?

AS1 - Hii ya shilingi mia moja
taondoa minyoo yote,
ni suri saidi.
(AS2 anaingia dukani)
(AS1 kwa AS2)
**Chho kem?**
(yako habari?)

AS2 - **Chhe saroo**
(yangu habari salama).

AS1 - Kazi **bandh karvu**

(…kupunga tunataka)

AS2 - Kazi **kharab che**

(… baya siku hizi)

**Bhau oocho ker**

(punguzia yeye bei)

AS1 - (Kwa AF)

*Customer* , leta *eighty shillings*

AF - Utachukua *sixty?*

AS1 - Hapo veve sasa taumiza kazi.

Dawa iko ongezea bei mara bili

hii maka, shauri ya *tax*.

AS2 - (Kwa AS1)

**aa mana saro** msuri

(huyu mtu ni…………)

**Mfano 3.1.20**

Mazungumzo yafuatayo yanahusu Waasia vijana (AS1 na AS2) na mfanyakazi wao Mwafrika (AF) mzee katika duka la kuuzia nguo. Waasia wanajitenga kiusemi kwa Mwafrika kwa kutumia Kiingereza.

AS1 na AS2 wanapotumia maneno ya Kiingereza wanamtenga AF kiusemi kwa sababu hakifahamu. Wanapofanya hivyo wanaonyesha uchaguzi wa lugha wa kipekee. Sio

jambo la kawaida/ linalotarajiwa vijana kuzungumza na wazee (wasiosoma) kwa kutumia lugha ya Kiingereza.

AS1 - (Kwa AF)

Ongea na **customer** apana

angalia bila kusema.

AF - (Kwa mteja)

Mama unataka nini?

Nguo iko kabila yote.

AS1 - (Kwa AS2)

**This old man fears talking to people.**

(huyu mzee anaogopa kuongea na watu).

AS2 - Mzee **said he may replace him** na kijana

(.... alisema atambadilisha .........)

AS1 - **A young man** atafaa **for this work.**

(Kijana ........ kwa hii kazi)

AS2 - (Kwa AF)

Mzee wacha kuniangalia

uzia **customer** nguo.

**SEHEMU F**

Sehemu hii inaonyesha mazungumzo ambayo yanadhihirisha ujitengaji wa Waafrika kiusemi kwa Waasia wanapotumia lugha zao za kwanza.

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

**Mfano 3.1.21**

Mazungumuzo yafuatayo yanahusisha vijana wa Kiafrika wawili (AF1 na AF2) ambao wameajiriwa na Mwasia AS katika duka la kuuzia vyuma vya magari . Wote wanakuwa sawa kiusemi wanapotumia msamiati sawa katika mazungumzo yao. Kila mmoja analenga kupata faida na kuepuka gharama itokanayo na tofauti za kiusemi. Hata hivyo AF1 na AF2 wanajitenga kiusemi wanapotumia lugha ya Kikamba ilhali AS anawasikiliza.

AF1 – Kimeu kuja saidia tupandishe
hii kitu.

AF2 – Kitu gani? Wewe hapana sikia
vile mdosi kwisha ambia wewe.

AS – Veve kichwa baya nini, veve apana
sikia mimi namesema **toa fagio**.
Kamata iko **toa fagio** sana haraka.

AF1 – Mimi nilitaka kupandisha hii nguo
tena nianze kufagia.

AF2 – (Akimchekelea AF1) Tafadhali
**toa fagio** vile mdosi anasema.

AF1- **Mwanoo ekana na ũtũndũu.**
(Jamaa wacha ujinga)
**Ti** lazima **nĩke ũndũ waasya.**
(Sio ……. nifanye yale anasema.)
**No nĩlee na ndĩnũka kwitũ, ndaaũaana.**

(Naweza kukataa na nirudi nyumbani, sikuua huko.)

AF2- **Kamwana ndũlee twone.**

(Kijana kataa tuone.)

**Ndwĩte mũtu nthĩ *(kicheko)*.**

(Aribu kazi .)

**Mfano 3.1.22**

Mazungumzo yanahusu Mwasia (AS) mwenye duka la kuuzia vyuma na Waafrika wawili (AF1 na AF2) wafanyakazi. Waafrika wanajitenga kiusemi kwa kutumia lugha ya Kikamba. Kwa kutumia maneno ya kimsamiati ya Kikamba AF1 na AF2 wanajitenga kiusemi kwa AS (ambaye haelewi Kikamba). AF1 anatarajia kwamba akimhusisha AF2 na kumtenga kiusemi AS watasaidiana na AF2 kutatua shida inayomkabili. Anajisawazisha kiusemi kwa AF2 kwa sababu kufanya hivyo kuna faida kwake kwani tayari AS amekataa kumtimizia haja yake (ya pesa). Hapa AF1 anafuata mihimili miwili ya nadharia ya Usawazishaji Usemi ya Kukadiria Gharama kati ya Wanajamii na Kujitambulisha Kijamii. Hali kadhalika, matumizi ya Kikamba baina ya AF1 na AF2 ni dhihirisho la uchaguzi wa lugha wa kipekee (usiotarajiwa).

AS - Mimi kwisha nambia

apana taka deni saidi.

Kamata alfu moja.

AF1 - Mimi nilikwambia niko

na shida nyumbani. Mtoto

yangu ni mgonjwa na

ninataka *advance*, elfu mbili.

AS - Apana weza alfu bili.

Mimi nakwambia panga maneno

yako sawasawa, alfu bili apana.

AF - Nipatie pesa elfu mbili

ya kupeleka mgonjwa

hosipitali. Kazi mimi

nafanya mzuri.

AS - Kwa wiki bili veve nafanya

saa kidogo, wewe nakaa nche

sana , wewe safari mingi wewe

naandikwa a*bsent*. Naona!

AF - (Kwa AF2)

**Wĩa ũũ nĩngũvuta. Nditonya kũthũkũma .**

**mwana wakwa atiw'a naĩ.**

(Kazi hii nitaacha. Siwesi kufanya kazi

mtoto wangu akiwa mgonjwa).

AF2 - **Osa silingi isu ngili imwe na**

(Chukua hiyo elfu moja na)

**Wasyoka mukaneena**

(ukirudi uende muongee).

**vai maana ma kũthokoana nake**

(hakuna haja ya kukosana naye)

maisha ni magumu bila kazi.

AF1 - Wacha nizungumze tena na *boss*

AF2 - Lakini ameenda kuomba

**oyu nĩ saa nyanya**

(Sasa ni saa nane)

**Mfano 3.1.23**

Maingiliano yafuatayo yanahusu vijana wawili Wameru (AF1 na AF2) na Waasia wawili (AS1 na AS2) . Mazungumzo yanadhihirisha ujitengaji kiusemi wakati vijana Wameru wanatumia maneno ya Kimeru katika mazungumzo yao. Mazugumzo yanafanyika katika kiduka cha vifaa vya gari.

Kwa kutumia maneno ya kimsamiati ya Kimeru, AF1 na AF2 wanawatenga AS1 na AS2 kiusemi katika kiwango cha semantiki. Ujitengaji hapa ni dhihirisho la uzingativu wa mhimili wa nadharia ya Usawazishaji Usemi wa Kujitambulisha Kijamii.

AS1 - Mbogo, peleka *carton store.*

AS2 - Lakini usiweke juu ya *glass.*

AS1 - Angalia , weka chini ya bao pale.

AF1 - (Kwa AS1)

Saidia, hii kitu mzito.

AF2 - Kwani wewe hapana kula leo?

AF1 - Nisaidieni, hii ni chuma,

wacha mchezo.

AS1 (Kwa AF2)

Kamanda, saidia Mbogo,

peleka *carton* bole bole,

apana anguka.

AF1 - (Kwa AF2)

Leo **tũgeta** ***south C?***

(…. tutaenda *south C*)

AF2 - **Tugeta kũthithia atĩa**?

(kufanya nini?

AF1 - **Nĩnkwenda kũmwona mwarĩ wetũ**

(nataka kumwona dada yangu).

AF2 - **Ndathiria ngũgĩ** naenda kuosha nguo

(Nikimaliza kazi …)

mimi si kama wewe **mwekũrũ wakwa arĩ kũraja**

(………………….. mke wangu yuko mbali)

AS2 - Apana potesa saa ote kama naongea.

Kuja endelea kazi

AF1 - Hio *carton* nzito, inakata mtu mgogo.

**Mfano 3.1.24**

Yafuatayo ni maingiliano baina ya Mwafrika mfanyakazi (AF1) katika duka la Mhindi la kuuzia nafaka , mteja Mwafrika (AF2) na Mwasia mwenye duka (AS). Baada ya kuongea kwa muda, AF2 anagundua kuwa anatoka sehemu ya huko mashambani sawa na AF1 (wote ni Waluyia). Jambo hili linawafanya waanze kuongea kwa kutumia lugha ya Kiluyia na kwa kufanya hivyo wanamtenga AS kiusemi. Kama inavyodaiwa katika

nadharia ya Upekee, wakati kipengele kimoja au zaidi vya kihali vinavyobadilika jozi ya haki na majukumu zisizo za kipekee nazo huenda zikabadilika (Scotton 1993:144). Katika mazungumzo haya, AF2 anapogundua kuwa anatoka katika kabila sawa na AF1, mitazamo kuhusiana na mmoja kwa mwingine inabadilika: wanaanza kuangalia uhusiano wao vingine (kama ndugu), papo hapo nayo jozi ya haki na majukumu inabadilika kwani wanaanza kuzungumza mambo ya nyumbani. Ugunduzi huu pia unawafanya wafanane na kwa hivyo kuwepo kwa mvuto kati yao, kuambatana na mhimili wa nadharia ya Usawazishaji Usemi wa Kufanana-Kuvutiana

AS1 - Ongea na *customer* ameingia , uzia yeye.

AF1 - Karibu ndani. Nikuuzie nini?

AF2 - Nataka maharagwe aina ya *Roscoco.*

AF1 - Aina hiyo iko.Utaona kwanza?

AF2 - Wacha nishike nione. Hii mnatoanga wapi?

AF1 - Siwezi kujua, lakini nasikia huyu (akiashiria AS) akiniambia kuwa *Weekend* alikuwa kwetu –Kitale

AF2 - Kwani wewe ni wa kutoka Kitale?

AF1 - Ndio, huko ndio nyumbani

AF2 - **Oluranga** Kitale wapi?
(unatoka…………?)

AF1 - Karibu **ende mtown** kilomita **nsibiri** hivi
(…… na mji……… mbili……)

**Nisei omwisukha**

(Mimi ni Mwisukha)

**Mfano 3.1.25**

Mazungumzo yafuatayo yanahusu Mwasia (AS) mwenye duka la kuuzia nguo na mfanyakazi Mwafrika (AF1) na mteja Mwafrika (AF2).

AF2 anajuana na AF1 na wanaongea lugha sawa (Kikuyu). AF2 anataka nguo kwa bei nafuu na anatumia uhusiano wake na AF1 kujadiliana bei. Wanatumia lugha ya Kikuyu na hivyo kumtenga AS kiusemi . Haya yanaambatana na madai ya mhimili wa nadharia ya Usawazishaji Usemi wa Kukadiria Gharama kati ya Wanajamii.

AS - Mbona leo kazi iko baya?

AF1 - Mwezi ni baya pia.

Lakini kuna *customer* aliniambia

atakuja leo saa nane , yule kijana

wa Murang'a. Wewe unajua yeye.

AS - Pigia yeye simu, angalia kama

iko taka nguo. Yeye anafanyia

sisi kazi musuri.

(Baada ya muda wa nusu saa)

AF1 - ( kwa AF2)

Kwani **uma kũ** nikikupigia simu?

(.......ulikuwa wapi **ngikũhũrĩra thimũ?)**

AF2 - **Ndatinda jamu-inĩ**

(Nimekuwa kwa jam)

**ithaa rĩmwe.**

(kwa muda wa saa moja)

**Ika atirĩrĩ, ũmũthĩ ndirenda**

( Fanya hivi, leo nataka)

**indo nyingĩ .**

(mali kwa wingi)

**Na thogora *ũ*korwo wĩmwega,**

(Bei lazima iwe sawasawa)

. **aria na m*ũ*nene.**

(Ongea na boss).

Kwa kuzingatia matokeo ya kufasiri maana ya kilichosemwa kwa kuhusisha mtindo fulani wa uneni, kifanani tambuzi kuhusiana na maingiano kimeonyeshwa na Larsen, Martin na Giles (1977) ambao waligundua kwamba wasikilizaji ambao walimfikiria mzungumzaji kuwa wa hadhi ya juu, na mwenye mamlaka na ambao wangependa maingiliano kati yao na mzungumzaji yaendelee siku zijazo, waliuelewa uneni wa mzungumzaji kama ni sawa na ule wao, kinyume na wasikilizaji ambao hawajui chochote kuhusu mzungumzaji. Hali kama hii inabainika katika baadhi ya maingiliano kati ya Waasia na Waafrika.

## 3.2 SIFA BAINIFU KATIKA USAWAZISHAJI WA USEMI WA KISEMANTIKI

Katika kuchunguza njia zinazofuatwa na wazungumzaji binafsi wakati wa usawazishaji wa usemi, jambo muhimu linalostahili kuzingatiwa ni ile haja ya kutaka kueleweka (Trudgill, 1986). Katika utafiti huu tunashughulikia maingiliano kwa kutumia launi ya Kiswahili ya Waasia na Kiswahili kitumiwacho na Waafrika katika maisha ya kila siku kwa hivyo kuelewana kwa Waasia na Waafrika sio shida kubwa au ya kudumu. Hata hivyo, wakati mwingine inaweza kuwa shida kwa muda, na wazungumzaji mara moja wanaanza kuwa na ufahamu kuwa sifa fulani za lugha (maneno katika sura hii) huenda zikawa na utata kuliko zingine. Swala tunalojaribu kufafanua hapa ni kwamba, je ni sifa zipi bainifu zinazobadilishwa katika usawazishaji wa usemi wa kisemantiki kati ya Waasia na Waafrika?

Uchunguzi wa maingiliano kati ya Waasia na Waafrika unaelekea kueleza kuwa Waasia wengi jijini Nairobi hawajakimudu Kiswahili sanifu. Hata hivyo wanayo njia yao ya matumizi ya Kiswahili inayowawezesha kuwasiliana na Waafrika. Hii ni pamoja na kule kujumuisha dhana ili kurahisisha mazungumzo na papo hapo kuelewana. Kwa hivyo watatumia neno moja ambalo kwao linaweza kuingia katika miktadha tofauti na kuleta maana tofauti. Hata hivyo matumizi ya maneno fulani yanategemea muktadha, uhusiano kati ya washiriki na pia mada. Matumizi ya maneno hayo mara kwa mara hujitokeza katika uneni wa Waafrika. Waafrika watayatumia kutoa maana ile ile katika uneni wa Waasia.

Ujumuishi tunaozungumzia hapa ni pale neno au maneno fulani yanaweza kupata matumizi katika miktadha mbalimbali. Neno linatumiwa kwa kijumla ili kujumuisha

shughuli au vitendo vingi ambavyo vinahusiana. Ujumuishi huu unajikita katika sifa za kitendo, kitu au jambo. Aidha, maumbile ya kitu na jinsi kinavyotenda kazi huelezewa kwa njia hii.

Ufupishaji nao unatokea pale ambapo sehemu ya neno hutumika badala ya neno nzima. Inaelekea kuwa kutamka sehemu ya neno ni rahisi kuliko kutamka neno nzima. Ufupishaji unafafanua sifa za kitendo, jinsi ya utenda kazi wa kitendo au tabia ya kitu. Kwa jumla aina hii ya ubunifu kwa upande wa Waasia ni kutaka kuwasiliana na Waafrika, waelewane na kufikia malengo fulani. Ilibainika kuwa Waasia hawana umilisi kamili wa lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo ili kutumia lugha hii wanalazimika kubuni namna ya kuzungumza. Inakisiwa ujumuishi na ufupishaji huu una chanzo chake katika athari za lugha za Kiasia.

Mfano wa maneno haya ni kama:

**Mfano 3.2.1**

1. Kula- ni neno ambalo kwa Waasia hutumiwa kuelezea aina yoyote ya kujipatia riziki ikiwa ni pamoja na vinywaji.
2. Konda- neno hili huwa na maana nyingi kutegemea muktadha, uhusiano kati ya washiriki na cheo chao. Kwa mfano, linaweza kumaanisha kufutwa kazi, kuwa na afya mbaya , kupata taabu na pia kwenda.
3. Shauri- hutumiwa na Waasia kuashiria 'sababu ya' 'kwa niaba ya', na 'ili'.
4. Bure- neno hili nalo hutumiwa na Waasia kuleta maana ya 'mtu asiyetumia bongo', 'jambo lisilowezekana' na 'mtu/kitu kisicho na maana'.

Sifa nyingine bainifu ya matumizi ya Kiswahili katika maingiliano ya Waasia na Waafrika ni ule ufupishaji au utumiaji kwa mkato wa maneno. Waasia katika kutumia Kiswahili hutumia maneno kwa mkato. Viambishi awali vya vitenzi na nomino katika lugha ya Kiswahili huondolewa na neno kutumika likiwa ni sehemu tu ya neno.

**Mfano 3.2.2**

Tazama sentensi zifuatazo.

a) Veve (toto) iko angalia wapi?

b) Mimi apana (taka) kelele

c) Veve iko (sema) nini?

Maneno 'toto','taka', na 'sema' si kamili; kuna viambishi ambavyo vimeondolewa. Kulingana na sentensi hizi maneno haya yalifaa kuwa

Toto - *m*toto

Taka - *una*taka

Sema - *una*sema

Matumizi ya maneno haya ya mkato (yaliyofupishwa) mara kwa mara yatapatikana katika mazungumzo ya Waafrika.

Kando na ujumuishi na ufupishaji wa maneno katika matumizi ya Kiswahili , Waasia pia hutumia maneno kihusishi. Neno fulani linatumiwa kwa sababu linahusishwa na dhana au kitendo fulani. Mara nyingi maneno mawili yatatumiwa pamoja kuelezea dhana / kitendo ambacho kinahusiana na maneno hayo ingawa maneno yenyewe yana maana tofauti.

**Mfano 3.2.3**

i) Toa fagio - hutumiwa kumaanisha kufagia. Neno 'toa' hapa linahusishwa na kazi ifanywayo na kifagio ya kutoa au kuondoa uchafu.

ii) Funga malango (mlango)- hutumiwa kuelezea ile hali ya kufunga kazi na watu kuenda nyumbani. Mahali pa kazi kama vile dukani huwa na mlango (wa kuingilia na kutoka ndani ya duka). Kawaida watu wanapofunga kazi kabla ya kwenda nyumbani hufunga milango ya mahali pa kazi kwa hivyo 'kufunga mlango' hutumiwa na Waasia kuelezea kitendo cha kufunga kazi.

Wanapowasiliana na Waasia, Waafrika watatumia maneno kama toa fagio, funga malango, na hapo kufikia maelewano. Hizo sifa ambazo zinapatikana katika uneni wa Waasia hudhihirika katika uneni wa Waafrika kama ishara ya kuwepo kwa usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika.

Sifa moja kuu ya athari za lugha za kwanza katika matumizi ya Kiswahili baina ya Waafrika, sana sana wale kutoka kundi la Wabantu ni kule kuongezea kiambishi awali *ka* –ili kuelezea udogo wa kitu au jambo. Pia Waafrika huweka kiambishi tamati *nga* kuonyesha uzoefu wa kitendo. Hali kadhalika, Waafrika wana sifa ya kuweka kiambishi tamati – *ko* katika maneno.

**Jedwali 3.2.4**

| **Kiswahili sanifu** | **Kiswahili chenye athari za Kiafrika** |
|---|---|
| Kitu kidogo | Kakitu (Wabantu wengi) |
| Mkate mdogo | Kamkate (Wabantu wengi) |
| Msichana mdogo | Kasichana (Wabantu wengi) |
| Kuimba mara kwa mara | Kuimbanga (Wabantu wengi) |
| Kununua mara kwa mara | Kununuanga (Wabantu wengi) |
| Kula mara kwa mara | Kulanga (Wabantu wengi) |
| Mchezo | Mchezeko (Waluhya) |
| Niambie | Niambieko (Waluhya) |
| Twende | Twendeko (Waluhya) |

Mara kwa mara, Waasia wanapowasiliana na Waafrika utawapata wakitumia maneno haya ambayo yameathiriwa na lugha za kwanza za Waafrika.

Kulingana na Finch (1997) maana kama fasili ya dhana akilini ni ya aina mbili: maana ya kimawazo na maana husishi .

Watu wengi huelewa maneno katika msingi wa maana ya kimawazo. Ni kile neno fulani linachukuliwa kuashiria, yaani ishara ya neno au maana halisi ya neno.

Maana husishi ni maana ya neno kutegemea uhusiano wake na miktadha ya matumizi ya kijamii na kiutamaduni ya matumizi ya neno. Kuambatana na maana husishi ya neno kuna taratibu kuu ambazo huathiri maana za maneno:

- Kidokezo: Vidokezo ni amali na mitazamo inayohusishwa na neno, kando na maana yake halisi. Hizi hutegemea utamaduni wa jamii na hubadilika kiwakati.
- Tangamano : Ni utokeaji/uendaji pamoja wa maneno.
- Mtindo kibadala : Hapa maneno hutambulishwa kimtindo – hutumika kutegemea rejista.

Fasiri hizo zote za maana zinajitokeza katika uelewaji wa maana za maneno katika matumizi ya Kiswahili kati ya Waasia na Waafrika. Kwa sababu Waasia wengi hawana umilisi wa Kiswahili sanifu, wanaishia kujumuisha maana za maneno wanapotumia lugha ya Kiswahili . Aidha, wanachagua neno kulingana na amali na mitazamo inayohusishwa na neno hilo, kulingana na utangamano wa neno na mwisho kutegemea rejista ya neno fulani linapotumika.

Kulingana na maelezo hayo inaelekea kuwa Waafrika hujisawazisha kiusemi kwa Waasia katika kiwango cha semantiki kwa kiasi na hivyo ndivyo ilivyo Waasia kwa Waafrika. Pia inaelekea kuwa ule ubunifu kwa upande wa Waasia wa kubadilisha Kiswahili sanifu umepokelewa na Waafrika zaidi kuliko vile Waasia wanavyotumia maneno yenye athari za kwanza za lugha za Kiafrika. Makundi haya yote yanaonyesha mwingiano moja kwa lingine lakini Waafrika katika kiwango cha maana katika matumizi ya lugha wanaiga Waasia zaidi. Waasia kwa kiasi fulani wanajitenga kiusemi pale ambapo wanadumisha matumizi ya Kiswahili ambacho wao wenyewe wamekibadilisha kwa namna fulani kikawa tofauti na Kiswahili sanifu.

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

### 3.3 HITIMISHO

Katika sura ya tatu tumechunguza usawazishaji wa usemi wa kisemantiki na mambo kadhaa yakajitokeza. Kwanza Waasia katika maingiliano yao na Waafrika walionyesha mwingiano kwa Waafrika kwani walibadili usemi wao kwa kutumia maneno ya kimsamiati ya lugha ya Kiswahili ambacho ni lugha ya Kiafrika na pia zaidi kwa kutumia Kiswahili chenye athari za lugha za kwanza za Waafrika. Aina hii ya mwingiano itaitwa mwingiano-chini kwani Waasia waajiri wanachukuliwa kuwa na hadhi ya juu kiuchumi wakilinganishwa na waajiriwa wao. Lengo la Waasia kufanya hivi ni kupata manufaa ya kibiashara, kudumisha wafanyikazi na pia kukubalika katika nchi geni (kuonyesha ushirikiano).

Waafrika nao waliweza kuonyesha mwingiano-juu pale ambapo walijisawazisha kiusemi kwa Waasia kwa kutumia maneno ya kimsamiati kutoka launi ya Kiswahili ya Waasia katika mazungumzo. Madhumuni ya mwingiano–juu kwa Waafrika ni kule kudumisha ushirikiano na Waasia na pia kufaidika kikazi.

Kwa upande mwingine,ujitengaji wa kisemantiki ulibainika. Ujitengaji unadhihirika pale ambapo Mwasia anatumia lugha yake ya kwanza na Mwasia mwezake ilihali msikilizaji ni Mwafrika na vivyo hivyo Mwafrika kwa Mwafrika, msikilizaji akiwa Mwasia. Ujitengaji pia unadhihirika pale ambapo Mwasia anatumia Kiingereza wakati anazungumza na Mwafrika ambaye hajakimudu sana Kiingereza.

# SURA YA NNE

## 4.0 UTANGULIZI

Sintaksia kulingana na Finch (1997) ni upangaji wa maneno katika uneni ili kuunda mikufu iliyopangika vizuri. Hii mikufu humaanisha mfuatano wa maneno kama vile virai, vishazi na sentensi. Polome (1982) anaelezea kuwa msemo wa kiisimu au muundo wa tamko unaweza kuwa tofauti kutegemea uchaguzi wa maneno, upangaji wa maneno, fonolojia, kiasi , kiimbo, na kadhalika. Tazama mfano ufuatao:

**Mfano 4.0.1**

a. Mtoto alimpiga paka

b. Paka alipigwa na mtoto

c. Paka alimpiga mtoto.

Sentensi *a* na *b* ni tofauti katika mapangilio wa maneno lakini zina maana sawa. Hali kadhalika sentensi *c* ni sawa na *a* na *b* kileksia lakini maana ni tofauti.

Maingiliano ya lugha huleta athari katika lugha husika katika viwango vyote: kifonolojia, kisarufi, kileksia, lakini kwa kiasi tofauti kutegemea namna ya muda wa maingiliano ya kitamaduni yanayohusika (Trudgill, 1986). Ruwaza za kisintaksia mara nyingi hubadilika bila ugumu, lakini kubadilika kabisa kwa muundo wa kisintaksia wa lugha fulani huchukua muda mrefu wa maingiliano wakati ambapo hadhi ya kijamii ya lugha moja hufanya jukumu kuu. Lakini hata hivyo, hali haiwi hivi kila wakati. Kwa mfano, Kiswahili kando na kuwa na maingiliano na Kiarabu kwa karne nyingi kimedumisha mfumo wa kisintaksia wa Kibantu (Finch 1997).

Wazungumzaji wawili wanaozungumza lugha moja lakini lahaja tofauti wanaweza kutofautiana kisintaksia (Mathooko, 2004; Finch 1997; Kebeya,1997; Trudgill, 1986).

Neno ndicho kipashio cha msingi katika sentensi na maneno tofauti hufanya kazi tofauti kisarufi katika sentensi.

Kila lugha huwa na utaratibu maalum wa kupanga vipashio katika sentensi na kujua lugha ni kuelewa kanuni zinazoongoza upangaji wa vipashio hivi. Hapa itachukuliwa kuwa sintaksia inahusu mpangilio wa maneno katika sentensi na jinsi mpangilio unaathiri maana. Katika sehemu inayofuata tutachunguza miundo ya sentensi katika lugha ya Kiswahili na launi ya Kiswahili ya Waasia ili kuona jinsi miundo hii inavyoingiliana wakati Waasia wanapowasiliana na Waafrika.

## 4.1 MUUNDO WA SENTENSI KATIKA LUGHA YA KISWAHILI

Kila lugha huwa na muundo unaozingatiwa wakati wa kuchanganua lugha hiyo.

Kunazo aina tofauti tofauti za maneno na maneno huunganishwa kuunda virai navyo virai huwekwa pamoja kuunda sentensi. Katika uundaji wa sentensi, maneno tofauti huchukua nafsi tofauti katika sentensi. Kuambatana na maoni ya Wanasarufi Miundo Virai, uchaguzi wa miundo ya tungo hufanywa kwa kuzingatia mpangilio wa maneno katika sentensi. Muundo wa kimsingi wa sentensi ya Kiswahili unaofuata na wanaisimu wengi ni mtendaji- kitenzi-kitendewa pamoja na vivumishi vinanyowekwa karibu na kipengele kinachovumishwa (Loogman, 1965; Russell, 1986).

Hali kadhalika, sentensi ya Kiswahili ya kimsingi huchukuliwa kuwa na sehemu mbili kuu: yaani, sentensi (S) itachanganuliwa kama Kirai Nomino (KN) na Kirai Kitenzi (KT), kwa ishara ni:

S ⟶ KN + KT.

Kando na kategoria za maneno zinazounda virai, kunazo pia visehemu vya uchanganuzi vinavyopatikana katikati mwa maneno na virai. Hivi pia ni muhimu katika muundo wa sentensi katika kila lugha.


**Mfano 4.1 .1**

Paka anakula panya

| | |

mtendaji kitenzi kitendewa

Mchoro matawi wa sentensi hii utakuwa:




**Mfano 4.1.2**

Panda kitandani

Katika sentensi hii 4.1.2 mtendaji ni nafsi ya pili katika umoja (*wewe*) ingawa haionyeshwi. Mtendaji awe ameelezewa au anaeleweka ndiye hubainisha kiambishi awali kitakachoambatanishwa na kitenzi.

Sentensi huwa na maana iliyo wazi. Maana hii iliyo wazi hutegemea kabisa maana za maneno yaliyounda sentensi hiyo (maana za mofimu) na pia sheria za kisintaksia zilizofuatwa. Sentensi inaweza kuwa na maana wazi zaidi ya moja (yenye utata) au maana hizo wazi zinaweza kuwa na kasoro au zisizofasirika (Searle, 1979).

Katika kutamka sentensi, mzungumzaji anaweza kutoa maana ambayo ina maana tofauti na maana za sentensi, kwa mfano, katika sitiari, au anaweza pia kumaanisha kinyume cha sentensi, kama katika kejeli au zaidi pia anaweza kuwa na maana zaidi ya maana katika hiyo sentensi, kama katika usemi tendaji usio moja kwa moja.

### 4.1.3 Dhana ya Virai

Kirai ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina muundo wa kiimakiarifu. Muundo wa kiimakiarifu ni ule ambao unahusisha mtendaji wa tendo linalotendwa na ambao ndio muundo wa msingi wa sentensi katika lugha yoyote ile (Massamba na wengine 1999; Russell, 1986; Wallwork, 1985). Uundaji wa virai umekitwa katika aina za maneno. Hivyo aina hizo za maneno ndizo zitatumika kama msingi wa kuainisha virai. Virai mbalimbali vinapounganishwa huunda sentensi.

**Mfano 4.1.3.1**

| | | | |
|---|---|---|---|
| ***Kirai 1*** | ***kirai 2*** | ***kirai 3*** | ***kiari 4*** |
| 1. Mtu mkubwa | amepika chakula | kwa kaka | upesi sana. |

| | | |
|---|---|---|
| ***Kirai 1*** | ***kirai 2*** | ***kirai 3*** |
| 2. Mtu yule mkubwa | amempikia Juma chakula | kwa uangalifu mkubwa na |

***kirai 4***
upesi kuliko ilivyotarajiwa.

### 4.1.4 Aina za Virai

Kama tulivyosema hapo awali, miundo ya virai hukitwa katika aina za maneno ambazo ndizo chimbuko la mahusiano maalumu ndani ya vipashio hivyo.

Kiswahili kina aina nane (8) za virai lakini hapa tutataja aina tano za virai ambavyo vinahusishwa na utafiti wetu na kutolea aina hizi mifano ya sentensi.

1. Virai – Nomino
    - *Mtoto* anaimba
    - *Nyumba* zenye kuta ndefu zitajengwa upya.
2. Virai-Vitenzi
    - Mwalimu *alimkataza mwanafunzi kuingia.*
    - Dereva *amesema kwamba atarudi kesho.*
3. Virai-Vivumishi
    - Mtu *mwenye kufanya fujo* amekamatwa.
    - Msichana mwenye nywele *nzuri ya kutamanika.*
4. Virai-Vielezi
    - *Huyu mtoto hulia sana sana* akiwa mgonjwa.
    - Ali na Juma walitembelea *Saku kwa Bako.*
5. Virai-Viunganishi.
    - Mzee *atasafiri kwa pikipiki.*
    - Ali *ameenda kwa baba yake.*

Katika kuchunguza usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika katika kiwango cha sintaksia, tunajaribu kulinganisha muundo wa sentensi ya Kiswahili sanifu ambao tayari umefafanuliwa na muundo wa sentensi katika Kiswahili kinachotumiwa na Waasia ili kuonyesha jinsi miundo hii inavyoingiliana. Maelezo ya muundo wa launi ya Kiswahili ya Waasia unaelezewa katika sehemu inayofuata.

## 4.2 MUUNDO WA SENTENSI KATIKA LAUNI YA KISWAHILI YA WAASIA

Kama tulivyotanguliza kusema, Waasia hutumia Kiswahili ambacho ni tofauti kwa kiasi na Kiswahili sanifu. Tofauti hizi hujitokeza katika viwango vya fonolojia, leksia, semantiki na sintaksia. Katika sura hii tutachunguza tofauti hizi katika kiwango cha Sintaksia.

Katika launi ya Kiswahili ya Waasia, sentensi huwa na ruwaza ya virai ambayo ni tofauti na muundo wa sentensi katika lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa wanasarufi Miundo Virai (tazama sura ya pili) sentensi katika lugha yoyote ile huwa na kirai nomino na kirai kitenzi

$$S \longrightarrow KN + KT.$$

Lakini launi ya Waasia huwa na muundo wa sentensi ulio na kirai nomino na kirai kitenzi na kirai nomino cha pili ambacho si cha lazima ( Neale, 1974)

$$S \longrightarrow KN + KT\ (+ KN)$$


**Mfano 4.2.1**

Muundo wa sentensi katika launi hii ya Waasia utakuwa tofauti na muundo katika Kiswahili sanifu.

Tazama sentensi ifuatayo iliyochanganuliwa kwa kutumia mchoro matawi:

Mutoto nakwenda malangoni veve naambia mimi

S ⟶ KN + KT (+KN)





Sentensi katika launi hii ya Kiswahili huwa na vielezi nyongeza; '*kama*' na '*huko*'.


'*Kama*' huwekwa mwanzoni mwa sentensi na '*huko*' hutokea mwishoni mwa sentensi.

**Mfano 4.2.2**


1. Kama nataka nguo mzuri leta mia tano.




2. Kama namaliza chakula kimbia.




3. Fasuh nakwisha tembea huko.



4. Mimi nakwenda huko




Mageuzi ya sentensi ambayo ni jambo la kawaida katika lugha ya Kiswahili haidhihiriki kuwepo katika launi hii. Mifanyiko hii ni pamoja na kauli tendwa, urejeshi na upatanishi wa kisarufi.

Sifa nyingine muhimu kuhusiana na muundo wa sentensi katika launi ya Kiswahili ya Waasia ni ugeuzajimaumbo kanushi. Hii hubainika kwa kuongezea neno '*hapana*' katikati mwa KN na KT katika Sentensi:

S ⟶ KN + hapana + KT (+ KN).

**Mfano 4.2.3**


Veve (hapana) lete chakula mimi kwishaenda

Katika launi ya Kiswahili ya Waasia, mara nyingi sentensi huanzia kwa maneno kama vielezi, vikanushi , vionyeshi na viunganishi.

**Mfano 4.2.4**


1. Kionyeshi

   Hii peleka huko





2. Kikanushi

   Hapana zungumza wakati mwingi.



3. Kielezi

Msuri sana hio nguo, letea mimi aone.




### 4.3 USAWAZISHAJI WA USEMI KATIKA KIWANGO CHA SINTAKSIA

Kulingana na maelezo ya sehemu ya awali kuhusu muundo wa sentensi katika Kiswahili sanifu na launi ya Kiswahili ya Waasia, tukizingatia misingi ya Sarufi Miundo Virai, ni bayana kwamba muundo wa Kiswahili kinachotumiwa na Waasia ni tofauti na Kiswahili sanifu. Lakini hata hali ikiwa hivyo (tofauti za kimuundo wa sentensi zikiwemo) Waasia na Waafrika wameweza kuingiliana na kuwasiliana bila shida. Hii hali imewezekana kwa sababu wazungumzaji hawa huweza kubadilisha mtindo wa uneni kadri iwezekanavyo na kufikia maafikiano.

Ubadilishaji tunaozungumzia hapa unahusu utumiaji wa sentensi katika mazungumzo ambazo zina muundo fulani ili kufikia malengo fulani. Basi usawazishaji wa usemi wa kisintaksia ni hali ya maingiliano ambapo mzungumzaji anatumia sentensi zenye muundo sawa na muundo wa sentensi katika lugha ya msikilizaji. Kunaweza kuwa na mwingiano na ujitengaji kiusemi kuhusiana na miundo ya sentensi zinazotolewa na wazungumzaji katika mazungumzo. Ikiwa mzungumzaji atatumia sentensi zenye muundo wa sentensi sawa na lugha ya msikilizaji atachukuliwa kuwa amechukua hatua ya mwingiano (Giles na wengine, 1979; Simpson, 1991). Kinyume cha hali hii huwepo (ujitengaji kiusemi) pale ambapo msikilizaji anatumia sentensi zenye muundo wa sentensi tofauti na muundo wa sentensi katika lugha ya msikilizaji. Ujitengaji huu unaitwa ujitengaji kiusemi wa kisintaksia (Trudgill, 1986).

Mwingiano na ujitengaji kiusemi katika kiwango cha sintaksia ni jambo ambalo liliweza kujitokeza katika maingiliano baina ya Waasia na Waafrika jijini Nairobi.

Mazungumzo yanayofuata yanafafanua mifano ya usawazishaji wa usemi wa kisintaksia baina ya Waasia na Waafrika .Data inayoonyesha mwingiano na ujitengaji wa kisintaksia itachanganuliwa kwa misingi ya nadharia za Usawazishaji Usemi, Upekee na Sarufi Miundo Virai. Mifano ya mazungumzo imepangwa katika sehemu nne:

**SEHEMU A**

Sehemu hii inahusu mazungumzo ambapo Waasia wanaonyesha mwingiano kwa Waafrika katika kiwango cha sintaksia. Mwingiano hapa unajitokeza pale ambapo Waasia wanatumia muundo wa sentensi sawa na Waafrika.

**Mfano 4.3.1**

Mazungumzo yafuatayo ni baina ya Mwasia (AS) kijana na Waafrika wawili (AF1) na (AF2) vijana. AF1 ni mfanyikazi na AF2 ni mnunuzi. Kulingana na kanuni isiyo ya Kipekee ya uchaguzi ya nadharia ya Upekee, uchaguzi wa lugha unaotarajiwa hutumiwa iwapo wasikilizaji, mada na mahali pa mazungumzo zinabainishwa na wazungumzaji. Mazungumzo haya yanaambatana na kanuni hii kwa sababu yanahusu wazungumzaji wanaokaribiana kiumri. Mtindo wao wa uneni unaelekea kuwa sawa, hata kuna matumishi ya 'Sheng' na muundo wa sentensi ni sawa. Wote wanajisawazisha mmoja kwa mwingine. Sentensi zingine zinaanza kwa kielezi. Pia wanajisawazisha kiusemi kama njia ya kuelewana kibiashara na ikiwezekana kila mmoja apate manufaa na kuepuka gharama.

AF1 – Unajua ile imenikasirisha ni kwa sababu hataki nisikiza.

AS – Watu wengi huwa ipo. Sijali

(kwa AF2)

sema, uziwa.

AF2 – **Hii '*nut*' tausia mimi ngapi?**

AS – **Hii tausia wewe mia nane hamsini.**

AF2 – Nitatoa mia nne

AS – Hata *second hand* haiwezi. Unataka kutoa ngapi?

AF2 – Nataka toa hio nimesema

AS – Una supuu na hana doo?

AF2- Supuu hana doo.

**Mfano 4.3.2**

Mazungumzo haya yanamhusu Mwasia (AS) mwanamke wa umri wa makamo na Mwafrika (AF) mwanamme mfanyakazi wa umri wa makamo. Katika mazungumzo haya, hali ya juu ya mwingiano inajitokeza. Mwasia mwanamke anatumia muundo wa lugha sawa na Mwafrika. Pia ana urejeshaji katika muundo wa sentensi. Mwafrika naye anatumia mtindo huo huo. Huu ni uchaguzi wa uneni usiotarajiwa kulingana na kanuni ya Kipekee ya uchaguzi. Mwajiri na mwajiriwa hawatarajiwi kuingiliana kirafiki hivyo. Hata hivyo kutegemea yale wanayolenga, wanaweka kando makisio ya awali waliyo nayo kuhusu kaida za kijamii na kuuangalia uhusiano wao vingine. Hii ni kwa sababu wamepima gharama na manufaa wanazotarajia. AS angetaka usaidizi kutoka kwa AF (kuhusu jambo lililotendeka awali) naye AF anafurahia kumpendeza mwajiri wake ili kudumisha kazi na faida zingine zitokanazo na uhusiano wa kikazi kama vile nyongeza ya mshahara, uhusiano mwema na cheo. Hii inamfanya atumie muundo wa sentensi sawa na AS.

AS- Mumo kuya hapa. Mimi naita wewe. Ile mpango yetu namna gani?

AF- Mimi niliambia wewe kwamba lazima uende kwa polisi.

AS- Ulimuliza rafiki yako

AF- Nani huyo?

**Yule ambaye alikuja hapa jana**?

AS- Ndio. **Yule ambaye mimi nilituma wewe kwake**.

Ulinambia anaitwa?

AF- Musembi. Hiyo ndio jina yake.

Kulingana na Akhamanova na Mikael'an (1969), sentensi inaweza kuwa haina maana lakini iwe ni sahihi kisarufi. Mara nyingi Waasia hutumia sentensi ambazo kimuundo si sanifu ingawa zina maana. Hizi sentensi huleta utata katika kufasiri maana yake. Kuzielewa kunategemea muktadha wa matumizi.

**Mfano 4.3.3**

Mazungumzo yafuatayo yanahusu Mwasia (AS) mwanamme na Mwafika (AF) mwanamme wote wa umri wa makamo. Mwafrika ananunua viatu katika duka la Mwasia la kuuzia viatu. Wazungumzaji hawa wana ubahatishi mwingi. Wanafanya hivi kwa kuchanganya lugha tatu- Kiswahili, Kiingereza na Kikamba katika mazungumzo yao. Hii ni kwa sababu wanataka kufikia malengo fulani lakini hawana uhakika na lugha itakayo wasaidia kufikia malengo hayo ya kijamii. Hata hivyo wanaonyesha mwingiano kwa kila lugha inayochaguliwa kwa vile AS anataka kuuza zaidi na AF anataka kununua viatu kwa bei nafuu. Mwingiano huu ni wa juu na pia chini.

| | | |
|---|---|---|
| AS | - | *Customer* karibu, welcome! |
| | | Ingia ndani na uone viatu. |
| | | Aina yote iko. |
| AF | - | Ile **type** mpya ya **leather** |
| | | ambayo imetokea juzi iko? |
| AS | - | **Everything** iko, karibu uone. |
| | | Veve iko vaa saisi gani? |
| AF | - | Arobaini au arobaini na moja. |
| | | **I'm not sure.** |

AS - Mimi tampa veve uvae.

Vaa uone.

AF - Wacha nivae nione.

Mbona ni kubwa ! aaah

**Nĩ kĩnene** (kicheko)
(Ni kikubwa)

AS - (Kicheko) **nĩ kĩnene**?

(ni kikubwa?)
Tampa veve saisi **thirty nine**.

Sika.

AF - Nadhani hio itatosha, wacha nivae.

AS - Imetosea veve?

Sawa basi.

**Mfano 4.3.4**

Mazungumzo yafuatayo yanahusu Mwasia Daktari (AS) na Waafrika (AF1 na AF2) wateja katika kliniki. AS anaonyesha hali ya mwingiano kiusemi kwa AF1 na AF2 kama njia ya kwanza, kutaka kukubalika na pili, kuwavutia ili waweze kujieleza ipasavyo. Kujieleza kwa wazi kwa AF1 na AF2 kutamwezesha kuwasaidia (kuwatibu). AF2 anaongezea habari inavyotolewa na AF1 (katika sentensi5) kama njia ya kutilia nguvu yaliyosemwa na AF1 (katika sentensi 4) na hivyo kuonyesha umoja kati yao. AS anapotumia muundo wa sentensi sawa na AF1 na AF2 nao AF1 na AF2 kuonyesha umoja ni dhihirisho la uzingativu wa mhimili wa nadharia ya Usawazishaji Usemi ya kukadiria Gharama kati ya Wanajamii na mwingiano huu ni mwingiano - chini.

AS – Kaa kwa kiti.

Nani mgonjwa? (1)

AF1 – Ni mimi. (2)

AS – Nini iko shida? (3)

AF1 – Ninaumwa na kifua, tumbo na wakati mwingine macho. (4)

AF2 – **Shida hii ilianza siku kadhaa zilizopita.** (5)

AS – **Sida iko anza siku kadha** kama siku gapi? (6)

AF1 – Siku mingi .... Kama **mwaka sasa** (7)

AS – **Mwaka sasa**

(Kwa AF1)

Unatoa kamasi kama nakooa? (8)

AF1 – Ndio, na tena **kifua kinaniuma sana** nikikohoa. (9)

AS – **Kifua nauma sana**

kama nakooa? (10)

AF1 – Ndio.(11)

AS – enda juu ya kitanda

pale nyuma. (12)

**Mifano 4.3.5**

Mazungumzo yafuatayo yanahusu Waasia watatu (AS1,AS2 na AS3) na Mwafrika (AF) mteja katika duka la kuuzia vifaa vya nyumba.

Katika mazungumzo haya AS1, AS2 na AS3 wanatumia muundo wa sentensi sahihi katika lugha ya Kiswahili. Wanafanya hivyo kama njia ya kuwa sawa na AF na pengine

wamvute anunue sahani. Wanakwepa kutumia muundo wa sentensi katika launi ya Kiswahili ya Kiasia kama ilivyodaiwa awali. Wanafanya haya kuambatana na mihimili ya nadharia ya Usawazishaji Usemi ya Kufanana – Kuvutiana na Kukadiria Gharama kati ya Wanajamii. Hii ni kwa sababu wakipunguza tofauti za lugha kati yao na AF watafanana kiusemi na kuvutiana. Haya yatasababisha AF kuwakubali na kununua bidhaa kutoka duka lao. Huu ni uchaguzi wa lugha usiotarajiwa (wa kipekee).

AF – Nataka sahani aina ya ***skyland***

**zile zinatengenezwanga India.**

AS1 – ***Skyland*** **sinatengelezewa India.**

Iko, enda pande ile, taona.

AS2 – Kuja apa, sahani mingi, angalia.

AF - **Unauza moja moja ama wholesale?**

AS2 – Tausia sahani mzuri wewe iko *customer*.

AS1 – Tampa veve **moja moja na tena wholesale** ukitaka.

AF - Nataka kushika nione.

AS1 – Sika, mimi nampa veve, angalia.

taona sahani ya *quality*.

AF - **moja moja ni ngapi**

AS1 – **moja moja ni sabini**

AF - **moja moja ni sabini ?**

Hio ni juu sana.

AS3 – (kwa AS1)

Patia yeye na sitini

shauri yeye ni *customer* etu.

AF - ukiweka *fifty* mimi tunanunua

*dozen* mzima.

AS1 - Lete pesa mimi

namafungia veve.

**SEHEMU B**

Sehemu hii inahusu mazungumzo ambapo Waafrika wanaonyesha mwingiano kwa Waasia kwa kutumia muundo wa sentensi sawa na Waasia.

**Mfano 4.3.6**

Mazungumzo haya yanahusu Mwasia (AS) mwanamme mzee na Mwafrika (AF) mwanamke wa umri wa makamo. Mwafrika ni mteja wa Mwasia katika duka la kuuzia rangi. Mwafrika anajisawazisha kwa muundo wa sentensi wa Mwasia kama njia ya kutaka kufanana ndiposa weweze kujadiliana bei ya bidhaa na kuweza kuelewana. Wanapopunguza tofauti za lugha watakuwa sawa. Haya ni kuambatana na mhimili wa nadharia ya Usawazishaji Usemi- Kufanana-Kuvutiana. Kwa kufanya hivi Mwafrika ananuia kupata rangi kwa bei nafuu- anafanya haya kuambatana na mhimili wa nadharia ya Usawazishaji Usemi- Kukadiria Gharama kati ya Wanajamii.

AF – Habari bwana?

AS – Salama, sema, **veve iko taka nunua nini?**

AF – Hii rangi iko?

**Mimi iko taka nunua hii**. Huko nayo?

AS – **Hii mimi nitakuuzia veve mia saba,**

mbei musuri. Shika, angalia.

AF – **Hii mimi tampa wewe mia tano**

Fungia mimi kama unataka.

AS – *Customer,* **apana peleka mimi** nyumbani.

Veve nataka mimi hapa kesho?

AF – Musee, **Mimi hapana taka wewe** uende nyumbani,

lakini niko na mia tano tu;

niuzie rangi musee.

AS – Mimi tapunguzia veve, shauri veve ni *customer*,

kama naweza, mia moja. Nimpe mimi mia sita.

AF – Fungia mimi kwa karatasi basi.

**Mfano 4.3.7**

Mazungumzo yafuatayo ni baina ya Mwafrika kijana mfanyikazi (AF) na Waasia wanawake wa umri wa makamo (AS1 na AS2) ambao wananunua nguo za watoto katika duka la Mwasia la kuuzia nguo za watoto. AS1 na AS2 wanachagua lugha kuambatana na kanuni Bahatishi ya uchaguzi wa lugha ya Kiingereza (*Ibleu (blue), qualitei (quality)* ni kubahatisha kwa sababu hawana uhakika na lugha itakayowasaidia kufikia malengo yao( kupata nguo nzuri kwa bei nafuu). AF naye anatumia muundo wa sentensi wa AS1 na AS2 kwa sababu ni jambo linalotarajiwa kwa muuzaji kujaribu kuwapendeza wateja (kanuni isiyo ya Kipekee ya uchaguzi). AF pia anaonyesha mwingiano kwa sababu angependa kuuza zaidi.

AF- Semeni niwauzie.

AS1- **Kama inataka nguo *Ibleu* itapata**?

AS2-(Kwa ASI) Inataka Ibleu au ni madoadoa?

AS1- Hizo vitu ndongodogo naenda pamoja.

AF- **Kama unataka hii nguo-ni blanketi ya blue nitakuuzia**.

AS2- Leta, inataka kuangalia *qualitei* msuri.

AS1- **Veve hapana mpa mimi ile watu kwisha sikasika,**

**nampe mimi mpya.**

AS2- Msuri sana hii nguo

Sasa tengeza bei

AF- Mzuri, mzuri hata wewe kwisha ona, ee!

AS2- **Tampa mimi na gapi?**

AF- Pesa kidogo sana, naona nguo mzuri , pesa kidogo.

Leta alufu mbili.

AS1- Kayana yangu tengeneza mimi bei

AF- **Utanipa mimi pesa ngapi?**

AS1- sika hii alfu moja na mia tano.

**Mfano 4.3.8**

Mazungumzo yanahusu Mwasia (AS) mzee mwenye duka la kuuzia nguo za watoto na Mwafrika (AF) mfanyikazi. Kulingana na Sheria ya Ushirikiano, kanuni za Kiasi na Udhahiri zinasisitiza utoaji wa habari isiyozidi au kupungua na isiyo na utata, ambayo ni fupi na yenye mpangilio maalumu. Mazungumzo haya yanaonekana yakienda kinyume na sheria hizi. Sehemu ya mazungumzo hayo iliyowekwa kwa maandishi mazito ina utata

katika kuelewa maana. Mwafrika na Mwasia wanatumia mtindo wa uneni ulio sawa (yaani kuhusiana na upangaji wa maneno katika sentensi ambayo yana utata) na wanaelewana. Lengo la ubadilishanaji huu ni kutaka kuwasiliana na kuelewana pale ambapo jinsi wanavyoongea mradi wanaelewana. Kutaka kujieleza na kueleweka kunawafanya waonyeshe mwingiano kama njia ya kila mmoja kufikia lengo lake.

AS. - **Kama nataka fanya kazi nataka pesa,**

**basi nataka** kutoa mkono.

AF. – Mimi kwisha mwambia wewe iko ongezea

mimi siku chache kisha niende ruhusa

AS. – **Kama nataka kaa chini na bibi yako**

**basi apana pesa.**

AF. – Wewe mzee, **kama hapana patia mimi**

**ruhusa hapana fikiria** mimi nitafanya

kazi yako. Kazi nyingi hapana pumzika.

**Kama nataka mimi iko fanya kazi tampa mimi**

**ruhusa tampa mimi pesa. Tena nafanya kazi** .

Kwa kutilia mkazo wazo kuhusiana na utata katika kufasiri maana katika sentensi, Simpson (1991) anasema kuwa miktadha ya sentensi huathiri uelewaji wa maneno katika sentensi. Katika kuelewa sentensi, watu hutumia habari inayotolewa na maneno katika sentensi kufasiri maana. Hata hivyo, wakati mwingine hali haiwi hivi, kwani kwa kawaida watu watachukua maana wazi ya sentensi (Wierzbicka, 1996).

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Aidha maana ya neno linalotangulia katika sentensi (Muuguzi) na ambalo linahusiana na linalofuata (daktari) husaidia kuelewa neno la pili (daktari) (Simpson, 1991). Kwa hivyo muktadha na mahusiano ya maneno ni jambo ambalo limezingatiwa na Waasia na Waafrika katika matumizi ya Kiswahili kuhusiana na utungaji wa sentensi.

**Mfano 4.3 .9**

Mazungumzo yafuatayo ni sehemu ya mazungumzo kati ya Mwasia (AS) mzee mwenye kiduka cha kuuzia vifaa vya nyumba na Mwafrika (AF) kijana mfanyikazi. AF anaonyesha mwingiano wa juu kwa sababu analenga kumpendeza AS (mwajiri). Na AS anajisawazisha kwa AF kwa vile angetaka kuuza zaidi kupitia usaidizi wa AF. Wanapima gharama na manufaa yanayotarajiwa na papo kuchagua namna ya uneni.

AS. – Alikuwa anaita nini yeye? (1)

AF. – Anaitangwa majina mingi yeye. (2)

AS. – **Mambie yeye vitu mingi siku hizi iko** (3)

AF. – Kama unataka mimi **namwambie yeye**
**vitu mingi siku hizi iko** kama masufuria, ikombe,
tamble maat na hata masaani . (4)

AS. – **Fanya hivi, kimbia wewe mite yeye saa hii**
**mimi iko taka yeye saa hii**. (5).

AF. – **Muzee, hapana jali mimi iko kimbia saa hii**
**namshika na kumleta yeye shauri**
**wewe iko taka yeye** (6)

Katika mazungumzo haya (mfano 4.3.9) kueleweka kwa baadhi ya maneno kunategemea uhusiano wa maneno yanayokaribiana (upanganaji wa maneno katika sentensi). Kwa mfano ili kuelewa sentensi (1) italazimu uoanishe maneno yaliyotumiwa. Neno '*anaita*' inatoa maana tofauti na ile mzungumzaji alikusudia lakini kusudi la mzungumzaji linaeleweka kwa kuzingatia neno linalofuata, yaani '*nini*' yaani, mzungumzaji alikusudia kusema '*anaitwaje*'. Vilevile sentensi (2) inafafanua zaidi sentensi (1) .

Hali kadhalika, muktadha unasaidia pia kuelewa mada ya mazungumzo, kwa sababu ni baada ya kuelewa maneno katika mazungumzo utakavyofahamu jambo linalozungumziwa (Scherer na Giles, 1979; Searle, 1979).

**Mfano 4.3.10**

Mazungumzo yafuatayo yanahusu Waasia wawili (AS1,AS2) mwanamme na mwanamke katika duka la kuuzia vyuma na Mwafrika (AF) msaidizi wao. Mwafrika anajisawazisha kiusemi kwa Waasia kwa kutumia muundo wa sentensi katika launi ya Kiswahili ya Waasia. Analenga kuwapendeza waajiri wake ili apate manufaa kama nyongeza ya mshahara na vile vile kudumisha kazi. Mwingiano anaoonyesha ni mwingiano – juu.

AF - Mzee, kasi iko kwisha.
Nataka kwenda pande ingine
ya *store* kufanya uko.

AS1 - Kama veve namaliza enda
endelea pande ingine ya *store*.

AS2 - Kayana, kuya. Apana enda *store* .

Angalia *customer* iko nakuja.

AF - *Customer* sema.

Nikuuzie nini?

AS2 - Ongea musuri na io mutu.

Iko nunua apa siku mingi.

Tengelezea yeye bei musuri.

**SEHEMU C**

Katika sehemu hii mifano ya mazungumzo inadhihirisha ujitengaji wa Waasia kwa Waafrika katika kiwango cha sintaksia wanapotumia lugha zao za kwanza ilhali wasikilizaji ni Waafrika. Wanafanya hivyo kwa kutumia muundo wa sentensi ambao ni tofauti na muundo wa sentensi katika Kiswahili sanifu.

**Mfano 4.3.11**

Mazungumzo yanahusu kijana Mwafrika (AF) mfanyikazi katika duka la Waasia wawili (AS1 na AS2) la kuuzia nguo. Waasia wanamtenga Mwafrika kiusemi kwa kutumia lugha ya Kigujarati.

AS1 na AS2 wanajitenga kiusemi kwa AF wakati wanapotumia lugha ya Kigujarati ambayo muundo wake wa sentensi unatofautiana na muundo wa sentensi katika lugha ya Kiswahili. Wanapobadilisha lugha kutoka Kiswahili (matumizi ya Kiswahili ni uchaguzi wa lugha unaotajariwa – usio wa kipekee) wanaonyesha uchaguzi wa lugha wa kipekee (usiotarajiwa). Uchaguzi huu wa lugha unasababisha ujitengaji kiusemi ambao unalenga kujitambulisha kijamii wanapojadiliana mambo pasipokumhusisha AF.

AF - Mzee, nimemaliza kazi

pande ile. Nimepanga nguo huko juu.

AS1 - Na fagio iko maliza kutoa huko ndani?

AF - Ndio.

AS1 - Basi kaa pale nangoja *customer*.

AS2 - (Kwa AS1)

**AA manas saro chhe**

(huyu mtu ni mzuri)

AS1 - **Apne Pagar Vadhari daye**?

(tunaweza kumwongezea mshahara?)

AS2 – **Kefla noo**

(ngapi iwe?)

Kiswahili sanifu – Iwe ngapi?

$AS_1$ - (Kwa AF)

Kuya usimame hapa.

Mimi iko ingia pale

tena narudi

(Kwa AS2)

**Khavano samaye**

(Wakati wa kula ni)

Kiswahilisanifu - Ni wakati wa kula.

**Mfano 4.3.12**

Mazungumzo haya yanahusu Mwasia (AS1) mwenye duka la kuuzia nguo, Mwasia mteja (AS2) na Mwafrika (AF) mfanya kazi. Waasia wanamtenga Mwafrika kiusemi pale ambapo AS1 anaongea kwa AS2 kwa Kihindi naye AS2 anajibu kwa kuchanganya Kigujarati na Kihindi.

Kulingana na Scotton ( 1993) uchaguzi wowote wa lugha zaidi ni majadiliano ya ubainifu wa mambo ( sifa) zinazozingira mawasiliano fulani. Nadharia ya Upekee inachukua uchaguzi wa lugha kama majadiliano ya jozi ya haki na majukumu. Ni kuambatana na madai haya AS1 anabadilisha lugha kutoka Kiswahili hadi Kigujarati na Kihindi ili kuwasiliana na AS2. Jambo hili linafanyika kufidia mahitaji ya $AS_2$ ambaye awali hakuhusika katika mazungumzo. Kwa kutumia lugha za Kigujarati na Kihindi wanamtenga AF kiusemi na pia wanajitambulisha kijamii.

AF – Iko Mhindi hapa nje anaita wewe.

AS1 – Nani?

AF - Anakuita, simjui.

( $AS_1$ anatoka nje ya duka na kumzungumzia $AS_2$)

AS1 – **Nikal udharse** (Kihindi)

(Ondoka pale)

AS2 – **chal avigia.**

(Kigujarati) (Kihindi)

(Nitaingia)

Kiswahili sanifu – nitaingia ndani

AS1 – **Nai chal avigia**

(Kigunjarati) (Kihindi) (Kigunjarati)

(Ndani usiingie.)

Kiswahili sanifu – usiingie ndani.

AS2 – **Bhok lagi he.** ( Kihindi)

(Nina njaa)

AS1 - (kwa AF)

Punga malango dogo ya kazi

AF – Tayari imefungwa.

**Mfano 4.3.13**

Haya ni maingiliano baina ya Waasia wawili (mume $AS_1$ na mke $AS_2$) na Waafrika wawili wafanyakazi (AF1 na AF2) katika kibanda cha maonyesho ya vyakula vya asili ya Bara Hindi. AS1 na AS2 wanawatenga Waafrika wanapotumia lugha ya Kihindi Waafrika wakiwa wasikilizaji. Mazungumzo haya yanadhihirisha uchaguzi wa lugha usiotarajiwa (wa kipekee) AS1 na AS2 wanapotumia lugha za Kigujarati na Kihindi wanaonyesha ujitengaji kiusemi kwa AF na mwingiano kati yao. Ujitengaji unafanywa baada ya haja ya kutaka kushughulikia mambo ya kinyumbani na ambayo hayamhusu AF.

AS1. (Kwa AF)

Panga doo ile masuri.

Apana acha kile kitu peke yake

AF- Ndoo gani?

AS1 - Ile ya lagi ya *ibleu*

AF - Ile kwisha maliza chakula.

Nataka kwenda kuongezea chakula kule *store.*

AS2. (Kwa $AS_1$)

**Agaye balko**

Wamerudi watoto

Kiswahili sanifu - watoto wamerudi.

AS1 - **Kitne baja he?**

Na saa ngapi?

AS2 - **Khara no samaye**

Ni saa za kula

$AS_1$ – **Te modo aviyo**

(wamechelewa)

AS2 - **Yo tene?**

(Unaona sasa)?

Kiswahili sanifu- Sasa unaona?

**Mfano 4.3.14**

Mazungumzo yafuatayo yanahusu Waafrika wawili ($AS_1$ na $AF_2$) wazee wafanyakazi katika kibanda cha kushonea sare na Waasia watatu wenye kibanda ($AS_1$, $AS_2$ na $AS_3$) Waasia wanajitenga kiusemi kwa Waafrika wanapoongea Kiasia pamoja na Kiingereza wakati Waafrika wanasikiliza.

Matumizi ya lugha ya Kiingereza ni jambo lisilotarajiwa katika uhusiano katika mazungumzo haya. Hata hivyo uchaguzi wa aina hiyo unawafanya Waasia $AS_1$ na $AS_2$ kujitenga kiusemi kwa AF. Kama waajiri wanataka kusuluhisha shida zao pasipo kumhusisha AF (mwajiriwa).

| | |
|---|---|
| AF – | Uzi umeisha pande hii. |
| | Niletee rangi nyeupe. |
| AS1 | ( Kwa $AS_2$) |
| | **Do we have colour white in the store**? |
| | Sisi tuna rangi nyeupe ghalani? |
| | Kiswahili sanifu – Tuna rangi nyeupe huko ghalani? |
| AS2 - | **I don't know but call Patel to confirm** |
| | (Mimi sijui lakini mwite patel uhakikishe) |
| | Kiswahili sanifu - sijui lakini mwite Patel uhakikishe |
| AS1. | ( Kwa $AS_3$) |
| | Patel, kuja |
| | **Chhoo kenu**? |
| | (Yako habari?) |
| | Kiswahili sanifu – Habari yako? |
| AS3 - | **chhe saroo** |
| | (Yangu habari salama) |
| | Kiswahili sanifu - Salama |
| AS1 – | Uzi rangi nyeupe iko? |

AS3 – **Noo khana?**

( ngapi unataka?)

Kiswahili sanifu - Unataka ngapi?

AS1 – lete mbili

( kwa AF)

Patel tempa veve uzi

AF- Ni sawa

**Mfano 4.3.15**

Haya maingiliano ni baina ya Waasia ( $AS_1$ na $AS_2$) wenye kibanda ambapo vyuma huchomelewa na Mwafrika ( AF) mfanyakazi. Waasia wanamtenga kiusemi kwa kutumia lugha yao ya kwanza ( Kigunjarati).

Ujitengaji katika mazungumso haya ni uchaguzi wa lugha unaotarajiwa ( usio wa kipekee). Inatarajiwa kuwa iwapo mwajiri anaongea mambo kinyume na matarajio ya mwajiriwa asimhusishe mwajiriwa. Kwa kujitenga kiusemi kwa AF, $AS_1$ na $AS_2$ wanakubaliana kuboresha biashara yao kwa kumuondoa AF kazini kwa sababu hafanyi kazi inavyotarajiwa. Ujitengaji unawafaidi $AS_1$ na $AS_2$ lakini ni hasara kwa AF.

AS1 – Veve, bona unatembea bolebole.

Arakisa, kazi iko nachelewa.

AF – Hii chuma hapana iko chomeka.

Nachoma tena inakatika.

AS1 – veve apana jua kuchoma?

Shika chuma namna hii

alafu veve iko choma apa

(akimwonyesha).

AS2 - ( Kwa $AS_1$)

**Fe manas adsu chhe.**

( Mtu mzenbe huyu ni)

Kiswahili sanifu – Huyu mtu ni mzembe

AS1 – **Ane kadhi nak**

(Mimi tafukuza yeye.)

Kiswahili sanifu – Nitamfukuza

(Kwa AF)

Nampa veve saa ya leo

Kama apana fanya kazi mimi

Iko ondoa veve ava.

AF- Wewe unapenda kunipigia

kelele – huoni ninafanya kazi

haraka. Hapana fikiria mimi

ni mashine. Ninatumia damu.

## SEHEMU D

Sehemu hii inabainisha ujitengaji wa Waafrika kwa Waasia wakati wanapotumia lugha zao za kwanza wakati wasikilizaji ni Waasia..

**Mfano 4.3.16**

Mazungumzo yafuatayo yanahusu Mwasia (AS) mzee mwenye duka la kuuzia nguo, Mwafrika (AF1) msichana mfanyikazi na Mwafrika (AF2) mwanamke wa umri wa makamo mteja. AF1 na AF2 ni Wakamba na ni marafiki. Wanajitenga kiusemi kwa AS kwa kutumia lugha ya Kikamba. Wanafanya hivi kwa sababu AF2 angetaka AF1 amsaidie kujadiliana bei ili apate maua kwa pesa kidogo. Hangepeda Mwasia aelewe haya. Ujitengaji huu ni namna ya ukadiriaji wa mahitaji ya kijamii.

AF1 - **Sasa, karibu, nĩwavika**?

( … … umefika)

AF2 - **Yĩĩ nĩnavika. Umũnthĩ**

**nĩenda ũndetheesye. Ndikwenda**

**Mũindi ũyũ ambinyĩĩye. Neena**

**nake atheesye thooa vyũ vatonyeka**

**ta nĩ *customer* wenyu.**

(Ndio nimefika. Leo nataka unisaindie.

Sitaki huyu Muhindi anifinyilie. Ongea na

yeye apunguze bei kabisa kama inavyowezekana

kwa sababu mimi ni *customer* wenu).

AF1 - **Wamũsyĩ ndũkamake**.

(Wa nyumbani usijali)

Sema kile unataka

AF2 - Nataka maua ya alusi.

Tena mengi sana.

AS - Nduku, usia *customer*

musuri. Iko sida?

AF1 - Hapana, lakini yeye

iko taka kununua

maua mingi. Yeye ni

*customer* wa zamani wetu.

AS - Apana baya. Tengelezea

yeye maua. Bei taongea;

apana kosana na *customer* etu.

AF2 - **Wamũsyi ndikwenda kũneena na**

**Mũindi, niwe ũũmũtavya.**

(wa nyumbani sitaki kuongea na Mhindi,

ni wewe utamwambia)

AF1 - **Maundu ni sawa wamusyi.**

(mambo ni sawa wa nyumbani)

**Mfano 4.3.17**

Mazungumzo haya ni mfano wa ujitengaji wa kiusemi baina ya Waasia na Waafrika. Mazungumzo yanahusu vijana wawili wa Kiafrika wanaozungumza lugha ya Kikuyu na mmoja anafanya kazi katika duka la Mwasia (AS) mzee ya kuuzia vyuma na yule mwingine ni mteja. Vijana hawa wanajitenga kiusemi kwa sababu wana nia ya kumwibia

Mwasia. Kando na ujitengaji, habari anazotoa AF1 haziambatani na kanuni ya Ukweli ya mazungumzo - anadanganya Mwasia.

AS - Veve apana kaa mbali na *customer*.

Kuja ongea na *customer*.

AF1 - *Customer* sema. Unataka nini?

AF2 - **Nindoka, hee mari**

(Nimekuja. Lete mali)

AF1 - **Kaiwoka na ihenya atia?**

(Umekuja haraka aje?)

AF2 - **Nindona handũ ha kũhitha, rehe**

(Nimeona mahali pa kuficha, lete).

AS - *Customer* iko taka nini?

AF1 - Mimi ninamwelezea bei ya *brakes*.

Anasema apunguziwe bei- yaani iwe alfu…

**Mfano 4.3.18**

Haya ni malalamiko juu ya wachuuzi wanaouza bidhaa kando kando ya barabara.

Mwasia (AS) mwenye duka anawalalamikia vijana Waafrika wafanyikazi wake kuhusiana na jambo hili. Waafrika kwa muda wamuunga mkono Mwasia lakini baadaye wanamtenga kiusemi wakati wanapoanza kuzungumza kwa lugha ya Kikamba.

Kijana mmoja ni mlinzi wa duka ( AF1) na yule mwingine (AF2) anasaidia kazi ya duka. AS anatafuta kuwahusisha AF1 na AF2 ili watazame shida hii kama anavyoiona. Wanamuunga mkono kwa kuanza kulalamikia wachuuzi lakini baadaye wanamgeuka na

kuanza kumdhihaki kwa kutumia lugha ya Kikamba. Kwa kumtenga AS, AF1 na AF2 wanaonyesha mwingiano na ujitambulishi Kijamii. Awali katika mazungumzo $AF_1$ na AF2 wanajisawazisha kiusemi kwa AS kama njia ya kumpendeza mwajiri wao lakini wanapogundua kwamba AS hawaheshimu Waafrika wenzao (wachuuzi) AF1 na AF2 wanajitenga kwa AS ili kuwatetea Waafrika wenzao. Ujitengaji unafanywa baada ya kupima gharama na faida inayotarajiwa.

AS – Askari ondoa hii mutu
kwa mlango. *Customer*
apana nafasi ya kuingia.

AF1 – Hawa watu wanawezwa tu
na *city council.* Lakini
City Council haitaki
kuwafukuza.

AF2 – Kweli kabisa – kila siku
redio inataganza hawa watu
wataondolewa lakini
wanaendelea kuishi hapa.

AS – Ii mtu iko aribu biashara
ya Mhindi. Saa ngapi mimi
tauza na *customer*
apana nafasi ya kuingia.
Hii mtu iko fungia
*customer* njia.

AF1 – Mungu tu ndiye atasaidia
sisi *boss*.

AS – Mungu! Mungu! kila kitu
Mungu! Ondoa yeye mara
moja kwa malango.

AF1 – (kwa $AF_2$)

**Andũ aa monaa kĩla kĩndu ko kyoo.**

(Watu hawa wanaona kila kitu ni chao.)

**Nũndũ nthĩ yonthe nĩyoo mũndũ ũngĩ**

(Kwani dunia yote ni yao mtu mwingine)

**ndeka ũndũ wake Ilovi yĩĩ.**

(hafanyi jambo lake Nairobi hii.)

Kiswahili sanifu -Hawa watu wanaona kila kitu ni chao kwani dunia yote ni yao?

Hakuna mtu mwingine atafanyia kazi yake hapa Nairobi?

AF2 – **Mũndũ mwiũ nde kyake kũũ mwa**!

(mtu mweusi hana chake huku!)

**Mfano 4.3.19**

Mazungumzo yafuatayo yanahusu vijana wawili (AF1 na AF2) Wajaluo na Mwasia (AS) mwenye duka la kuuzia vitabu. Kijana mmoja ni mfanyikazi ($AF_1$) na yule mwingine ni rafiki yake (AF2). $AF_2$ ana ripoti ya $AF_1$ kutoka nyumbani na hangetaka AS asikie kwa

hivyo anaingia dukani kama mnunuzi na kutumia lugha ya Kiswahili kwa $AF_1$ na AS. Baadaye anatenga AS kiusemi wakati anaposemesha $AF_1$ kwa Kidholuo.

Huu ni uchaguzi wa lugha unaotarajiwa na ambao unasababishwa na mabadiliko ya mada katika mazungumzo. Uchaguzi huu unaleta mwingiano baina ya $AF_1$ na $AF_2$ na papo hapo ujitengaji kwa AS. Wanaonyesha mwingiano kama (ndugu) na wanajitenga kiusemi kwa AS wakijitambulisha kijamii.

| | | |
|---|---|---|
| AF2 | – | Habari zenu? |
| AS na AF2 | – | Salama |
| AF2 | – | Naona kuna vitabu mpya vingi? |
| AF1 | – | Ndio, *stock* imeongezwa. |
| AF2 | – | Hata vya hadithi naona mmenunua – kama kile cha Masaibu ya Ndugu Jero. Nakipenda sana. |
| AS | – | Kitabu kizuri hicho, kinafurahisha na kuchekesha. Bei yake rahisi sana. |
| AF2 | – | Unauza aje? |
| AF1 | – | Bei imeandikwa, karibia uone. |
| AF2 | – | **nyoro nawuok dala ing'eyo?** (Jana nilitoka nyumbani unajua?) Kiswahili sanifu - unajua nilitoka nyumbani jana? |
| AF1 | – | **gin nade?** |

(Wako aje?)

AF2 – **.... maber**

(mambo sawa)

Kiswahili sanifu- mambo sawa

**Mamau emane oora**

(Mama yako ndiye alinituma)

Kiswahili sanifu -mama yako alinituma kwako.

AF1 – **Ang'o mane oori**

(Nini ndio alikutuma)

Kiswahili sanifu -Alikutuma nini?

AF2 – **nyithindo emane oviembi**

(Watoto ndio walifukuzwa)

**Skul koro iore pesa dala.**

(Shule kwa hivyo utume pesa nyumbani)

Kiswahili sanifu- Alisema upeleke pesa nyumbani kwa sababu watoto wamefukuzwa shuleni.

**Mfano 4.3.20**

Haya ni mazungumzo baina ya vijana wawili wa Kiafrika wanaozungumza lugha ya Kiluhya na Waasia ($AS_1$ na $AS_2$) wenye duka la kuuzia Vioo .Wote wanaonyesha mwingiano kwa muda kwa kutumia lugha ya Kiswahili lakini baadaye Waafrika wanawatenga Waasia wanapoanza kuongea kwa lugha ya Kiluhya. Kijana mmoja ($AF_1$) ni mfanyikazi na yule mwingine ni mteja. Wanazungmza kwa Kiluhya ili kuficha maovu

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

AF1 aliyoyafanya hapo kazini na ni AF2 peke yake anayeonekana kugundua hayo. $AF_1$ alivunja na kuficha kioo.

Haya yanaambatana na mihimili wa nadharia ya Usawazishaji Usemi ya kujitambulisha kijamii na Kukadiria Gharama kati ya Jamii. AF1 na AF2 wanapotumia lugha ya Kiluhya wanawatenga AS1 na AS2 kiusemi na jambo hilo linawawezesha kuepuka gharama ambayo AF1 angepata akigunduliwa na AS1 na AS2 kuwa amevunja kioo.

AF1 – Karibu sasa.
Ndio umefika?

AF2 – Ndio, nimechelewa
kidogo, sababu ya jam.

AS1 – Sema na *customer,* anataka nini?

AF1 – Anataka kioo *size thirty by fifty.*

AS2 – Enda pande ile umtolee.

AF2 – **Sijali imali ino** yetu).
(usijali mali hiyo ni yetu)

AF1 – **Lakini vamanya Abhaidi ni abhajinga**
(Lakini unajua Wahindi ni wajinga)

AF2 – **Alichuwa ikhupanga abhunaka nende Amuindi alachal abuyaka.**
(Tukionekana tukiongea wataanza kupiga kelele).

AF1 – **Icho jiyoni**
(wewe kuja jioni)

AF2 – **Kubuka akhuvisia imali iriya**

(Kumbuka kuficha mali ile).

Kiswahili sanifu – kumbuka kuficha ile mali.

Lengo kuu la Waasia la kutumia lugha ya Kiswahili ni kuwasiliana na kuafikiana na kundi ambalo ni tofauti kijamii na kiuchumi. Waasia na Waafrika wana lugha tofauti za kwanza kwa hivyo Kiswahili ni lugha inayowezesha mawasiliano kati ya makundi haya mawili. Mawasiliano haya yanajikita katika mahusiano ya kibiashara kwa hivyo lengo kuu ni kuendeleza biashara za Waasia. Kwa hivyo, iwapo Waasia wanabadilisha mtindo wa uneni wanafanya hivi ili kupata faida katika biashara. Faida hii inapatikana kupitia kuwa na wateja wengi na ambao wana uhusiano mwema na mwuzaji. Uhusiano unadumishwa na kule kuwepo na maelewano kupitia namna ya uzungumzaji.

Faida nyingine Waasia wanayolenga kupata ni wafanyikazi ambao watasaidia biashara kuendelea. Kwa hivyo kudumisha wafanyikazi kutakuwepo iwapo mwajiri na mwajiriwa wanaweza kuvutiana kwa kuwepo jambo/kitu kinachowafanya wafanane. Mtindo wa uneni hapa ndio unaowafanya wawe sawa. Kwa hivyo ubadilishaji wa miundo ya sentensi ni muhimu ili wazungumzaji wawe sawa na papo hapo kuvutiana. Hali inavyokuwa hapa ni kwamba Waasia walibadilisha muundo wa Kiswahili wa sentensi nao Waafrika wakafuata muundo uliobadilishwa na kwa kufanya hivyo wakamsaidia Mwasia katika lengo lake kwa sababu jambo hilo limewafanya waelewane.

Inafaa kuwekwa wazi hapo kwamba Waasia walibadilisha muundo wa sentensi katika lugha ya Kiswahili kwa sababu tatu kuu: Moja ni kule kutokuwa na uwezo wa

kuzungumza Kiswahili sanifu kinachozingatia sheria za uundaji wa sentensi sahihi; pili ni jitihada za kutaka kudumisha ule ujitambulishi wa kijamii; na tatu ni kutaka kupata faida za kiuchumi na kijamii – kukubalika nchini Kenya na kuweza kuwasiliana na wenyeji, kunufaika kibiashara kwa kupata na kudumisha wafanyikazi na wateja.

La muhimu sana kutokana na utafiti huu ni kwamba inaelekea kuwa kwa Waasia cheo na hadhi ni jambo lisilochukuliwa kuwa la maana sana kwani walionekana wakithamini shughuli za kiuchumi zaidi ya zile za kijamii.

Wengi wa Waafrika ambao wana mahusiano na Waasia ni wafanyikazi madukani ya Waasia na wateja katika maduka haya. Kama ilivyotajwa awali katika sura hii, Waafrika mara nyingi hujinasibisha kwa muundo wa sentensi katika launi ya Kiswahili ya Waasia . Wengi wa Waafrikka hawa ni wa hadhi ya chini wakilinganishwa na Waasia kwa hivyo inatarajiwa aliye katika hadhi ya chini ajisawazishe kwa yule mwenye hadhi ya juu. Waafrika wamefanya hivyo kwa sababu wanatarajia kupata manufaa kama vile uhusiano mwema na waajiri na zaidi cheo kazini, kudumisha kazi kwa wanaofanya kazi kwa Waasia na kwa upande wa wanunuzi kupata bidhaa kwa bei nafuu. Kuna wakati ambapo sheria hii imevunjwa pale ambapo Waafrika matajiri na ambao ni wateja katika maduka ya Waasia wanapojisawazisha kiusemi kwa Waasia kwa kutumia muundo wa sentensi katika launi ya Waasia ya Kiswahili. Ingawa Waafrika hawa wanaelewa kwamba wao ni wa hadhi ya juu kiuchumi, wanajisawazisha kiusemi kwa sababu wanaelewa kuna faida kupitia kufanya hivyo (kupata bidhaa kwa bei nafuu).

Jambo lingine linalojitokeza kuhusiana na usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika katika kiwango hiki cha sintaksia ni kwamba baadhi ya sentensi katika launi ya Kiswahili ya Waasia zinadhihirisha kiwango fulani cha utata katika kuzifasili maana.

**Mfano 4.3.21**

Tazama sentensi zifuatazo.

1. Malinge kama nasikia mimi iko naita veve.
2. Kayana hii kama nataka kazi iko nasema mimi iko napea wewe.
3. Hii nguo kamata mimi namempa veve.
4. Kama nalaleni hapana nagoja pesa mezi hii.
5. Apana kamata fagio bure, toa fagio.
6. Iko sema nini?
7. Apana kuchukua mzee, mzee nalikuwa pande ingine.

Baadhi ya sentensi katika mfano 4.3.21 zinaweza kuchukuliwa kuwa zenye utata, sio tu wa kimaana mbali kuhusiana na upangaji unaoleta uhusiano kati ya maneno.
Sentensi 1, 4, 5 na 7 ni tata kimaana, tena ni vigumu kuzichanganua kwa kuzingatia kategoria za maneno.

Kwa hivyo kwa jumla tutasema hakuna ukawida katika usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Wafrika katika kiwango cha sintaksia kwa sababu hakuna ruwaza maalumu ya virai katika sentensi katika Kiswahili cha Waasia. Tena, aina tofauti za maneno (nyingine zikitumiwa kimakosa) zinatanguliza sentensi.  Kinachojitokeza wazi hapa ni kwamba

muundo wa sentensi katika launi ya Kiswahili inayotumiwa na Waasia ni tofauti na muundo wa sentensi katika Kiswahili sanifu. Zaidi muundo huu tofauti ndio unaopatikana ukitumiwa na Waasia na Waafrika katika maingiliano ya ana kwa ana.

## 4.4 HITIMISHO

Katika sura ya nne tumefafanua hali inavyokuwa katika maingiliano ya Waasia na Waafrika kuhusiana na usawazishaji wa usemi katika kiwango cha sintaksia. Imebainika hapa kwamba mwingiano na ujitengaji ni baadhi ya mambo yanayojitokeza. Waasia waliweza kuonyesha maingiano lakini mwingiano huu utachukuliwa kuwa mwingiano – kinyume katika kiwango cha sintaksia kwa sababu ingawa walitumia Kiswahili kuwasiliana na Waafrika hawakutumia muundo wa sentensi katika lugha ya Kiswahili. Walibuni muundo wa sentensi ili kuwasiliana na Waafrika. Inakisiwa kuwa muundo huu wa sentensi katika launi ya Kiswahili ya Waasia ulisababishwa na athari za lugha za kwanza.

Hali hii haiwezi kuchukuliwa kama ujitengaji kiusemi kwa sababu lugha inayotumika ni Kiswahili. Kwa kiwango ingawa kidogo zaidi Waasia walionyesha mwingiano-chanya pale ambapo baadhi yao walitumia miundo ya sentensi katika lugha ya Kiswahili.

Kwa upande wa Waafrika, jambo linalojitokeza ni kwamba wengi wao waliweza kuepuka muundo wa sentensi katika lugha ya Kiswahili kila walipokuwa wakiwasiliana na Waasia. Hii ina maana kuwa walijisawazisha kiusemi katika kiwango cha sintaksia

kwa Waasia. Waafrika walionyesha mwingiano wa kiwango cha juu wakilinganishwa na Waasia.

Kwa jumla mwingiano na ujitengaji baina ya Waasia na Waafrika uliletwa na jitihada za kutaka kupata faida za kiuchumi na kijamii.

Ujitengaji ulibainika pale ambapo Waafrika walitumia lugha za kwanza wasikilizaji wakiwa Waasia. Hali kadhalika Waasia walijitenga kiusemi katika kiwango hiki kwa kutumia lugha zao za kwanza wasikilizaji wakiwa Waafrika.

# SURA YA TANO

## 5.0 MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 UTANGULIZI

Sura ya tano imegawika katika sehemu tatu: sehemu ya kwanza ni muhtasari wa utafiti kwa jumla. Sehemu ya pili inahusu matokeo ya uchunguzi katika kila sura na mahitimisho yake. Mwisho katika sura hii, ni mapendekezo kuhusiana na utafiti huu.

## 5.2 MUHTASARI WA UTAFITI

Utafiti huu ulinuia kuchunguza usawazishaji wa usemi katika hali rasmi ya kikazi, jijini Nairobi. Utafiti ulijikita katika maingiliano baina ya Waasia waajiri na Waafrika wafanyakazi na wanunuzi. Madhumuni ya utafiti yalikuwa ni kuchunguza na kutambua viwango vya kiisimu hasa vya kisemantiki na kisintaksia vya usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika. Pia utafiti huu ulijishughulisha na sababu zinazowamotisha wazungumzaji kubadili usemi. Kwa kutumia nadharia za Usawazishaji Usemi, Upekee na Sarufi Miundo Virai, matumizi ya lugha katika viwango vya semantiki na sintaksia baina ya Waasia na Waafrika yalifafanuliwa. Ilibainika kuwa usawazishaji wa usemi ulimotishwa na mwingiano, ujitengaji, uchaguzi wa kipekee na usio wa kipekee na mwishowe ubahatishaji.

## 5.3 MATOKEO NA MAHITIMISHO

Jambo ambalo limejitokeza kupitia utafiti huu ni kwamba Waasia na Waafrika katikati mwa jiji la Nairobi hujisawazisha kiusemi. Imebainika kwamba usawazishaji wa usemi ni bayana katika viwango vya semantiki na sintaksia.

Katika kujisawazisha kiusemi katika kiwango cha semantiki Waasia walionyesha ubunifu pale ambapo waliweza kutumia maneno ambayo kimaana ni tofauti na Kiswahili sanifu. Ubunifu huu ulibainika kupitia ufupishaji, ujumuishi na urahisishaji wa maneno katika mazungumzo. Inakisiwa kuwa jambo hili linatokana na kule kutokuwa na umilisi wa kutosha wa lugha ya Kiswahili kwa upande wa Waasia. Waafrika walionekana wakijinasibisha kwa msamiati uliobuniwa na Waasia kama ishara ya mwingiano. Hali kadhalika, nao Waafrika waliweza kubuni maneno katika mazungumzo na ambayo yalitumika katika kujitenga kiusemi kwa Waasia. Hata hivyo, wakati mwingine Waasia waliweza kujinasibisha kwa msamiati uliobuniwa na Waafrika.

Katika kiwango cha sintaksia Waasia waliweza kutumia Kiswahili ambacho kinatofautiana na Kiswahili sanifu. Baadhi ya tofauti hizi ni pamoja na matumizi ya miundo ya sentensi iliyolazimishwa, matumizi ya sentensi zilizofupishwa na wakati mwingine zilizorefushwa, matumizi ya sentensi zinazoanza kwa vielezi, viunganishi, vikanushi na vionyeshi. Hali kadhalika katika kiwango cha sintaksia, Waasia walionyesha kutokuwa na umilisi wa lugha ya Kiswahili pale ambapo walitumia sentensi ambazo kwa wazi hazidhihirishi upatanishi wa kisarufi, urejeshi na kauli tendwa ambao unazingatiwa katika muundo wa sentensi katika Kiswahili sanifu. Zaidi Waasia walijitenga kiusemi na Waafrika kwa kutumia lugha za Kiasia ambazo zinazingatia miundo ya sentensi tofauti na Kiswahili sanifu. Mara kwa mara, Waafrika walionekana wakijinasibisha kwa muundo wa sentensi uliobuniwa na Waasia. Kwa upande mwingine, Waafrika walionyesha ujitengaji kiusemi kwa Waasia walipotumia miundo ya sentensi

katika lugha za kwanza ambayo ni tofauti na muundo wa sentensi katika launi ya Kiswahili ya Waasia.

Kwa mujibu wa nadharia ya Usawazishaji Usemi, Waasia na Waafrika walibadilisha lugha iwapo walidhamiria kufanana ndiposa wavutiane mmoja kwa mwingine. Wazungumzaji pia walibadilisha lugha kama ishara ya kutaka kukadiria gharama kati ya wanajamii na kujitambulisha kijamii.

Hali kadhalika ubadilishaji wa lugha kati ya makundi haya ya wazungumzaji ulisababishwa na ile hali ya uchaguzi wa lugha wa kipekee, usio wa kipekee na ubahatishaji kama inavyodaiwa katika nadharia ya Upekee.

Uchaguzi wa lugha kuambatana na nadharia ya Usawazishaji Usemi na nadharia ya Upekee ulikuwa ni jitihada za kupata manufaa na kuepuka gharama inayotarajiwa na washiriki. Waasia walilenga kupata faida kama vile kuuza zaidi, kukubalika na Waafrika, kupata na kudumisha wafanyakazi na wanunuzi. Walionyesha mwingiano ili kupata faida hizi. Waasia walilenga kuepuka gharama ya kupoteza nafasi mahsusi katika kikundi na jitihada katika lugha. Jambo hili lilisababisha Waasia wajitenge kiusemi kwa Waafrika.

Hali kadhalika Waafrika walitazamia kupata faida kama vile nyongeza ya mshahara, uhusiano mwema na waajiri wao na pia kununua bidhaa kwa bei nafuu. Waliweza kujitenga kama ishara ya kutaka kujitambulisha kijamii.

Kando na kujitenga ili kufidia mahitaji binafsi wazungumzaji, walijitenga ili kupata manufaa kibiashara na kuepuka kununua bidhaa kwa bei ya juu au kuwapoteza wateja pale ambapo matumizi ya lugha ya Kiswahili haikufaa katika shughuli kama hii. Katika hali kama hii uchaguzi wa kipekee ulifaa zaidi. Uchaguzi usio wa kipekee ulifaa pale ambapo shughuli ilihusu washiriki kutoka kabila tofauti lakini wanaelewana kwa kutumia Kiswahili. Pale ambapo vyeo na hadhi za washiriki hazikuwa zinabainika wazi, kanuni bahatishi ya uchaguzi ilitumika.

## 5.4 MAPENDEKEZO

1. Utafiti huu umechunguza aina ya Kiswahili ambayo imeibuka nchini Kenya na ambayo ina uwezo wa kuathiri ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili shuleni na vyuoni. Ujuzi wa Kiswahili hiki ni mwafaka kwa wakuza mitaala ili kuibua nadharia na mbinu mwafaka katika ufundishaji wa Kiswahili sanifu. Kwa hivyo utafiti zaidi kuhusiana na aina hii ya Kiswahili ni muhimu.

2. Utafiti wetu umechunguza usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika katika viwango vya semantiki na sintaksia. Utafiti zaidi kuhusiana na makundi haya lakini katika viwango vingine vya kiisimu kama vile pragmatiki, leksia na sarufi utafaa katika kutoa habari zaidi kuhusu usawazishaji wa usemi.

3. Tumefanya utafiti katika hali rasmi za kibiashara katika maeneo ya mjini. Labda utafiti wa aina hii katika maeneo yasiyo rasmi utaleta matokeo tofauti. Kiswahili sanifu na launi ya Kiswahili ya Waasia zimezingatiwa. Pengine katika mazingira

yasiyo rasmi matokeo ya utafiti huu yanaweza kuwa tofauti na utafiti wa aina hiyo. Tena katika hali zisizo rasmi mambo yanaweza kuwa vingine.

4. Viziada lugha ni baadhi ya mambo ambayo wakati mwingine huandamana na mawasiliano. Katika utafiti huu Waasia na Waafrika walionekana wakijisawazisha mmoja kwa mwingine kwa kutumia viziada lugha ingawa jambo hili halikushughulikiwa kwa hivyo utafiti unaoangalia usawazishaji wa viziada lugha utaangazia / unaweza kutoa data muhimu kwa wanaisimu na wanasaikolojiaisimu.

5. Utafiti huu ulichunguza utaratibu wa usawazishaji wa usemi kati ya Waasia na Waafrika kwa kutumia nadharia tatu: Usawazishaji Usemi, Upekee na Sarufi Miundo Virai. Utafiti ambao utajumuisha nadharia zaidi na tofauti kama vile nadharia ya Uamilifu na nadharia ya Utofauti unaweza kusaidia kufafanua zaidi usawazishaji wa usemi na kwa kufanya hivyo utoe data muhimu kwa wanaisimu na wanasaikolojiaisimu.

# 6.0 MAREJELEO


Abdulaziz, M. (1982). Patterns of Language Acquisition and Use in Kenya; Rural and Urban Differences. An Introduction to Language and Communication", International Journal on Language & Society 34 pp. 95 – 120 Mouton Publishers.

Agheyisi, R (1977). Language Interlarding in the Speech of Nigerians. In P.F.A Kotey & H. Der Houssikian (eds). Language and Linguistic Problems in Africa. Columbia SC.

Akhamanova, O. na Mikael'an, G. (1969). The Theory of Syntax in Modern Linguistics. The Hague: Mounton & Co. N.V Publishers.

Amutabi, M (2002) "Globalisation and the Mainstreaming of Kiswahili Research in 21st Century" katika Utafiti wa Kiswahili. Eldoret: Moi University Press.

Appel, R. and Muysken, P. (1987) . Language Contact and Bilingualism. London: Edward Arnold Publishers.

Cook, G. (1989). Discourse. Oxford: Oxford University Press.

Crystal, D. (1985). A Dictionary of Linguistics and Phonetics. Oxford: Basil Blackwell.

Deshpande, M..M. (1979) Sociolingustic Attitudes in India. An Historical Reconstruction. USA Karoma Publishers, Inc.

Doughty, P. (1971). Language in Use. London: Edward Arnold Publishers.

Deo Ngonyani (2003). "Swahili Language" Ethnologue Report for Language Code: Languages of the World. SIL International.

Fasold, R. (1984). The Socio- Linguistics of Society .England : Basil Blackwell

Finch, G. (1997). How to Study Linguistics. A Guide to Understanding Language 2nd ed. Great Britain: Palgrave Macmillan.

Fowler, R. (1971). The Languages of Literature. London and Henley: Routledge and Kegan Paul Ltd.

Gachinu, N. (1996) "Linguistic Aspects of Codeswitching in Kikuyu , Kiswahili and English" Unpublished M.A Thesis, Kenyatta University.

Giles, H. (1973). Accent Mobility: A Model and Some Data: Anthropological Linguistics, 15, 87-105.

Giles, H & Powesland, P.F (1975). Speech, Style and Social Evaluation. London Academic press.

Giles, H. (ed) (1977). Language, Ethnicity and Inter-group Relations. London; Academic Press.

Giles,H. and St. Clair, R. (eds) 1979). Language and Social Psychology . Oxford: Basil Blackwell.

Giles, H.& Robinson P. and Smith P. (Eds) 1980). Language and Social Psychological Perspectives. New York : Pergamon Press.

Giles ,H.&Hewstone,M.(1982) Cognitive Structures,Speech and Social Situatians:Two Intergrative Models. Language Sciencies, 4 187-219

Giles, H. and Robinsons, P. (eds). (1990) Handbook of Language and Social Psychology. England: John Wiley and Sons.

Gregory, M. (1978). Language and Situations: Language Varieties and their Social Contexts. London; Routledge and Kegan Paul Ltd.

Grice, H. (1975). Logic and Conversation in P. Cole and Morgan ( Eds ) , Syntax and Semantics. New York: Academic Press.

Grosjean, F. (1982). Life With Two Languages: An Introduction to Bilingualism. Cambridge, M.A: Harvard University Press.

Gumperz, J. (1982). Discourse Strategies. Cambridge: Cambridge University Press.

Guthrie,M.(1967). Comparative Bantu :An Introduction to the Comparative Linguistics and Prehistory of the Bantu Languages. Amersham: Gregg Press Ltd,England.

Hammers, J. and Blanc, M. (1982)."Towards a Social - Psychological Model of Bilingual Development". Journal of Language and Social-Psychology, 1,29-49.

Hornby, P.A (ed.) (1977). Bilingualism. Psychological, Social and Educational Implication. New York: Academic Press. Inc.

Hymes, D. (1972). Models of the Interaction of Language and Social Life: In J.J Gumperz and D. Hymes (eds.). Directions in Sociolinguistics. New York: Holt Rinehart and Winston.

Kanana, F.E. (2003). " Codeswitching in Business Transactions: A Case Study of Linguistic Repertore: In Maasai Market in Nairobi , Kenya" Unpublished M.A Dissertation, Kenyatta University. Kenya.

Kebeya, H. (1997). "Investigating Linguistic Accommodation Between Two Luhya Dialects: Logooli and Lwitakho", Unpublished M.A Thesis, Kenyatta University. Kenya.

Labov, W. (1972). Sociolinguistic Patterns. Oxford: Basil Blackwell.

Laver, J. (1994). Principles of Phonetics. Cambridge: Cambridge University Press.

Lyons, J. (1981). Language and Linguistics. An Introduction. Cambridge: Cambridge University Press.

Massamba, D.P.B Kihore, Y.M na Hokororo, J.I. (1999). Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA) Sekondari na Vyuo . Dar-es-Salaam TUKI

Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M. (2001). Sarufi Miundo ya Kiswahili (SAMIKISA) Sekondari na Vyuo. Dar –es- Salaam TUKI

Massamba, D.P.B. (2002). Historia ya Kiswahili. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mathooko, P.M. (2004). "Towards an Integrative Perspective of Linguistic Accommodation: A Case of Kikamba and Kitharaka." Unpublished Ph.D Thesis, Kenyatta University Kenya.

Mbaabu, I. (1985). New Horizons in Kiswahili. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mbaabu, I. (1992) . Sarufi ya Kiswahili . Nairobi: Longman Publishers

Mesthrie, R. Swann, J. Deumert, A. & Leap, W. (2000). Introducing Sociolingustic. Edinburg: Edinburg University Press.

Mgullu, S. R. ( 1999). Mtaala wa Isimu . Nairobi Longman Publishers

Milroy, L. and Muysken, P.(Eds.) (1995). One Speaker Two Languages : Cross-Discipline Perspective on Code Switching. Cambridge: Cambridge University Press.

Moscovici, S. (1967). Communication Processes and the Properties of Language in Advances in Experimental Social Psychology 3, 226 – 270.

Mugenda, O. and Mugenda A. (1999). Research Methods: Quantitative and Qualititive Approaches Nairobi: ACTs.

Munyua, J.G. ( 2002). The Emerging Viswahili and Kiswahili Research, katika Utafiti wa Kiswahili . Eldoret : Moi University Press.

Muthuri, G. (2000). " Functions of Codeswitching among Multilingual Students at Kenyatta University.Unpublished M.A. Thesis ,Kenyatta University,Kenya.

Muthwii ,M.J. (1994). "Variability in Language Use: A Study of Kalenjin Speakers of English and Kiswahili in Kenya" Unpublished Ph.D Thesis; University of East Anglia, Norwich.

Mutugu, B.N. (2001). "Makosa ya Kileksia katika Insha na Chanzo Chake . Uchunguzi wa Shule Tano za Upili Wilayani Kiambu . Tasnifu isiyochapishwa ya Uzamili , Chuo Kikuu cha Kenyatta . Kenya

Neale, B. (1974). "Kenya's Asian Language". In Whiteley, W (ed) 69-86.

Parkin, D.J (1974). "Language Shift and Ethnicity in Nairobi. The Speech Community of Kaloleni" in W.H Whiteley (Ed) Language in Kenya, P.P 189-210 Nairobi: Oxford University Press.

Polome E.C. (1982). Language, Society and Paleoculture. Stanford: Stanford University Press.

Romaine ,S. (Ed) (1982). Sociolinguistic Variation in Speech Communities.London: Edward Arnold

Romaine, S. (1984). The Language of Children and Adolescents. New York: Basil Blackwell.

Russell, J. (1982). "Networks and Sociolingustic Variation in an African Urban Setting" in Romanie, S. (ed) 125 –140).

Russell, S.T (1986). Basic Word Order: Functional Principles. Beckenham, Ken't: Croom Helm.

Scherer, K.R. and Giles, H (eds.) (1979). Social Markers in Speech. Cambridge: Cambridge University Press.

Scotton, M. (1983b). "The Negotiation of Identities in Conversation: A Theory of

Markdress and Code Choice" International Journal of Sociology of Language. 44.115-136.

Scotton, C. (1993). Social Motivations for Codeswitching: Evidence from Africa. Oxford: Clarendon Press .

Searle, J.R. (1979). Expression and Meaning. Studies in the Theory of Speech Acts. Cambridge: Cambridge University Press.

Simpson, G.B. (1991). Understanding Word and Sentence. Amsterdam: Elsevier Science Publishers.

Trudgill, P. (1974). Sociolinguistics. An Introduction to Language and Society Harmondsworth: Penguin Books Limited

Trudgill, P. (1986). Dialects in Contact. Oxford: Basil Blackwell.

Tumbo, Z.N.Z., Massambo na Mdee, J.S (Wah.) (1999). Mulika . Na 25.

Wallwork, J.F. (1985). Language and Linguistics: An Introduction to the Study of Languages. London: Heinemann Educational Books Ltd.

Whiteley ,W.H (ed) (1974). Language in Kenya. Nairobi: Oxford University Press.

Wierzbicka, A. (1996). Semantics. Primes and Universals. Oxford: Oxford University Press.

Yule, G. (1996). Pragmatics. London: Oxford University Press.

**VIAMBATISHO**

Mazungumzo kuhusu usawazishaji wa usemi:

Kiambatisho 1

Mwingiano

1. Mazungumzo yanahusu Mwasia (As)mzee mwenye duka la kuuzia mapambo na Mwafika (AF) mzee mfanyakazi.

AS – kuja pande hii.

AF – unasema nini?

AS – **nataka kutia** veve **maneno**
iko nasikia?

AF – **unataka kutia maneno** gani?

AS – Kesho nataka wewe aingie subui sana.
Shauri mimi tatumia veve
kachukue masigo ya kazi.

AF – unataka nikuchukue masigo wapi?

AS – Kama veve nakuja mimi tamambia
veve, iko sikia?

AF – Mimi hapana iko shinda ya kuingia kazini mapema.
Wewe tapate
mimi hapa.

2. Mazungumzo haya yahahusu Mwafrika (AF) mteja katika duka la kuuzia viatu na Mhindi (AS)

AF – Habari ya leo?

AS – Iko salama.

AF – Hii kiatu rangi nyeusi iko?

AS – Iko.

Namba **ngapi taka?**

AF – *Nine* au nane…………

**Gapi bei** yake ?

AS - Tausia veve na mia nane.

Kiambatisho 2

Ujitengaji

Mazungumzo haya yanahusu Waasia

Wawili (AS1 na AS2) na Mwafrika (AF)

AF – Hii *material* taweka wapi?

AS1 – Enda juu, alafu weka musuri pale.

AF – Hapana weza peke yangu.

(AS1 kwa AS2)

AS1 – **Fe manas adsu chhe**

(huyu mtu mzembe)

AS2 – **Tene yo**

(Hebu muone)

Kiambatisho 3

Uchaguzi wa lugha wa kipekee.

1. Haya ni mazungumzo baina ya Mwasia kijana (AS1) , Mwasia mzee (AS2) na Mwafrika mzee (AF) katika duka la kuuzia vyuma vya magari.

| | | |
|---|---|---|
| AF | – | *customer* anataka chuma ya mzunguko. |
| AS1 | – | Angalia pale. |
| AF | – | Hakuna ya mzunguko. |
| AS1 | – | (kwa AS2) |
| | | Iko na **rounded pistol?** |
| AS2 | – | **yes, check the other** |
| | | **side, below the shelves.** |
| | | (AS1 kwa AF) |
| | | Kuja , shika patia *customer*. |

2. Mazungumzo yafuatayo yanahusu vijana wawili wa Kiafrika (AF1 na AF2) na Mwasia(AS) mwenye duka la kuuzia vioo.

| | | |
|---|---|---|
| AS | – | Leo kazi baya. |
| AF | – | Hio ni kawaida, mwezi ni baya, tarehe ishirini? |
| AS | – | Lakini *customer* etu mingi iko torokea sisi. |
| | | (AF2 anaingia dukani na kuingilia mazungumzo ya AS na AF1) |
| AF1 | – | Karibu *customer,* |
| | | **umunthi wienda kuthooa ki?** |
| AF2 | - | **nienda kioo,** *size* kubwa. |

AF1 – Iko ndio hii.

AS – (kwa AF1)

*Customer* iko taka nini?

AF – Anataka kioo ile kubwa.

Kiambatisho 4.

Uchaguzi wa lugha usio wa kipekee

1. Mazungumzo yafuatayo yanahusu wazee wawili, Mwasia (AS) na Mwafrika (AF) katika kiduka cha maonyesho ya vyakula vya asili ya Bara Hindi.

AS – Kamata ii karatasi, weka karibu na malango,

*Customer* apana ona mzuri. Taonyeshe *customer* njia.

AF – Kweli, sasa hii karatasi itaonyeshea *customer*, wanauliza mashwali mingi?

Sasa C*ustomer* ataelewa.

AS – Mimi iko taka veve naenda pale kwa Patel, namuliza yeye aandike karartasi mingi shauri ya io kasi.

AF – *Customer* wakiwa wachache nitaenda, sana sana saa nane.

2. Mazungumzo yafuatayo yanahusu Mwasia kijana (AS) na Mwafrika kijana (AF) katika duka la Mwasia la kuuzia dawa.

AF – Stock mpya italetwa lini?

AS – Ya nini?

AF – Ya dawa aina ya Epanutin…

ile ya generic? Iko watu wengi wanaotaka.

AS – Ni watu gapi wanaotaka?

AF – *Customer* karibu nne sasa wameuliza.

AS – Yule tauliza mambie yeye akuje jioni. Mimi iko enda kuchukua saa ii.

Kiambatisho 5

Uchaguzi wa lugha bahatishi

Mazungumzo haya yanahusu Mwafrika (AF) mteja na Mwasia (AS) mwenye duka la kuuzia nguo.

AS – Karibu customer.
Iko taka……**what can I do for you**?

AF – Nataka nguo, ile ya wanawake na watoto

AS – Yote ilo, karibu dani uone.

AF – Nataka nyingi………..**I don't know whether the price is the same for wholesale** na mojamoja?

Kiambatisho 6

MAHOJIANO YASIYO RASMI: MASWALI YA MWONGOZO.

- Kwa Waasia

1. Wafanyakazi (wasaidizi katika kazi) wako ni wa asili gani?

   (a) Afrika______________________

   (b) Bara Hindi________________

   (c) Kwingineko (eleza)__________

2. Unatumia lugha gani kuwasiliana nao?

(a) Kiswahili_______________

(b) Kiingereza_____________

(c) Lugha nyingine (eleza)_______

3. Matumizi ya lugha ni sawa kwa wafanyakazi wote au inategemea?

(a) Umri_______________

(b) Uana_______________

(c) Cheo_______________

4. Kwa nini unachagua kutumia lugha hiyo (katika jibu 2)

_________

_________

_________

5. Wateja wako ni wa asili gani ?

(a) Afrika__________.

(b) Bara Hindi_______

(c ) Kwingineko (eleza) __________

6. Unatumia lugha gani kuwasiliana nao?

(a) Kiswahili_____________

(b) Kiingereza ____________

(c) Lugha nyingine (eleza)___________

(d) Mchanganyiko wa lugha (eleza zipi)__________

- Kwa Waafrika

1. Unatumia lugha gani kuwasiliana na mwajiri wako?

    (a) Kiswahili___________

    (b) Kiingereza___________

    (c) Lugha nyingine (eleza)_________

2. Kwa nini unachagua kutumia lugha hiyo (jibu katika 1)?

    (a)__________

    (b)__________

    (c)_________

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY